CHAGUO LA WANANCHI

TAARIFA YA TUME YA MAREKEBISHO YA KATIBA YA KENYA

TOLEO FUPI

Imewekwa tarehe, kupigwa muhuri na kutolewa rasmi Jumatano Septemba 18, 2002, saa nne asubuhi, Jijini Mombasa

YALIYOMO

TARATIBU WA MATUKIO YA TUME iv
SURA YA KWANZA 1
UTANGULIZI 1
1. Msingi wa Marekebisho 1
Nini Kitakachotendeka Baadaye? 2
2. Utaratibu 3
(a) Malengo na Maadili 3
(b) Elimu Ya Uraia: Kuwatayarisha Wananchi Kushiriki 4
(c) Kuwasikiliza Wananchi 5
(d) Uchanganuzi wa Mawasilisho ya Wananchi 5
(e) Kujitayarisha, Kuandika Ripoti Na Mswada Wa Katiba 6
f.) Hitimisho la Kuhusu Utaratibu wa Marekebisho 7
3. Tuliyoambiwa Na Wananchi: Muhtasari 8
4. Tuliyojaribu Kutekeleza Katika Katiba Mpya 13
(a) Usawa Na Ulinganifu 15
b.) Haki za Binadamu 19
c.) Usalama 19
d.) Kuilinda Katiba Na Kanuni Zake 19
e.) Tuwasikilize Wananchi 19
5. Waraka wa Katiba 20
a.) Mtindo Wa Kuutayarisha Mswada Wa Katiba 20
b.) Muundo wa Katiba 21
SURA YA PILI **25**
MSWADA WA KATIBA **25**
MAADILI, KANUNI, HAKI NA SERA **25**
1. Utangulizi 25
2. Maadili Na Matumaini Ya Taifa 25
3. Watu wa Kenya 26
Mawasilisho kwa Tume 27
4. Haki za Binadamu 28
Mswada Wa Katiba Unawafanyia Nini Watoto? 31
5. Ardhi, Mazingira, Uchumi na Maliasili 33
Mambo ambayo Tume Iliambiwa na Wananchi Kuhusu Ardhi 34
6. Mazingira 35
Uchumi 38
7. Fedha za Umma 38
8. Kenya na Ulimwengu 40
SURA YA TATU **43**
MSWADA WA KATIBA **43**
UTARATIBU NA ASASI ZA SERIKALI **43**
1. Bunge Na Wabunge 43
Ukumbi mmoja wa Bunge ama Kumbi Mbili? 45
2. Uwakilishi wa Wananchi: Utaratibu wa uchaguzi 46

3. Vyama Vya Kisiasa 49
4. Rais, Waziri Mkuu na Mawaziri: 51
Rais 55
Waziri Mkuu 58
5. Serikali Ya Uwezo Uliopunguzwa na Serikali ya Wilaya 58
Kuunda Sheria katika Viwango Tofauti 59
6. Uchaguzi wa Rais, Bunge, Baraza la Kitaifa na Mamlaka Zilizosambaziwa uwezo 59
7. Mahakama na Mfumo wa Mahakama 60
a.) Matumaini 61
Mifumo mipya ya Mahakama 64
b.) Mahakama za Kadhi 64
c. Uwajibikaji na Udhibiti 66
d.) Hatua za Mpito 67
8. Mambo Mengine Kuhusu Mfumo wa Sheria 68
9. Mfumo wa Kuadhibu 68
10. Huduma kwa Umma, Polisi na Jeshi la Ulinzi 69
a.) Huduma kwa umma 69
b.) Huduma za Usalama 71

SURA YA NNE 75
UKATIBA 75
1. Mambo Ambayo Wakenya Waliiambia Tume 77
2.) Vyombo Vya Kikatiba Vilivyopendekezwa 78
a.) Tume ya Maadili na Uaminifu 79
b.) Tume Ya Uchaguzi 80
c.) Kamati Ya Mishahara na Malipo 80
d) Tume ya Hazina ya Upunguzaji na Usambazaji Madaraka 80
e.) Tume Ya Katiba 80
f.) Mahakama 80
g) Mkuu wa Sheria 80
g) Mkurugenzi wa Mashtaka 80
h.) Wakili wa Umma 80
m.) Msimamizi wa Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fedha 81
n) Mhasibu mkuu na Afisi ya Kitaifa ya Uhasibu 81
o.) Mkurugenzi wa Shirika Kuu la Takwimu 81
p.) Tume ya Ardhi 81
3. Kanuni Zinazoongoza uundaji wa Tume Huria 81
4. Rais Kama Mlinzi Wa Katiba 82
5. Kubadilisha Katiba 82

SURA YA TANO 83
MPITO 83
1. Kudumisha ya Kale 83
2. Kuleta Mapya 83
HITIMISHO 84

DIBAJI

Tume ya Marekebisho ya Katiba ya Kenya ina furaha kuichapisha na kuitangaza taarifa hii ya kazi yake, na mapendeke zo kuhusu Katiba mpya. Toleo refu lenye juzuu tatu, litachapishwa na kutangazwa hivi karibuni. Wakati huo huo kwenye waraka huu, kuna taarifa ya vikao vya maeneobunge mia mbili na kumi (210) ya kikatiba, ambavyo viliwajibika kuwahamasisha na kuwashawishi wananchi katika maeneo yao ya bunge kushiriki kwenye marekebisho. Mswada wa sheria kuhusu Katiba mpya umeandaliwa na utachapishwa mnamo tarehe 25 Septemba 2002. Pamoja na machapisho haya, Tume itakuwa imekamilisha kazi yake kubwa, ambayo ilikuwa ni kufanikisha elimu ya uraia, kuwasikiliza Wakenya na kutoa mapendekezo kwa minajili ya marekebisho ya Katiba. Taarifa yetu na mapendekezo inatolewa kwa umma ili wasome na kutoa maoni yao kabla ya kuanza Kikao cha Kitaifa cha Katiba mwishoni mwa Oktoba, 2002 na kuijadili, kuifanyia masahihisho na marekebisho kisha kuipitisha pamoja na mswada wa Katiba. Licha ya matatizo makubwa pamoja na majaribu ya ndani na nje yaliyokumba taratibu za kazi, tume haikujali bali ilijitahidi zaidi kikazi na kutimiza wito pamoja na lengo kwa kadri ya uwezo wetu.

Ni heshima kubwa kwa Tume kutunukiwa ama kuaminiwa kuifanya kazi hii. Imetambua umuhimu mkubwa wa kuwapo kwa Katiba Mpya wakati ambapo awamu ndefu ya kazi ya urais wa Rais Daniel arap Moi inapofika kikomo na wakati Wakenya wanapotazamia maisha mapya ya baadaye. Tumesikiliza kwa makini maoni ya Wakenya kote nchini. Tumeguswa na kusikitishwa na maelezo yao, na kugundua busara nyingi kwenye mapendekezo.yao.Tumechambua maendeleo ya kijamii,kisiasa,kiuchumi na kikatiba nchini Kenya kwa miongo minne iliyopita,na kujaribu kuwaza na kufikria maisha ya baadaye ambayo kwayo Katiba mpya itatumika.

Kwetu sote wanatume hii pia imekuwa ni safari ya kujitambua.Tumejifunza mengi ambayo hatujayafahamu kuhusu watu na nchi yetu. Ingawa tulishangazwa na kiwango cha umaskini unaowakumba Wakenya wengi,,masikitiko ya kuporomoka kwa uchumi,ukabila katika siasa na ghasia zinazoambatana nazo, tunaamini kuwa tukipata utaratibu unaofaa wa utawala na uongozi mwema unaojali malengo ya umoja na maendeleo yenye usawa, Kenya inaweza kurudia nafasi yake ya awali kama taifa ambalo limeendelea kiuchumi barani Afrika. Tumeweka wazi malengo yetu kwenye taarifa hii tunayotarajia kuyatimiza kupitia mapendekezo yetu kikatiba, yanayowaweka wananchi katika shina la siasa na maendeleo.

Tunafahamu kwamba watu wana matumaini makubwa ya marekebisho na tunaelewa kuwa katiba mpya inatoa ahadi nyingi sana kwao. Tunaamini kwamba ikiwa mapendekezo yetu yatatekelezwa kihaki, ahadi hizo zinaweza kutimizwa. Tunawasihi viongozi wetu, wasiwavunjie wananchi matumaini yao.

Yash Pal Ghai
Mwenyekiti

Septemba 18, 2002

TARATIBU WA MATUKIO YA TUME

Katiba ya sasa ya Tume ya Marekebisho ya Katiba ya Kenya ilitokana na muungano wa taratibu mbili zilizokuwa zinaendelea sambamba. Baada ya serikali na raia kutosikilizana kuhusu utaratibu wa marekebisho, *Kundi la Ufungamano* lilianzisha Tume ya Wananchi wa Kenya (People's Commission of Kenya) kwa kurekebisha Katiba mnamo Juni 2000, chini ya uenyekiti wa marehemu Dkt. Oki Ooko- Ombaka. Mnamo Oktoba 2000 Bunge lilipitisha Sheria ya Marekebisho ya Katiba ya Kenya na, pakaundwa Tume ya Marekebisho ya Katiba yenye wanachama kumi na watano (15) wakiongozwa na Profesa Yash Pal Ghai. Mnamo Machi 2001 maafikiano ya kuunganisha Tume zote mbili yalifikiwa na ilipofika Juni 2001 Sheria ya Marekebisho ya Katiba ilibadilishwa ili kuongeza idadi ya wanachama wa Tume ya Marekebisho ya Katiba, kwa kushirikisha wanachama kumi (10) wa Tume ya Wananchi wa Kenya na wateuzi wawili (2) wa Kamati Teule ya Bunge.

Uteuzi wa awali wa Tume ya Marekebisho ya Katiba ulichapishwa katika gazeti la serikali mnamo Novemba 10, 2000, kama ifuatavyo:

1. Prof. Yash Pal Ghai - Mwanatume na Mwenyekiti
2. Bi. Kavetsa Adagala - Mwanatume
3. Bi. Phoebe Asiyo - Mwanatume
4. Kasisi Zablon Ayonga - Mwanatume
5. Bw. Ahmed I. Hassan - Mwanatume
6. Bw. John M. Kangu - Mwanatume
7. Askofu Bernard N. Njoroge - Mwanatume
8. Dkt Githu Muigai - Mwanatume
9. Prof. H.W.O. Okoth-Ogendo - Mwanatume
10. Bw. Domiziano M. Ratanya - Mwanatume
11. Prof. Ahmed I Salim - Mwanatume
12. Dkt. Mohamed Swazuri - Mwanatume
13. Bw. Keriako Tobiko - Mwanatume
14. Bw. Paul. M. Wambua - Mwanatume
15. Bi. Alice Yano - Mwanatume
16. Mkuu wa Sheria - Mwanatume
17. Bw. Arthur O. Owiro - Mwanatume kwa wadhifa wake na Katibu

Majina ya wanachama kumi wa Tume ya Wananchi wa Kenya yalichapishwa katika gazeti la serikali mnamo Juni 11, 2001:

1. Bw. Abubakar Zein Abubakar
2. Bi. Abida Ali-Aroni

3. Dkt. Charles M. Bagwasi
4. Bi. Nancy M. Baraza
5. Bw. Isaac Lenaola
6. Dkt. Wanjiku M. Kabira
7. Bw. Ibrahim A. Lethome
8. Bi. Salome W. Muigai
9. Dkt. Oki Ooko-Ombaka
10. Bw. Riunga L. Raiji

Wakati huo huo, wafuatao ambao waliteuliwa na Kamati Teule ya Bunge, waliwekwa katika gazeti la serikali:

1. Dkt. Mosonik arap Korir
2. Dkt. Abdirizak A.Nunow

Kati ya Mwezi Juni 2001 na Septemba , 2002, mabadiliko mawili muhimu ya uanachama wa Marekebisho ya Katiba yalitokea. Kwanza, ni kujiuzulu kwa aliyekuwa Katibu wa Tume Bw.Arthur O. Owiro mnamo Agosti 2001, na kuteuliwa kwa Patrick L.O. Lumumba mnamo Oktoba 4, 2001, badala yake. Mnamo Julai 15, 2002 Naibu Mwenyekiti wa Kwanza wa Tume, Dkt. Oki Ooko-Ombaka, alifariki. Nafasi hiyo ilijazwa kwa uteuzi wa Dkt. Andronico O. Adede aliyeingizwa katika gazeti la serikali mnamo Agosti 13,2002.

SURA YA KWANZA

UTANGULIZI

1. Msingi wa Marekebisho

Wakenya walianza kujadili masuala ya kugeuza Katiba mwishoni mwa miaka ya themanini. Mwamko huu wa mageuzo ulianza kwa juhudi na harakati za kubadilisha mfumo wa kisiasa kutoka kwa ule wa chama kimoja na kuuweka mfumo wa kidemokrasia wa vyama vingi. Mwamko huu wa kutaka mageuzo ulitia fora katika miaka ya tisini. Uliwaleta pamoja watu binafsi na mashirika kutoka katika sekta nyingi za jamii na sehemu nyingi za nchi. Waliokuwa katika msitari wa mbele walikuwa mashirika ya kidini, kijinsia na ya haki za binadamu. Mwanzoni, serikali ilipinga wito wa mabadiliko. Lakini, katikati ya miaka ya tisini, serikali iliingia katika mazungumzo na wale waliotetea umuhimu wa mabadiliko kuhusu mbinu za kufuata katika marekebisho ya Katiba. Mkataba ulifikiwa kuhusu malengo na mbinu za marekebisho. Makubaliano haya yaliwekwa katiba mpya ingetenenezwa kwa kuzingatia, ushirika wa wananchi, haki za binadamu na haki za kijamii. Tume ya Marekebisho inayoshirikisha watu wa nyanja tofauti ingeundwa ili kukusanya maoni ya wananchi na kutayarisha mswada wa Katiba ili uzingatiwe na mkutano maalum wa kikatiba.

Ilitokea kwamba, vyama vya kisiasa havikuweza kukubaliana kuhusu muundo wa Tume ya Marekebisho na Mkataba uliowekwa ukavunjika. Juhudi za kutaka mabadiliko ziliendelea lakini harakati za kuibuka na utaratibu wa kitaifa wa marekebisho hazikupatikana. Jamii za kidini, kupitia kikundi cha Ufungamano na kwa kushirikiana na vyama vya kisiasa vya upinzani, jamii za wataalamu na raia, walibuni utaratibu wa marekebisho mnamo Oktoba 2000 kwa kuannzisha Tume ya Wananchi ya Kenya ambayo mwenyekiti wake alikuwa Dkt. Oki Ooko Ombaka na ambayo ingekusanya maoni ya Wakenya na kutayarisha mswada wa Katiba kwa kufuata malengo ya marekebisho ambayo washikadau wote wa awali walikuwa wameyakubali. Kwa upande mwingine, serikali iliufadhili utaratibu mwingine ulioidhinishwa na Sheria ya Marekebisho ya Katiba ya Kenya 2000 (Sheria ya Marekebisho) ambayo kwa kuifuata sheria hii. Bunge na Raisi waliiteuwa Tume ya Kenya ya Marekebisho ya Katiba (CKRC) ambayo mwenyekiti wake alikuwa Profesa Yash Pal Ghai mnamo Novemba 2000. Malengo ya Marekebisho yalibaki vile vile ilivyokuwa katika sheria ya 1998. Pia, japo kwa kushirikisha mabadiliko machache, hatua na asasi za marekebisho zilibaki vile vile.

Kuwepo kwa taratibu sambamba za kupingana, japo zote zilifuata kanuni na malengo ya kufanana za marekebisho kulisababisha mivutano mikubwa miongoni mwa Wakenya. Palitokea wasiwasi katika miondoko ya kisiasa na kijamii na pakawa na hatari ya kutokea ghasia. Isitoshe, hapakuwa na matumaini kuwa mswada wa Katiba ambao ungetokana na kila kikundi

ungekubalika kama sheria kwa sababu hakuna kikundi kilichokuwa na washiriki thuluthi mbili wakiwa wabunge. Ilikuwa muhimu kuwa taratibu za marekebisho zingewaleta Wakenya pamoja, wasuhulishe matatizo yaliyopita na kuibuka na makubaliano kuhusu Katiba mpya ili kuweka nguvu mpya katika kuutumikia umoja wa taifa na kubainisha malengo na sera za kitaifa. Hatimaye Profesa Ghai aliamua kuwashawishi washikadau wote kuja pamoja ili kufanya kazi pamoja. Alianzisha mazungumzo baina ya kikundi cha kamati teule ya bunge kuhusu na cha Ufungamano. Aliungwa mkono kwa wingi na wananchi kote nchini na juhudi hizi zilifua dafu. Mnamo machi 2001 kanuni za kushirikiana baina ya makundi haya mawili zilikubalika. Tume ya Marekebisho ilipanuliwa ili kushirikisha wawakilisi wa Tume ya Wananchi mnamo Juni 2001 baada ya kuibadilisha Sheria ya Marekebisho.

Sheria ya Marekebisho iliweka muda wa miaka miwili (itakayokwisha tarehe 3 Oktoba 2002) ambamo marekebisho ya Katiba yanatarakiwa kukamilika. Mnamo Juni 2002, Tume iliamua ya kwamba haingewezekana kuyakamilisha marekebisho kwa muda uliowekwa na kwa kufuata kifungu 26 (3) cha Sheria wakaliomba bunge liwaongezee muda hadi Juni 2003. Bunge lilikubali waongezewe muda wa miezi mitatu lakini ufike tu Januari 3, 2003. Wakati huo huo, bunge liliibadilisha sheria ili kuufupisha muda wa kushauriana na wananchi na kuijadili ripoti na mapendekezo ya Tume kutoka Siku Sitini (60) hadi thelathini (30) ili kukamilisha utaratibu kwa wakati. Pia iligeuza kanuni ya kupiga kura katika Kongamano la Taifa la Katiba kutoka jumla ya wingi wa kura kwa theluthi mbili hadi theluthi mbili za wale waliopiga kura. Siku ya mwisho iliyowekwa na Bunge ilitwika Tume shinikizo kubwa. Lakini Tume imejitahidi kutekeleza wajibu wake.

Nini Kitakachotendeka Baadaye?

Raia wana siku thelathini (30) za kuijadili ripoti ya Tume na kuutolea Mswada wa Katiba maoni. Kisha, maoni haya yatajadiliwa katika Kongamano la Taifa la Katiba ambalo litaanza kazi yapata mwezi mmoja baada ya ripoti hii kuchapishwa. Kongamano linashirikisha wabunge wote wa sasa, wanachama wa Tume ya Marekebisho ya Katiba ya Kenya (ambao hawapigi kura), mwakilishi mmoja wa kila chama cha kisiasa ambacho kilikuwa kimesajiliwa wakati marekebisho yalipoanza mnamo 2000, watu watatu kutoka kila wilaya (ni mmoja tu wa hawa anayeweza kuwa diwani na ni lazima mmoja wao awe mwanamke), na wawakilishi wa jumuia ya Umma ikiwemo Vyama vya Wanawake, Mashirika ya Kitaaluma, Vyama vya Wafanyi kazi, makundi ya kidini na mashirika mengine yasiyokuwa ya kiserikali. Ni kongamano hili ambalo lina mamlaka ya kutoa uamuzi. Litajadili mswada uliotayarishwa na Tume ya Marekebisho. Linaweza tu kuufanyia mswada mabadiliko iwapo wingi wa thuluthi mbili za washiriki wataafikiana. Mapendekezo ya mwisho yatapelekwa kwenye Bunge ambalo itabidi liyakubali au liyakatae katika ujumla wake (kwa vile wabunge watakuwa wameshiriki katika kongamano hatuoni ni kwa nini wasiukubali mswada utakaokuwa umekubalika huko kama kiwakilishi cha maoni ya wananchi.

2. Utaratibu

(a) Malengo na Maadili

Malengo, asasi, taratibu na hatua za Marekebisho zimeelezwa kwa undani katika Sheria ya Marekebisho. Malengo ya utaratibu huu yanawakilisha makubaliano ya wengi miongoni mwa Wakenya ambayo yalifikiwa wakati wa mazungumuzo ya kiKatiba na kuhifadhiwa katika sheria za 1998. Jambo muhimu zaidi na lengo kuu la sheria ni nafasi ya wananchi.

Kwa mara ya kwanza kabisa, katiba utaratibu huu marekebisho haya yamewapatia Wakenya nafasi ya kuamua maadili na masharti ambayo wangependa kujitawala. Marekebisho yanatarajiwa yawe yenye undani ili kila kipengele cha Katiba ya sasa kiweze kufanyiwa uchunguzi. Ni lazima utaratibu wa Marekebisho uwe jumuishi na ushirikishe tofauti zote za Wakenya. Itabidi wananchi wapewe nafasi za kutosha ili kushiriki katika marekebisho haya. Ni lazima, Ripoti na mapendekezo ya Tume yawakilishe mapenzi ya wananchi. Hiki ni kitendo kikubwa mno cha kuliwezesha taifa kujitawala.

Malengo ya marekebisho yanasisitiza kanuni za kujitawala. Lengo la msingi ni udumishaji wa mfumo wa kidemokrasia ambao unaruhusu ushiriki wa wananchi katika masuala ya umma. Usambazaji wa mamlaka ili yawafikie wananchi mwishoni katika viwango vya utawala ambapo wanaweza kushiriki kikamilifu katika maamuzi na mbinu za uwajibikaji unatokana na lengo hili. Sambamba na lengo hili pia ni malengo yanayohusu utawala mwema, utawala wa kisheria na uwajibikaji wa viongozi na maafisa wa umma. Malengo haya yatatimizwa kwa kiasi fulani kufuatia ubainishaji wa nguvu za serikali na kanuni ambazo huvipatia vyombo vya serikali mamlaka ya kuweza kusawazisha na au kusimamia utekelezaji wa nguvu zao. Malengo mengine muhimu ni kulinda haki za binadamu, ikiwemo hasa kanuni za usawa na ulinganifu ili raia wote na jamii zote zitendewe haki. Kuna msisitizo mkubwa unaohitaji kuhusisha ujinsia, usawa na ulinganifu ili kukuza ushiriki wa wanawake katika siasa, maisha ya kijamii, na ya kiuchumi ya taifa. Kimsingi, hasa kwa kutazama hali ya Kenya ya kiuchumi na umaskini ulivyoenea, Sheria ya Marekebisho inasema kwamba ni lazima Katiba mpya ihakikishe kuwa Wakenya wote wanapata mahitaji ya msingi. Mahitaji ya msingi ni yale yaliyo muhimu kwa maisha katika hali za starehe na heshima, ambayo yanahusu umuhimu wa kuwa na chakula cha kutosha, afya nzuri, makao, elimu, mazingira safi yenye usalama, utamaduni na usalama wa kiuchumi.

Msingi wa malengo haya yote ni umuhimu wa kuwapo na amani ya kitaifa umoja na uadilifu ili kulinda maslahi ya wananchi. Lengo hili linatokana hasa na jinsi ambavyo siasa za Kenya na mambo mengine yamekita mno katika ukabila. Sheria inatambua kuwa, njia ya kuifikia amani ya kitaifa na umoja

haitatokana na kuweka ulazima wa kufanana jinsi ambavyo nchi nyingi zilielekea kufikiri wakati wa kupata uhuru. Kenya ina jamii nyingi na makundi yanayotofautiana katika misingi ya historia, lugha, dini na tamaduni. Umoja wa kitaifa unahatarishwa pale ambapo baadhi ya jamii zinaona kuwa zimetengwa an zimedhulumiwa, au tamaduni zao hazipewi heshima inayostahili.

Ni lazima umoja ujengwe katika misingi ya kuzitambua tofauti hizi za kitaifa ili katika miktadha ya kuibuka na kitambulisho kimoja cha utaifa, sheria na mazoea viweze kushirikisha utambuzi wa tofauti za kitamaduni, kijamii na kidini.

(b) Elimu Ya Uraia: Kuwatayarisha Wananchi Kushiriki

Kulingana na agizo lililotolewa, Tume iliendesha na kutekeleza mafunzo ya elimu ya uraia iliyohusiana na utaratibu wa marekebisho, Katiba ya sasa, dhana za kikatiba na masuala mengine ya kuhusu mabadiliko. Iliyohimiza mashirika ya raia kuiendeleza elimu ya uraia. Pia tume iliweka mipango rasmi na makundi mengine ili yaisaidie katika kuiendesha elimu ya uraia. Waliwahakikishia ufadhili wa kifedha na kazi nyinginezo. Tume iliandaa mitaala ya kitaifa na vifaa vya kufundishia elimu ya uraia ambavyo vilisambazwa kwa wingi. Ilisambaza vile vile kijitabu cha ***Marekebisho ya Katiba ya Kenya: Masuala na Maswali kwa Ajili ya Mijadala ya Hadharani*** (The Constitution of Kenya Review Process in Kenya: Issues and Questions fo Public Hearing), ili kichochee tafakuri za kuhusu mabadiliko na kuwashawishi wananchi kutoa mapendekezo. Pia iliwezesha vifaa vilivyotengenezwa na mashirika mengine kutumika. Ilipowezekana, makala na nyaraka ambazo zilitayarishwa katika Kiingereza zilitafsiriwa katika Kiswahili.

Wanatume walisafiri kote nchini huku wakitoa habari kuhusu marekebisho na ajenda ya mabadiliko; walihutubia mikutano kadha ya wataalamu, ya kijinsia, ya kidini, ya kitawala na mashirika mengine ya kijamii. Tume pia ilitumia vifaa vya kimtambo na vya habari kwa wingi na wakaifadhili kifedha mikutano mingi ya hadhara na warsha. Wananchi waliendesha mijadala yao wenyewe na mashirika mengi yakatoa mawasilisho yao kwa Tume. Vyombo vya habari vilizungumzia mara kwa mara habari za kuhusu marekebisho. Vilibeba makala zilizozungumzia maswala maalum ya kikatiba.

Elimu ya uraia na mijadala ya kuhusu maswala ya kikatiba ilitekelezwa na uwekaji wa Vituo vya Nyaraka katika kila wilaya. Katika Vituo vya Nyaraka kulikuwa na maandishi ya kuhusu historia ya Katiba ya Kenya na Katiba ya sasa, Katiba nyingine linganishi, nyaraka na kumbukumbu za Tume ya Marekebisho ilikuwemo ripoti za makongamano na warswa na makala yaliyowasiliswha za Tume. Maandishi haya pia yalihifadhiwa katika maktaba za umma. Pili, Tume ilibuni Vikao vya Kikatiba Katika Maeneobunge

(Constituency Constitutional Forum) – CCF) ili kuwezesha kuwepo kwa mikutano na keundeleza mijadala. Tatu, waratibu wa wilaya waliteuliwa ili kuwaongoza watu katika wilaya na maeneobunge na pia walishikilia nafasi za msingi katika utunzaji wa vituo vya nyaraka, uratibishaji wa elimu ya uraia shughuli za vikao vya kikatiba katika maeneobunge na utekelezaji wa ushiriki wa wananchi katika vikao vya Tume. Palibuniwa pia wavuti (Website) ambamo habari zote zilizomo katika vituo vya nyaraka vya wilaya yakiwemo mawasilisho yote yaliyotolewa kwa Tume. Hivi ndivyo Wakenya walio katika nchi za ng'ambo walivyochangia na kupata habari za kuhusu marekebisho. Mwenyekiti wa Tume na naibu wake wa kwanza waliihutubia mikutano ya Wakenya walioko Uingereza na Marekani walipozuru nchi hizo.

(c) Kuwasikiliza Wananchi

Tume ilianza kufanya mikutano ya kuwasilikiza wananchi jijini Nairobi na katika makao makuu ya mkoa mapema mwezi wa Desemba 2001. Mikutano hii iliendelea jijini Nairobi hadi mwisho wa Julai 2002. Mwishoni mwa Aprili hadi mapema Agosti 2002, Tume ilitembelea kila eneobunge kwa mikutano ya kuwasilikiza wananchi. Walienda katika vikundi vya Wanatume watano watano, au watatu watatu huku wakikaa siku mbili katika kila eneo bunge na wakati mwingine siku tatu katika maeneobunge makubwa makubwa. Kwa jumla, walipokea mawasilisho 35,015; mengi ya haya yakitokana na makundi maalum kama vile Vyama vya Kisiasa, Makundi ya kidini Mashirika ya Kitaaluma, Vyama vya Wafanyi kazi, Mashirika Yasiyokuwa ya Kiserikali na Jamii za Kikabila. Kwa njia hii ya kutumia mikutano ya rasmi na uwasilishaji wa memoranda, mamilioni ya Wakenya kote nchini na ng'ambo wameweza kuwasiliana na Tume.

(d) Uchanganuzi wa Mawasilisho ya Wananchi

Tume iliajiri idadi kubwa ya watafiti, wachanganuzi, karani wa data, wapiga chapa wa hatimkato ili kufasiri na kunakili kumbukumbu za mawasilisho ya mikutanoni na ya changanuo pamoja na mawasilisho mengine. Ripoti zilizotokana na vikao vya kikatiba vya maeneobunge ikiwemo mihtasari pamoja na nakala za maoni ya wananchi, zilitayarishwa na kupelekwa kwa hawa walioajiriwa. Kwa kutumia programu maalum za kompyuta zilizoundwa kwa matumizi ya Tume, mawasilisho yote yalichanganuliwa na kuratibishwa katika mitazamo tofauti. Haya yaliiwezesha Tume kutambua katika mtazamo mmoja matamanio ya Wakenya kuhusu masuala kadhaa katika viwango vya eneobunge, wilaya, mkoa na kitaifa. Matamanio haya pia yalianzishwa kwa kuzingatia ujinsia wa aina ya mtu au kikundi ambacho kilitoa mawasilisho. Majedwali jumuishi na yasiyokuwa jumuishi yalitolewa kwa Tume wakati ilipoanza shughuli zake. Wanatume waliangalia kwa makini maoni yaliyotolewa na wananchi na wakafanya kila juhudi ili kuyawakilisha katika ripoti ya mapendekezo na mswada wa sheria.

(e) Kujitayarisha, Kuandika Ripoti Na Mswada Wa Katiba.

Tume ilianza kazi kwa kulitalii agizo lake kwa mujibu wa Sheria ya Marekebisho. Ilipanga warsha na makongamano kumi na nne (14) ili kujadili masuala ya mabadiliko jinsi yaliyopangwa katika sheria. Wataalamu wa hapa nchini na wa ng'ambo waliisaidia Tume kuyafikiria masuala na kujifunza kutokana na tajriba za nchi za kigeni. Waliidhinisha utafiti na kupata namna nyingine za usaidizi kutoka kwa Wakenya wengine na kwa wasomi. Maafisa wa utafiti walitayarisha makala ya msingi huku wakitilia mkazo ujuzi wa kulinganisha. Tume ilifaidi pakubwa kutokana na tafiti za mashirika mbalimbali na za vikosi tume ambavyo viliwekwa na mkuu wa sheria ambavyo vilishughulikia masuala ya kikatiba katika mwongo mmoja ulopita. Wakati walipoanza shughuli zao, tayari walikuwa wamepata mazoea ya kuhusu masuala muhimu ya kuhusu mabadiliko.

Tume ilirejelea ajenda ya mabadiliko jinsi ilivyo katika Sheria ya Marekebisho na ya mambo mengine ili kutoa mapendekezo yake. Ilirejelea pia uchanganuzi ulioeleza udhaifu wa Katiba ya sasa, maoni ya wananchi na tajriba za jumla za Wanatume na ufafanuzi wao kuhusu umuhimu wa uadilifu, asasi na taratibu zilizowekwa ili kutimiza malengo ya marekebisho. Tumezingatia kwa dhati maoni ya wananchi lakini hatujafuata moja kwa moja yale tuliyoagizwa kufanya. Katika hali nyingi kuna maafikiano ya kwa ajabu baina ya maoni ya umma na ya mashirika maalum ilhali hakuna makubaliano yoyote katika baadhi ya miktadha hasa kuhusu baadhi ya masuala nyeti. Katika miktadha kama hii, Tume iliona kuwa haikulazimika kufuata maoni ya walio wengi. Zaidi ya hayo, iliona kuwa haikulazimika kufuata mapendekezo ya umma, hasa pale pale ambapo yalihitalafiana kimsingi na maagizo yaliyomo katika Sheria ya Marekebisho.Kwa kiasi kikubwa tuna furaha kusema kwamba maoni ya wananchi ya wananchi yaliafikiana kwa kiasi kikubwa na malengo ya Sheria ya Marekebisho, na kwa jumla yalionyesha kuwa yalifikiriwa kwa makini hasa kwa kutegemea uhalisia wa maisha ya kila siku.

Uchanganuzi wa ndani wa mawasilisho, malengo ya Marekebisho kuhusu nyanja maalum, na vifaa vilivyopo uliweza kutekelezwa katika miktadha ya kutumia kamati sita za mada kuu za Tume. Ripoti zao na mapendekezo vilijadiliwa na kamati katika vikao vya washiriki wote ambao walifikia maamuzi wa mwisho. Ripoti hizi za kamati zilipitiwa ili ziwakilishe maoni ya Tume. Kikundi cha kuandaa miswada kilikaa na Tume katika vikao vyao vyote na kuandaa mswada wa kwanza wa Katiba ambao Tume iliupitia kwa makini, aya baada ya aya. Mswada uliokuwa umepitiwa ulishughulikiwa na ukakubaliwa na Tume. Mswada huu umeambatanishwa na Ripoti hii.

Nyaraka kadha zinachangia ripoti na mswada wa Katiba. Kuna Ripoti nyingine kama hii lakini amabayo ni ndefu na inayoeleza kwa undani

uchaganuzi wa yale ambayo wananchi walituambia ripoti hii ndefu pia inayoeleza kwa undani kanuni za msingi na uhalalishaji wa mapendekezo yetu. Juzuu nyingine ya ripoti inabeba habari za kuhusu inaeleza semina na makala ya utafiti ambayo yalitayarishwa kwa niaba ya Tume. Kuna pia Juzuu nyingine ambayo inaeleza mbinu zilizotumika katika utekelezaji wa kazi yetu na orodha ya shughuli zetu zote. Juzuu hii ya mwisho pia ina maoni ya wananchi ambayo yamechanganuliwa kwa undani. Mwishowe kuna ripoti 210 za shughuli zilizofanywa na kila Kikao cha KiKatiba cha Maeneobunge. Maandishi haya ya ziada yatawasaidia Wakenya kuchambua uimara wa kazi yetu na kiwango ambacho tumekuwa waaminifu kwa maagizo yetu, hasa lililotuhitaji kuwasilikiliza wananchi na kuyawakilisha maoni yao.

Aghalabu, haikuwezekana kuweka kwenye mswada wa Katiba mapendekezo yote ambayo yalipokelewa na Tume – bila kuifanya kuwa waraka mrefu kupita kiasi au kuathiri kwa njia isiyofaa uhuru na uamuzi wa sheria na bunge kuhusi sera za baadaye. Licha ya haya, Makala marefu ya Ripoti yanaeleza kuwa maoni ya Wakenya na baadhi ya mapendekezo ya sera yaliyotolewa na Tume kama kielelezo kwa bunge katika uwekaji sheria wa siku za usoni.

f.) Hitimisho la Kuhusu Utaratibu wa Marekebisho

Tume imefurahi sana kuhusu jinsi ambavyo wananchi waliitikia mwito wa kushiriki katika marekebisho. Inashukuru kwa jinsi ambavyo wananachi wamewaunga mkono, jambo ambalo limeiwezesha Tume kuvuka vizuizi kadha wa kadha na kustahamili juhudi za kutaka kuukanyaga mkondo wa marekebisho. Tunaamini kuwa utaratibu wa marekebisho hadi sasa umekuwa wa manufaa mengi. Daima tumeona kuwa marekebisho haya yamekuwa zaidi ya harakati za kukubaliana tu kuhusu kanuni za Katiba Mpya. Yamehusu pia hali ya kujitambua upya na utambulisho wetu. Imekuwa ni kuwapatia wananchi sauti na kuidhihirisha umuhimu wao. Imekuwa ni kuwapatia nafasi ya kutafakari juu ya historia ya taifa letu na ya Katiba yetu. Imekuwa pia uhasibu wa taifa letu na serikali, na namna ya kwanza ya pekee na ya dhati ya kutathmini kumbukumbu za tawala zetu za sasa na zilizopita. Ni utaratibu wa kutambua jinsi ambavyo mwananchi wa kawaida anavyofafanua kinachomanishwa na kuwa mkenya huku wakieleza kwa uwazi vitambulisho vyao vya umoja na wingi wa tofauti zao. Ni kusisitiza azimio letu la kutaka Kenya iliyoungana na dhamiri ya kupata mfumo utakaoziwezesha jamii kudumu kwa pamoja. Ni kukubaliana kuhusu, na kuimarisha maadili na malengo ya kitaifa. Ni kupata kwa pamoja mbinu ambazo zitatuwezesha kutambua maono yetu ya pamoja kuhusu maslahi ya kila mmoja ya utu na ya haki katika jamii. Mambo haya ni muhimu hasa wakati ambapo nchi inajaribu kujibadilisha ili idumishe utaifa. Wajibu wa Katiba si tu kutupatia kielelezo cha mfumo wa jamii bali pia ni kuishikamanisha au kuipatia jamii yenyewe uhai. Tunaamini kuwa utaratibu wa Marekebisho umekuwa wa muhimu katika kufanikiwa kwa malengo haya.

Hoja kumi na tatu muhimu kutoka kwa wananchi

- Tupatie nafasi ya kuishi maisha ya heshima: tupate mahitaji ya msingi ya chakula, maji, mavazi, makao, ulinzi na elimu ya msingi ambavyo tutavilipia na juhudi zetu kwa kusaidiwa na serikali.
- Tunataka mfumo wa haki utakaotuwezesha kupata ardhi kwa siku zijazo na kutendewa haki kwa maovu yaliyopita
- Tupatie nafasi ya kuthibiti maamuzi yanayotolewa kuhusu maisha yetu, karibu na umma – tusaidie kuelewa vizuri maamuzi ambayo hatuwezi kuyafanya wenyewe lakini yanayohusu maisha yetu kwa undani
- Hatutaki mtu mmoja kumiliki uwezo mwingi
- Tunataka wabunge wetu wafanye kazi kwa bidii, watuheshimu na waheshimu maoni yetu – na tupewe uwezo wa kuwatimua kama hawatayatimiza haya.
- Tunataka tuweze kuwachagua viongozi ambao wana sifa za kuwa weledi, wanaokuwa na uadilifu na wa kujali maslahi ya wengine, sifa ambazo zitawafanya kuwa viongozi wa kustahiki
- Tunataka tuumalize ufisadi
- Tunataka polisi wanaowaheshimu raia – na ambao wanaweza kuheshimiwa na raia
- Tunataka wanawake wapate haki na usawa wa kijinsia.
- Tunataka watoto wawe na siku za usoni za kuweza kutegemewa – ikiwa ni pamoja na mayatima na watoto wa mitaani
- Tunataka walemavu wapewe heshima na kutunzwa kwa heshima
- Tunataka jamii zote ziheshimiwe na ziwe huru kuzingatia tamaduni na imani zao
- Tunataka kusisitiza haki yetu ya kuzitaka sehemu zote za serikali yetu kuwajibika - na tunataka asasi zilizo aminifu na za kuweza kufikiwa ili kuhakikisha uwajibikaji wao.

3. Tuliyoambiwa Na Wananchi: Muhtasari

Wakati Tume iliposafiri kote nchini au ilipokaa katika makao yake makuu ambako makundi yenye mpango ya aina zote yaliwajia ili kuwasilisha memoranda zao, masuala kadha wa kadha yaliibuka kwa uwazi mno. Ilibainika wazi kuwa kuna mengi ambayo huwaunganisha Wakenya katika maoni yao kuhusu pale ambapo taifa limefikia sasa, na yale ambayo yalikwenda mrama tangu hapo awali.

Baadhi ya matatizo yaliwasilishwa kwa Tume kwa nguvu wakati walipokuwa wakisafiri. Tume ilijua, bila shaka, kuwa takwimu zilizopo zinaonyeshwa kuwa kadri asilimia sitini (60%) ya Wakenya iliishi chini ya kiwango cha umaskini kilichowekwa cha pato la dola moja ya Marekani (US$ 1) kwa siku. Walijionea wenyewe kwa macho yao uhakika wa hali hii ambayo ilikuwa ya kuhuzunisha mno. Walipata watu wakiwa katika hali ya kukosa karibu kila

kitu walichohitaji lili kuishi maisha ya manufaa japo walikuwa wanafanya kazi kwa bidii. Watu hawa walikuwa hawataki kupewa misaada ya bure bali walitaka wasaidiwe ili waweze kujisaidia wenyewe. Tume iliwapata watu ambao japo walikuwa na mali haba, waliwakarimia mno Wanatume na wakajitolea kuacha shughuli zao za kila siku ili washiriki kwa uchangamfu katika harakati za marekebisho. Walipata taifa ambalo limesalitiwa mno na mfumo uliopo wa serikali na wa Katiba.

Suala muhimu linalotokana na hali hii na pia la kuwahusu hawa ambao wanaonyeshwa kama asilimia Sitini (60%) ni kile ambacho Sheria ya Marekebisho imeainisha kama "Mahitaji Ya Msingi". Muhimu kwa yote ni chakula na maji. Wakulima walitoa wito wa kuweza kufanya ukulima wa kunyunyizia maji ili waweze angalau kukuza mimea zaidi – na katika baadhi ya miktadha, waweze kukuza mimea. Hakuna maji ya mfereji katika sehemu nyingi na wanawake wanalazimika kwenda safari ndefu kwa miguu kila siku ili kupata maji na kuyabeba wenyewe kwa kutumia ndoo. Katika jamii nyingi hakuna aina yoyote ya huduma za afya, hakuna hata zahanati ndogo – au utapata jengo la zahanati ambalo halina mwuguzi (ni ndoto kufikiria au kuwaza kuwa daktari anaweza kupatikana karibu) na hakuna dawa. Inawezekana pawe na shule – lakini karo ya shule na malipo mengine yasiyoweza kutimizwa humaanisha kuwa watu wengi hawawezi kuwapeleka watoto wao shuleni. Badala ya viwango vya kujua kusoma na kuandika kuongezeka na pia idadi ya watoto wanaoenda shule kuongezeka, hali inazidi kudidimia na idadi kupunguka. Watu walioenda shule zamani wanalalamika kuwa wajukuu wao hawawezi kuhudhuria hata shule za msingi. Ufunguo wa kuboresha maisha ya wananchi katika jamii nyingi unategemea kuwepo kwa barabara zinazostahili kuitwa barabara. Katika sehemu nyingi, barabara, hata katika nyakati za ukame ni mbaya mno kiasi kuwa hakuna namna ya kufikisha mazao sokoni, watoto hawawezi kufika shuleni, wagonjwa hawawezi kupelekwa hospitalini. Kuna baadhi ya jamii ambamo wananchi walisema ya kuwa barabara zao ni mbaya mno kiasi kuwa hawawezi hata kuwapeleka wagonjwa hospitalini kwa kuwasukuma kwa toroli (wheelbarrow). Kwa wengi wa wananchi hawa, hakuna makao ya kufaa – iwe ni mijengo au usalama kwa sababu wengi wao ni maskuota au kwa sababu hawana vyeti vya kumiliki ardhi ambayo wanaistahili.

Wakulima walilalamikia, si tu haja ya maji na barabara bali walilalamikia pia ukosefu wa masoko kwa mazao yao kwa sababu viwanda vingi vilikuwa vimefungwa (kama vile kiwanda cha korosho cha Kilifi na viwanda kadhaa vya sukari). Au kwa sababu ya kutowajibika kwa makundi yanayoshughulikia uuzaji. Wakati mwingine walilalamikia hali ya kuwa hakuna mashirika ya kuuza bidhaa. Wakulima wa mifugo walilalamika kwa sababu kilimo kilitiliwa makini kwa upande wa upandaji mimea lakini uboreshaji wa mifugo na ufugaji havikuzingatiwa. Wakulima wameathirika mno na bei za dunia za kahawa na chai na baadhi wanalalamika na kuitaka serikali ifanye juhudi za kuwasaidia ili wapate mimea mingine ya mauzo ambayo ni ya kutegemewa.

Wengi walilalamika kwamba mimea na mazao yanayotoka nchini yaliletwa kutoka nje, bila malipo ya kodi ya forodha, jambo linaloharibu juhudi za viwanda nchini. Wafugaji walilalamika kuhusu ukame na ukosefu wa maji, miundo msingi na biashara (kwa mfano kuporomoka kwa Tume ya Nyama ya Kenya -KMC)

Usalama ni tatizo katika baadhi ya sehemu za nchi. Kiwango cha uhalifu jijini Nairobi kinazungumziwa kama mada kuu za magazeti lakini si kwa njia inayoonyesha jinsi ambavyo hali hii inawaathiri maskini hohehahe wanaoishi katika jiji. Ingawa Tume inafahamu kuwa ni matajiri w anaolengwa na ukosefu wa usalama huathiri imani ya wawekezaji uchumi wa asili na wa kigeni na pia biashara ya utalii, ilipata kusikia jinsi ambavyo wakazi wa mitaa ya mabanda hawawezi kuthubutu kutoka nje baada ya giza kuigia kwa sababu ya hatari ya kushambuliwa, ya kuibiwa au ya kubakwa. Wanawake kote nchini wanakabiliwa na hatari ya kudhulumiwa na kudhuriwa manyumbani mwao na hata nje. Malalamishi ya migogoro ya nyumbani yalielezwa kutoka katika jamii zote (mawasilisho ya namna hii yalifanywa mara nyingi katika vikao ambapo wanaume hwakuruhusiwa), za sehemu za mashambani, kuna jamii ambazo zimehatarishwa daima na wizi wa mifugo, chuki baina ya jamii za ufugaji na za kiukulima na pia hatari ya moja kwa moja ya maharamia ambao wamedumishwa na kuwepo kwa silaha zinazotokana na mizozo ya kimaeneo. Mnamo 1999, uwiano ya polisi kwa raia nchini Kenya ilikuwa polisi mmoja kwa raia mia saba themanini na saba (1:787). Umoja wa kimataifa umependekeza ratio ya polisi mmoja kwa raia mia nne (1:400).

Sheria ya Marekebisho ya Katiba imetaja pia mahitaji ya pembeni. Huenda ikasemekana kuwa Tume zinahisi kuwekwa pembeni. Jamii kadha zinaona kana kwamba zimedharauliwa na kuachwa au zimelenga kudhulumiwa na serikali. Wakulima wa mifugo wanaona kama kwamba mienendo yao ya maisha inadharauliwa na mahitaji yao ya ardhi kutoeleweka. Jamii zilizo karibu na mpakani, hasa mipaka ya kaskazini zinaona kana kwamba uaminifu wao kwa serikali unatiliwa shaka, na pia kuwa vifaa wanavyopewa na serikali si vya dhati na wakati mwingine havifai na kwamba hakuna anayeyatambua mahitaji yao. Waislamu wanaona kuwa dini yao ni ya walio wachache na kwamba wamedhulumiwa kwa kufanyiwa ubaguzi na haki zao zimepuuzwa. Pia, kwa jumla, wanaona kuwa maadili na asasi vimezorota. Baadhi ya jamii, ni za kiislamu, zinaishi mipakani na pia ni za wafugaji na kwa hivyo zinahisi kubaguliwa mara tatu. Baadhi ya jamii ndogo zinaona kama kwamba zinakabiliwa na maangamizi. Hasa jamii ya Ogiek ambao wanakabiliwa na hatari ya kufukuzwa kutoka misituni ambako wanaishi na kwa hivyo kufukuzwa kutoka katika mazingira yao ya maisha ya kila siku. Wananchi wa asili ya Kihindi wanajiona kama waliowekwa pembeni kisiasa japo si kiuchumi (hasa Wagoa ni wanyonge kiuchumi na kwa sababu za kihistoria mara nyingi hujikuta wakiwa bila utaifa). Jamii zinazoishi karibu na mbuga za wanyama (hasa kama ziliishi au kulisha mifugo yao katika maeneo ya mbuga tangu jadi) wanajiona kuwa wamewekwa pembeni kwa kuondolewa

na kutoshirikishwa katika masuala kuhusu ardhi hizo na pia kwa sababu ya hali wanayoiona kuwa ya kuwapendelea wanyama wa pori dhidi ya binadamu. Katika sehemu za pwani, wananchi wanaona kuwa ploti zenye thamani zimemilikiwa, karibu zote, na watu wasiokuwa wenyeji. Jamii zilizo karibu na kambi za wakimbizi zinaona kuwa Shirika la Umoja wa Mataifa Linaloshughulikia Wakimbizi (United Nations High Commission for Refugees - UNHCR) halipendi kuwaajiri wenyeji; mifereji ya maji huwekwa katika maeneo ya baadhi ya jamii na kuelekezwa kwenye Mahoteli za watalii ilhali wenyewe hawana maji safi wala ya kutosha. Pia mara nyaya za umeme hupitia katika vijiji vyao ambavyo havina umeme.

Wakenya walemavu wanahisi kuwekwa pembeni: hawawezi hata kushiriki kwa sababu majengo, njia (endapo ziko) na usafiri havipatikani. Mahitaji yao hasa ya kimawasiliano (kwa mfano kutumia lugha-ishara na breli) na elimu havijazingatiwa. Wanawake wanajiona kama ambao wamewekwa pembeni. Bunge la Kenya ni kati ya mabunge yenye idadi ya chini ya wanawake ulimwenguni. Zaidi ya hayo, kuna viwango vya chini vya wanawake ambao hushiriki katika elimu wakilinganishwa na wanaume, na pia ni wanawake wachache ambao hushiriki katika ulimwengu wa biashara wakilinganishwa na wanaume. Wazee wamewekwa pembeni kwa jinsi nyingi hasa wanapokuwa dhaifu na wanyonge. Hata vijana ambao kwa kawaida wanahitaji ulinzi maalum, wanakumbana na matatizo mengi. Wengi hawana kazi, hata kama wana shahada za vyuo vikuu. Tuliona uchungu wao popote tulipoenda.

Uwekaji pembeni wa watu si sawa na ubaguzi – japo mara nyingi hutumika kwa maana moja. Watu walemavu (au wenye hali ambazo si za kulemaza kama vile zeruzeru na walio na virusi vya UKIMWI) wananyimwa haki zilizo sawa na za wengine ama kwa vitendo vya kuwadhulumu au kwa kupuuzwa tu. Makundi ya kidini na ya rangi pia yanaona yakibaguliwa jinsi walivyo wanawake. Ubaguzi unafanywa na serikali na pia na raia wenzao, wakati mwingine kwa kutojua au kwa kuwabagua na wakati mwingine kwa maksudi. Sheria za kitamaduni zinawanyima wanawake urithi wa ardhi na mara nyingi huwaacha wajae na watoto wakihangaika. Au pia wajane wanaweza ‘kurithiwa’ na shemeji zao.

Taifa zima linaona kama ambalo limebaguliwa na serikali na nyenzo za utawala. Wananchi wanajiona kama ambao wamepuuzwa na kudhulumiwa. Wanaona kama ambao hawawezi kuyadhibiti maisha yao au hatima yao. Licha ya kuweza kupiga kura, ushiriki wao ni haba mno. Hakuna asasi za mamlaka ambazo wanaweza kukimbilia ili kutoa malalamishi yao – hawawezi hata kuwaendea polisi. Hata tabaka lililobahatika la wafanyi biashara linalalamika kuhusu uhuni unaofanywa na asasi na vyombo vya serikali na hali ya kunyimwa haki na mahakamu kwa sababu ya mahakama hizo kukosa umilisi na pia kwa sababu ya ufisadi, au kukosekana usawa kwa sababu ya kutegemea mamlaka ya nchi. Kuna uoza wa hali ya juu wa asasi. Serikali imekuwa sasa nyenzo za wachache kujiinua na kujitajirisha na wengi

kudidimia katika umaskini. Tofauti katika viwango vya utajiri nchini Kenya ni kubwa na miongoni zile za juu zaidi ulimwenguni. Wakenya hawaoni ajabu kuwepo viwango vya juu vya uhalifu na ukosefu wa motisha miongoni mwa wafanyi kazi wa umma kiasi kuwa hawafanyi kazi kwa bidii wala kwa uhalali.

Baadhi ya matatizo ya leo yanatokana na maovu ya jana – labda jana inayoenda nyuma hadi karne ya kumi na tisa hasa kuhusu maswala ya ardhi katika maeneo ya pwani, na matatizo ya hivi majuzi kama vile mizozo ya kikabila ya 1997. Kuna jamii ambazo bado zinaumia kwa sababu ya sera za ardhi za kikoloni, na baadhi ya jamii zinaona kuwa Wakenya wengine ndio wanaomiliki ardhi ambazo awali zilikuwa zao. Kuna makundi ambayo yananyimwa nafasi ya kufikia sehemu zao za ardhi zilizotengwa kwa madhabahu kwa sababu hivi sasa ni ardhi ya serikali. Mawasilisho mengi yanabainisha matatizo yaliyomo katika sera za serikali za awali. Licha ya kutoshughulikia masuala ya kuhusu maslahi ya maisha na mahitaji ya msingi ambayo tumeyataja awali, kuna kilio cha jumla kuhusu usimamizi mbaya wa uchumi - hali ya kuipora nchi - kuhusu kutoweza kuuangamiza ufisadi, kuhusu kuzorota kwa mazingira ikiwemo kutoweza kuuondoa uchafu, kuharibu misitu na kuichafua hewa na uchafu unaotoka viwandani, mmomonyoko wa udongo, mito ambayo hivi sasa imekuwa mifereji ya wazi ya maji machafu, na pia kuhusu unyakuzi wa ardhi ambao umesababisha unyakuzi wa maeneo ya ardhi iliyotengewa umma, na pia vifaa vya umma kubinafsishwa. Licha ya hayo, hata ardhi ambayo awali ilitolewa kwa mashirika maalum imetolewa kimaajabu kwa watu wenye uwezo.

Wananchi wametaja hofu waliyo nayo kuhusu mfumo uliopo wa kisiasa uliopo. Kila mmoja anaona kuwa Rais ana uwezo mwingi sana. Hawawaamini wabunge wao. Baada ya kuchaguliwa, wabunge hawaonekani tena katika maeneobunge hadi wakati wa uchaguzi unaofuata, ingawa raia hawana imani na yale wanayoyafanya jijini Nairobi, hawaoni faida yoyote ya wabunge kwao wenyewe na hata kwa taifa ilhali hawawezi kufanya chochote. Wanaamini kuwa kuna haja ya na kuwajibika. Ujumbe muhimu kwa serikali ulikuwa kwamba, mamlaka yaletwe karibu na wananchi. Walitaka kuwa maamuzi yaliyofikiwa na ya kuwahusu yafanywe na watu wa kuaminika na yaweze kuwafikia. Watu wengi walilalamikia utawala wa mikoani kama uliokuwa na kiburi na uliotekeleza mambo yake kiholela wala haukuitikia kilio cha wananchi wala matumaini yao. Walitaka utawala huu wa mikoani ufutiliwe kabisa au kwa kiasi kwa sababu baadhi ya wananchi walitaka nafasi za chifu na naibu wao na hata nafasi za wakuu wa wilaya zihifadhiwe.

Vyombo vingine vya kiserikali pia vilionekana vya kutoridhisha kamwe Mahakama ni ghali mno, hayafikiki na pia yana ufisadi mwingi. Malalamishi ya kuhusu usumbufu wa polisi, ukatili wao, ufisadi na kwa hakika ushiriki katika uhalifu mdogo mdogo na hata mkubwa ni miongoni mwa mambo

yaliyorudiwa mara kwa mara katika mawasilisho. Magereza yalielezwa kama ambayo hazifai kwa binadamu.

Mapendekezo ya mabadiliko ya kuhusu kila jambo hayakulingana katika hali zote. Wananchi wengi walishutumu jinsi ambavyo serikali na Katiba vilivyotekeleza nyadhfa zao, lakini bila kutoa mapendekezo ya moja kwa moja kuhusu jinsi ya kuirekebisha hali hii – hapakuwa na sababu ya kuwafungia watu katika kuyatoa mapendekezo haya kwa sababu lilikuwa jukumu la Tume kufikiria kuhusu namna ya kuyazingatia malalamishi na matatizo katika Katiba. Palikuwa pia na maoni mengi yaliyotolewa kuhusu baadhi ya matatizo haya na ambayo yaliafikiana: kama vile kutoweka nguvu nyingi katika mikono ya mtu mmoja, kuibuka na mfumo wa kuweza kuyapokea malalamishi – wengi wao walitaja moja kwa moja umuhimu wa kuwa na Mpokeaji Wa Malalamishi (Ombundsman) – ili kukuza vyombo vya uwajibikaji, kwa jumla, ili kukuza upataji wa haki za binadamu, ili kuhakikisha kuwa uteuzi wa wanaoshikilia afisi za umma unafanywa kwa njia huria, na ili pia kuhakikisha ugawaji sawa na matumizi ya rasilmali. Wananchi waliitaka Katiba iwatambue kwa namna ambavyo haijawatambua awali. Walitaka waipate Katiba: iwe katika lugha wanayoifahamu na itafsiriwe katika lugha zetu zote. Wangependa sana wapewe fursa ya "kuwaondoa" wabunge wasiotimiza wajibu wao.

Katika baadhi ya miktadha kuna makubaliano kuhusu matokeo lakini si katika hatua za kuyafikia matokeo hayo. Kuna dalili za baadhi ya wananchi kutaka kurudisha sifa za Katiba huru jinsi ilivyokuwa awali, au kushirikisha baadhi ya maoni ya kutokana na Katiba ya Uganda ambayo ni mpya, na pia wakati mwingine walitoa maoni yaliyopendekezwa kutokana na matarajio yao ya kisiasa. Maoni yao kuhusu namna ya kuuleta utawala karibu na umma na kuyawakilisha katika Katiba yanatofautiana. Baadhi walitaka mifumo ya majimbo, au ya kuimarisha tawala za wilayani ili kuwashirikisha wazee. Kutoshinikiza uwezo katika nyenzo maalum kwa wengine kulimaanisha mifumo ya bunge na kwa wengine ikamaanisha kitu kama mfumo uliopo sasa lakini ambamo nguvu za Rais zinapunguzwa. Baadhi wanataka pabuniwe Ukumbi wa pili katika bunge – ambao utawakilisha matakwa ya walio mashinani. Wengi wanataka siku ya kupiga kura iwekwe na ijulikane wazi.

4. Tuliyojaribu Kutekeleza Katika Katiba Mpya

Ili kushirikisha malengo yaliyo katika Sheria ya Marekebisho na maoni ya wananchi, ni muhimu kuibuka na waraka mpya. Tume inachukulia kuwa dhima ya Katiba katika utawala wa Kenya si tu ya kuimarisha nguvu na

miundo iliyopo ya kiutawala bali ni kuwezesha utekelezaji wa mabadiliko ya kijamii na kiuchumi ambayo wananchi wanayataka na ambayo ni muhimu katika kuhakikishia kuwepo kwa demokrasia, ushiriki na jamii ya haki. Tunaamini kwamba mengi ya mabadiliko haya yatatimilika kupitia asasi mpya na taratibu za kiutawala na kiuwajibikaji ambazo tunapendekeza. Lakini katika muktadha wa tajriba zetu za kikatiba, itabidi tuzingatie hata zaidi ya asasi zilizopo. Tunahitaji kuweka malengo ya nchi na matumaini, na kanuni ambazo zitatawala utekelezaji wa nguvu za serikali.

Tunapendekeza kuwa Katiba itumike ili kuimarisha ukubalifu wa hali ya kuwa sote tu washiriki katika jamii moja ya kisiasa. Katiba inatupatia motisha ya kufikiria katika viwango vya juu ambavyo vinazidi utambuzi wa siasa za kikabila kupitia sheria za uchaguzi, kanuni na miundo ya uundaji wa serikali. Ni lazima tuhakikishe kuwa utambuzi wa makabila ya Kenya na wingi wa tofauti za kimaeneo na kidini havipatikani kwa kupuuza umoja wa kitaifa. Mahali pa kusherekea aina na wingi wa tofauti za Wakenya ni katika nyanja za kijamii na kibinafsi bali si za kisiasa. Isitoshe tunatambua kuwa umoja wa kitaifa haupatikani pasipo jamii zote kutendewa haki. Tunapendekeza kuwa jamii ambazo zimenyimwa fursa ya kufaidi kutokana na maendeleo ya kiuchumi zisaidiwe ili zifikie kiwango cha maisha bora cha Wakenya wengineo. Tunapendekeza pia kuwa, kuhusu masuala ya ardhi na mengineyo, dhuluma zilizotendwa zamani zizingatiwe na papo hapo tunapendekeza namna na vyombo vya kutumika katika uzingativu huu.

Mswada wa Katiba unalenga kuifanya siasa kuwajibika na kuwa yenye amani – ili iwe inayomulika utaifa. Tunapendekeza ukadiriaji wa vyama vya kisiasa ili kuhakikisha kuwepo kwa demokrasia ya ndani na uwajibikaji kwa umma. Isitoshe, hali hii pia itahakikisha kuwepo kwa kanuni ya maadili ambayo kwayo haki ya ushiriki wa wote katika harakati za kisiasa bila kuogopa fujo au vitisho vya vurugu inahakikishwa. Nguvu za Tume ya Uchaguzi za kuhakikisha kuwepo kwa uchaguzi huru na wa haki, na za kuondoa fujo na ufisadi zitaimarishwa. Utekelezaji wa mamlaka ya taifa utatawaliwa na kaida na asasi mpya. Patakuwa na usambazaji wa mamlaka ya kisiasa toka kitovuni ili yaenee baina ya Bunge, mamlaka ya nchi, mahakima, huduma za umma na Tume huria na maafisa wanaoshikilia afisi za kikatiba.

Uwezekano wa bunge kushiriki katika uundaji wa sera na kutekeleza usimamizi wa mamlaka ya nchi utaongezeka kiasi. Rais atakuwa na majukumu maalum ya kudumisha umoja wa kitaifa na kuilinda Katiba. Mawaziri, wakiongozwa na Waziri Mkuu ndio watakaoshikilia mamlaka ya juu ya kiutawala. Baraza la Mawaziri, wakiongozwa na Waziri Mkuu ndio watakaoshikilia mamlaka ya juu. Waziri Mkuu atasaidiwa na naibu wawili ambao watateuliwa na Rais na kuidhinishwa na Bunge. Isipokuwa Waziri Mkuu, na naibu wawili wake mawaziri watateuliwa kutoka nje ya Bunge ili kuhakikisha uteuzi wa watu wanaostahili na kuwaepusha na majukumu ya maeneobunge. Mawaziri hao watakuwa wabunge kwa mujibu wa nyadhifa

zao kwa hivyo hawatapiga kura. Mawaziri watakuwa na haki ya kutoa hotuba katika Kumbi zote mbili.

Tumejaribu kuwaweka wananchi katika kitovu cha Katiba –tukizidi kusisitiza umuhimu wa ushiriki wa umma, na uletaji wa mamlaka karibu na umma, kupitia upunguzaji na usambazaji wa mamlaka ili kufikia mikoa, wilaya na ngazi za chini za utawala, hadi katika mikutano ya vijijini. Miundo ya upunguzaji na usambazaji wa mamlaka na nguvu wanazopewa itaimarishwa na mabadiliko yo yote yatahitaji uidhinishaji wa robo tatu la wanachama wa Baraza la Taifa (inayowakilisha mikoa na wilaya).

Tumejaribu kuunda mfumo wa kikatiba ambao unazingatia jamii yenye haki na utu – ili ishughulike na malengo ya kuhusu umaskini na ishughulike na malengo ya kuhusu umaskini na ufisadi. Tumependekeza utekelezaji wa Vitendo Visawazishi (Affirmative Action) pale ambapo vitasaidia katika kurekebisha dhuluma na maonevu ya awali, yawe ya kijinsia, ya kijamii au ya kimaeneo. Tumependekeza kanuni na asasi za maendeleo sawazishi, ugawaji wa haki wa rasilmali na usimamizi mzuri wa rasilmali. Ili kuhakikisha Wakenya wote wanapata mahitaji ya msingi, tumetoa nafasi kubwa kwa haki za kijamii, kiuchumi na kitamaduni ambazo hazitaimarishwa na mahakama tu bali pia zitatoa misingi ya kuundwa kwa sheria na sera. Tumefikiria pia kuhusu wajibu wetu kwa vizazi vijavyo na tukapendekeza kanuni za maendeleo tegemevu na ulinzi wa mazingira.

Mapendekezo yetu yanalenga kuifanya nchi ya Kenya kuwa na uraia mwema kimaneneo na kimataifa, itakayodumisha amani, maendeleo ya kiuchumi, haki za binadamu na maslahi mengineyo. Tunaitaka nchi ya Kenya kushikilia wadhfa wenye manufaa katika masuala ya Afrika na ya kimataifa. Tunaamini kwamba Kenya ambayo itajitawala vyema kidemokrasia, kishirikishi na kwa kutumia mwelekeo wa haki kikatib itakuwa na uwezo mkuu wa kimaadili katika vikao vya kimataifa.

(a) **Usawa Na Ulinganifu**

Sheria ya Marekebisho inasisitiza umuhimu wa kutekeleza usawa na ulinganifu. Usawa unamaanisha kutenda haki. Ulinganifu unaashiria kumtumikia kila mmoja kwa njia ya usawa – japo wakati mwingine usawa haumaanishi haki. Kila mwananchi anastahili kupewa nafasi sawa au ulinganifu wa kiuwezekano. Lakini kwa wale ambao awali hawajatendewa haki, au ambao kwa sababu ya ulemavu ama sababu nyinginezo huanza maisha kwa kudhulumiwa hawataridhishwa na usawa wa moja kwa moja. Ili kuwa na mfumo wa kiulinganifu, ilibidi tuchunguze na kubainisha kinachosababisha ukosefu wa usawa na pia kutambua ni nani wasiokuwa sawa. Sheria ya Marekebisho ilitupatia mahali pa pema kuanzia ilipozungumzia ujinsia, ulemavu na jamii zilizowekwa pembeni. Mawasilisho ya wananchi yaliongeza pia makundi ya wazee. Wananchi waliitikia mwito wa kubainisha visababishi vya ukosefu wa usawa na

wakataja: mielekeo ya kitamaduni, historia ya ukosefu wa haki kabla, wakati wa, na baada ya kipindi cha ukoloni, masafa ya kijiografia, na ukosefu wa uvumilivu na kutokuwa weledi.

Mswada Wa Katiba Unawafanyia Nini Wanawake?

- Unakataza ubaguzi katika misingi ya uana, ujauzito na hali ya ndoa; Unahitaji sheria mpya ambazo zitayafanya haya kuweza kutekelezwa
- Unaanzisha Mfumo wa Kimseto Wenye Wiano wa Wanachama (Mixed Member Proportional System); na kuhitaji ya kwamba asilimia fulani ya waliomo katika ngazi za juu (Top–Up) wawe wanawake; Unaruhusu wagombea kura huria; kwa hivyo wanawake hawategemei uteuzi wa chama na unahakikisha usawa katika uwakilishi wa wanawake katika ukumbi wa pili na katika mabaraza ya wilaya na mikoa.
- Unaweka kanuni ya jumla ya ushiriki wa wanawake kuwa thuluthi moja ya jumla inayotarajiwa.
- Inatoa lazima ya kutambua haja ya kuwashirikisha wanawake katika vyombo vya umma na mahakama.
- Vyama vya kisiasa viwe vya kidemokrasia na vinavyowashirikisha wanawake.
- Haki sawa zitakuwa pamoja na haki ya ardhi, elimu, kushikilia afisi n.k.
- Sheria za kitamaduni ni lazima ziafikiane na kanuni za kikatiba.
- Haki sawa ili wanaume wa kigeni waliowaoa Wakenya au wanawake wa kigeni wanaoolewa na Wakenya wapate uraia.
- Kulinda maslahi ya wanawake hasa kuhusu umama kwa kuwapatia haki ya likizo ya zingizi au likizo ya kujifungua.
- Kulinda haki za kuhusu kazi kwa kuweka kanuni za jumla ambazo hazibagui kanuni maalum za kazi.
- Haki sawa za kuoa, haki za katika ndoa na pia haki katika hatima ya ndoa.
- Haki za wanawake wafungwa ziheshimiwe ikiwemo ulinzi dhidi ya matumizi ya nguvu dhidi yao, kutengwa na wanaume; haki ya kuvaa nguo zinazokubalika na dini yao n.k.

Visababishi vyenye asili nyingi vya ukosefu wa usawa vinahitaji kukabiliwa kwa njia tofauti na za kufaa. Matatizo mengi ya Kenya leo yana misingi katika hali ya jumla inayotokana na ukosefu wa maendeleo kwa upande mmoja na udhaifu ikiwemo ukosefu wa makini miongoni mwa wanasiasa na ukosefu wa maarifa kwa upande wa umma. Hata bila ya kuyalenga haya kwa njia ya moja kwa moja, Katiba mpya yenye malengo mapya kwa nia ya wema wa kitaifa itaibua mbinu za kuondolea baadhi ya visababishi hivi vya ukosefu wa usawa. Malipo bora kwa huduma za jamii, ikiwemo polisi kwa mfano, yatawawezesha wafanyi kazi za umma kujikinga dhidi ya ufisadi. Raia

wenye kisomo bora watakuwa walinzi bora wa haki zao. Lakini tahadhari kuwa Katiba isichukuliwe kuwa imo katika kuyatafuta maendeleo, (kwa hakika si rahisi kwa Katiba kuyatimiza haya). Katiba ya wakati wa uhuru ilitakikana kuyatimiza haya – na Wakenya wamegundua jinsi ambavyo utekelezaji wa Katiba unaweza kuivuruga ili kutimiza manufaa ya wachache walio na uwezo huu. Miongozo maalumu kwa serikali na mbinu bora za kukuza uwajibikaji ni muhimu ili kuhakikisha kuwa mazoea ya zamani hayarudi tena.

Mswada wa Katiba unajaribu kupendekeza namna ya kuufikia usawa ifuatavyo:

- Haki: mswada unatoa haki za msingi kwa watu wote, na pia ukubalifu wa uzingativu maalum pale ambapo kuna hatari ya kutaka kuendeleza aina za ukosefu wa usawa zilipo. Haki hizi zimeungwa mkono na mbinu za utekelezaji zilizowekwa.
- Mielekeo: mswada unaagiza kuwa serikali, vyombo vya habari na wengine wanaochangia maoni wawaelimishe raia kuhusu Katiba na uadilifu wake ikiwemo kudumisha ulinganifu.
- Sera: mswada unazungumzia sera ambazo ni lazima serikali ifuate ili kutimiza ahadi za Katiba
- Miundo: mswada unaweka miundo ya uundaji na utekelezaji wa sheria.

Majedwali yaliyomo katika Sura hii na Sura ifuatiayo yanaonyesha baadhi ya njia ambamo kanuni hizi za usawa na haki zitazingatiwa kuwahusu wanawake, watoto, wazee na kwa masuala kuhusu makundi yanayoona kuwa nafasi zao hazithaminiwi na pia kuwa wanabaguliwa.

Kikundi kingine katika jamii ni cha wale ambao wakati mwingine wanaitwa “walio wachache” (minorities). Mswada wa Katiba hauitumii lugha ya aina hii – kwa sababu ambazo tumezitoa katika Nakala Ndefu ya Ripoti hii. Lakini hofu za jamii ambazo zilitolewa kwa Tume kuhusu ubaguzi, kutoheshimu desturi, dini, tamaduni na uwekwaji pembeni wa namna mbalimbali.

Mswada Wa Katiba Unawafanyia Nini Walemavu?

- Ubaguzi katika misingi ya ulemavu umekatazwa
- Ufafanuzi wa ulemavu umepanuliwa ili kuhusisha wengine kama vile zeruzeru na walio na virusi vya UKIMWI.
- Walemavu wana haki sawa kama wegine ikiwemo haki ya kuoa na kuanzisha familia.
- Inaunda kanuni kwamba walemavu wawakilishwe katika viwango vyote vya asasi za kutoa uamuzi na utawala.
- Ni lazima serikali isitumie lugha ya kudhalilisha na pia izuie matumizi ya lugha ya namna hii.
- Inatoa haki ya kuweza kushiriki kikamilifu iwezekanavyo katika masuala ya kijamii jinsi ilivyo katika kanuni ya ushiriki na kauli kwamba walemavu wapate haki zote.
- Mahitaji ya watoto walemavu inavyoelezwa katika haki za watoto.
- Mswada unataja kwa njia maalum haki za wafungwa walemavu.
- Lugha-ishara na breli zinahitaji kutambuliwa na kukuzwa kwa njia mbalimbali. Kwa mfano ikuzwe katika mifumo ya mahakama na elimu. Ni wajibu wa serikali kuhimiza na kuyakuza haya.
- Kanuni za haki za binadamu zinataja kwa njia maalum mahitaji ya elimu ikiwemo umuhimu wa kuwa na elimu ya mseto inayowashirikisha walemavu na wengineo (Intergrated Eduction).
- Kuna kanuni ya kuhusu usalama wa kijamii lakini kanuni hii itatekelezwa tu kama itawezekana.
- Walemavu wana haki sawa na za wengine - ambazo zinahusu ulinzi dhidi ya kupoteza urithi kwa sababu ya ulemavu.
- Kuna jukumu la jumla la serikali kuhakikisha na kuwezesha walemavu kuyaingia majengo, kupata usafiri, mawasilisano ya kiteknolojia na vifaa vingine kwa jumla.
- Tume ya Haki za Binadamu izingatie suala la ulemavu kwa makini.
- Mfumo mpya wa uchaguzi uimarishe viwango vya ushiriki wa walemavu katika nafasi za kuchaguliwa.

Haki ya uhuru wa wa kidini, haki ya lugha, na ya kudhihirisha utamaduni, haki za msingi za kuuheshimu utu na kutofanya ubaguzi ni muhimu. Vivyo hivyo ndivyo zilivyo muhimu kanuni za upunguzaji na usambazaji wa mamlaka ili kuhakikisha ugawaji sawa wa rasilmali za kitaifa ili kuweza kushughulikia masuala ya kihistoria kuhusu ardhi. Na mfumo wa serikali – uliokusudiwa kutoa picha nzuri ya matumaini ya wananchi kuhusu uchaguzi, wa kuzingatia maslahi ya kila mmoja, ya kuwajibika na kwa kiasi fulani isiyokuwa na ukinzani – uwe pia unayelekea kujenga taifa lenye usawa.

b.) Haki za Binadamu

Sheria ya Marekebisho inawekea mkazo haki za binadamu. Baadhi ya masuala ya kuhusu haki za kibinadamu ni yale ambayo tumeyataja hivi punde – lakini si haki zote za binadamu ambazo zinajishughulisha kimsingi na usawa. Haki nyingi kati ya hizi ni muhimu katika kuwezesha ushiriki kamili katika maisha ya kidemokrasia ya nchi. Haki hizi: za maoni, za kujumuika, za kushirikiana na kadhalika ni za kawaida katika Katiba nyingi za kisasa, na kuna mapendekezo kamili katika mswada wa Katiba - pamoja na baadhi ya mazungumzo mengineyo ya baadaye katika ripoti hii.

c.) Usalama

Usalama: ni mahitaji ya kimsingi kwa wanajamii na ambao umeonyesha kuleta wasiwasi mkubwa miongoni mwa Wakenya. Ripoti hii inayashughulikia masuala haya ya usalama kwa njia kadha. Inaitwika serikali na vyombo vyake vya utawala jukumu la kuulinda usalama wa raia. Inapendekeza mabadiliki muhimu katika vikosi vya polisi na vikosi vya majeshi kwa njia ambazo zitawafanya kuwajibika kwa taifa. Inapendendekeza mabadiliko kwa Mifumo Wa Haki kwa Jinai (Criminal Justice System) katika viwango vyake vyote. Mabadiliko haya yanatarajiwa kuwajengea raia utawala wa haki na ulio tekelezi, pia, watuhumiwa na wafungwa watashirikishwa katika mabadiliko haya ya kuhusu usalama.

d.) Kuilinda Katiba Na Kanuni Zake

Kwa kuhitimisha, tumependekeza kanuni kadha ambazo zitailinda Katiba, ili isifanyiwe mabadiliko ya haraka yenye nia mbaya, na pia kuilinda dhidi ya utawala mbaya na kuzitumia afisi za umma kwa njia za ufisadi. Tumependekeza matumizi mapana ya Tume huria, viwango vya uadilifu na uaminifu, na taratibu za malalamiko mapya na vyombo vya utekelezaji.

e.) Tuwasikilize Wananchi

Tume inaamini kuwa imefanya kadri ilivyoweza kuipata Katiba na maadili yake. Inatambua pia kuwa Katiba, hatimaye, ni kikaratasi tu. Ingawa ufanisi wake unategemea mbinu za ndani za utekelezaji, kimsingi kufaulu kwake kunategemea mielekeo ya umma na kujitolea kwao ili kuifuata Katiba. Ushirikishi wa asasi za raia katika taratibu za kisiasa na za kiKatiba ni muhimu katika kufaulu kwa Katiba. Hali ya serikali kujitolea kuufuata uKatiba ni muhimu pia katika kufaulu kwa Katiba. Hali ya serikali kuufuata ukatiba ni muhimu katika utekelezaji wa, na heshima kwa Katiba. Kile ambacho Katiba mpya itafanya ni kuibua kanuni, taratibu na asasi za kutekelezea nguvu za umma ili kuweza kuwajibika; Ni wajibu wa wananchi

na mashirika mengine kuhakikisha, wananchi na mashirika mengine kuhakikisha, kwa matumizi ya kura, kuyafikia mahakama, na nyenzo nyinginezo za uwajibikaji n.k kuwa, kanuni, taratibu na asasi hizi za Katiba zinakuwa na ufanisi. Uzito wa majukumu umewekewa viongozi wa kisiasa kuhakikisha kuwa wanaheshimu nia na lengo la Katiba na kufuata maadili ya kuvumilia, mapatano na kukuza vyama vya kisiasa vya taifa na miungano ya kisiasa. Tumependekeza kanuni za uraiamwema, pamoja na hizi na nyingine zitkazotoa majukumu ili kutofautisha matumaini ya katiba mpya. Wananchi na viongozi wao wanahitaji kupewa nafasi za kijifunza kuhusu maadili na taratibu za Katiba mpya na jinsi ya kutumia mbinu zake ili kuyatimiza maadili haya.

Mitaala ya masomo ya uraia ifanywe ya lazima shuleni. Itabidi wananchi wanapoisoma ripoti hii yetu wawe wakifikiria wajibu wao katika uhamasishaji na utekelezaji wa Katiba. Wananchi ambao, ni katika jina lao Katiba hii imetayarishwa, ndio hatimaye watakaokuwa walinzi wake (wa Katiba).

Licha ya matatizo yanayoikabili Kenya katika kuimarisha kanuni za kidemokrasia na kuufufua uchumi, matumaini ni mema kwa sababu Wakenya tayari wamejiandaa kwa mabadiliko. Tunaamini kuwa, iwapo Katiba itatekelezwa kwa uaminifu, inaweza kutupatia msingi wenye nguvu za wananchi ambazo zinaweza kutumika katika kuitekeleza Katiba hii, Kenya ina nafasi ya kuwa mfano mzuri katika Afrika nzima katika masuala ya kuhusu haki za kijamii, ushiriki wa kidemokrasia na serikali iliyo safi.

5. Waraka wa Katiba

a.) Mtindo Wa Kuutayarisha Mswada Wa Katiba

Katiba iliyopo imetayarishwa kwa njia ambayo mtu asiyekuwa mwanasheria hawezi kuielea bila kuchukua muda mrefu na kuwa na subira. Kwa hakika hata baadhi ya sehemu ni ngumu kwa mwanasheria kuelewa. Pamoja na hayo, inapatikana tu katika Kiingereza. Labda ni muhimu kuwa Katiba iweze kueleweka zaidi na msomaji yeyote ambaye ameelimika, kuliko ilivyo na sheria nyingine. La sivyo, inakuwa vigumu kuona jinsi ambavyo malengo ya Sheria ya Marekebisho kuhusu ushiriki, uwajibikaji na utekelezaji wa haki yanaweza kutimizwa.

Kuna uwezekano wa kutumia mtindo ulio rahisi katika kuutayarisha mswada na kikundi cha Watayarishaji Miswada kimedhamiria kufanya hivi. Kinatumia sentensi fupi fupi, hakirejelei sana sehemu nyingine za Katiba, kinatumia lugha ya moja kwa moja ambayo haizushi utata kama vile '*must'* badala ya *'shall'*; na inaepuka lugha ya Kiingereza isiyovutia na isiyokuwa ya kawaida. Mifano ya maneno ni kama *'whereby'*, *'provided that', 'such'* na

'notwithstanding'. Ilhamu ya kurahisisha kueleweka kwa Katiba imetokana na Katiba ya Afrika Kusini. Tunaamini kuwa matokeo ya juhudi hizi yatakuwa ni Katiba ambayo nakala yake ya Kiingereza itakuwa rahisi ya kueleweka na wananchi na pia rahisi ya kutafsiriwa katika Kiswahili na lugha nyingine. Tunaamini pia kuwa urahisi huu utatimizwa bila kupoteza chochote muhimu (hili ni rahisi kutimiza katika Katiba kwa sababu imekubalika kwa ni wajibu wa mahakama kutimiza majukumu ya waraka wa Katiba bali si kutiliwa vikwazo na mambo rasmi). Kikundi cha waandalizi wa mswada kinastahili kupongezwa kwa kutimiza mafanikio ya kurahisisha lugha ya mswada wa Katiba.

Kaida ya utayarishaji wa sheria nchini Kenya, ambayo inatokana na ile ya Uingereza, inahitaji kuwa neno *'man'* litumike ili kumaanisha pia *'woman'* na *'his'* itumuke pia kumaanisha *'her'* na kawaida. Ingawa hali hii inaeleweka kwa wanasheria, huenda isieleweke kwa raia na hata katika akili za wanasheria inaweza kuzua fikra ya kwamba daima ni lazima rais n.k. awe mwanamume. Si vigumu kutumia lugha ambayo haina utata huu. Ili kuusuluhisha utata huu, *'he'* au *'she'* na *'she* au '*he'* yanaweza kutumika na wakati mwingine tatizo lote likaepukika katika matumizi ya vifungu jumuishi kama vile raia na uraia (*citizens vs a citizen*)**.** Katika Afrika Kusini, waandalizi wa miswada walipiga hatua zaidi. Walibainisha wazi ya kuwa mtu wa jinsia yoyote anaweza kushikilia afisi au kutimiza majukumu yo yote, hata pale ambavyo muundo wa sentensi haukubainisha hivi: kwa hivyo, Katiba inasema, kwa mfano 'Ni lazima Muhasibu Mkuu awe Mwanamke au mwanamume mwenye uraia wa Afrika Kusini'. Pili Katiba inamtanguliza mwanamke kabla ya mwanamume katika kila hali ya kuwarejelea. Tatu, Waandalizi Wa Mswada walijiepusha na hali ambazo zingesababisha matumizi ya '*he au she*'. Mswada wa Katiba ya Kenya umechukua mwelekeo huu. La muhimu kufahamu ni kuwa utata ambao umeelezwa kuihusu lugha ya Kiingereza haumo katika Kiswahili kwa hivyo hatari ya kuibuka utata na ukengeushi wa kijinsia haiwezi kutokea katika nakala ya Kiswahili ya Mswada wa Katiba wala ripoti nyingine za Kiswahili.

b.) Muundo wa Katiba

Katiba si hadithi – ingawa inawakilisha kisa cha taifa. Inabidi iangaliwe katika ukamilifu wa ujumuishi wake. Namna sehemu moja inavyotenda kazi haiwezi kuangaliwa kwa peke yake mbali na sehemu nyingine.

Lengo moja – kama vile ulinganifu wa kijinsia au ushiriki – halitashughulikiwa katika sehemu moja tu. Hali ya Katiba kutenda kazi katika ukamilifu wake ina maana inayoangazia zaidi ya ujumla wa sheria na asasi zilizomo. Lakini utaratibu ni muhimu: namna ambavyo kanuni za haki za binadamu 'zilishushwa' toka Sura II katika Katiba ya 1963 hadi Sura V ilivyo katika Katiba ya sasa inaeleza mengi kuhusu umuhimu unaopewa haki za raia. Mswada wa Katiba ambao tumetayarisha unaanza na kifungu cha kuhusu

kanuni na uadilifu: Ni nini lengo la serikali. Lengo hili ni faida ya wananchi wa taifa – watu wote. Maadili ni yale ya uvumilivu, demokrasia na umuhimu na ushiriki wa wananchi. Kisha haki za binadamu zinaelezwa kwa undani, zikitanguliwa na kanuni za kuwahusu raia. Ni nani wananchi wa Kenya? Sehemu ya Katiba inayohusu ngazi za serikali inatoa umuhimu kwa uwakilishi wa wananchi kupitia bunge kabla ya kushughulikia wale wanaotekeleza utawala kwa niaba ya wananchi. Kisha inafuatia asasi ambazo zimewekwa ili kuhakikisha kuwa Katiba inaendelea kutimiza malengo yaliyokusudiwa: Mahakama, udhabiti wa mali ya umma, Tume ya haki za binadamu. Hatimaye zinafuatia taratibu za kubadilishia Katiba, kama itahitajika (ambazo pia ni taratibu za kuilinda dhidi ya mabadiliko ya kiholela au mabadiliko ya hila) na pia ya kuingiza Katiba mpya kwa utaratibu.

Katiba Mpya Imetofautiano Vipi na Katiba ya Zamani?

- Hii ni orodha ya njia maalumu zinazoonyesha jinsi mswada wa Katiba unavyotofautiana na Katiba ya zamani:
- Ni Katiba ya wananchi; inatambua uhuru wa wananchi, lugha iliyotumika na mtindo wake. Lugha yake "inazingatia ujinsia". Mswada wa Katiba unaungwa mkono na kujimuisha uelewano wa wananchi, na, utakuwa sheria kwa sababu wananchi wanataka iwe hivyo.
- Inaashiria masuala yanayoathiri wananchi – badala ya kuwa tu kama kanuni za miundo ya serikali.
- Ina utangulizi – falsafa ya kimsingi ya Taifa – na orodha ya kanuni za kuiongoza serikali na wananchi katika kupata na kufanikisha jamii yenye haki.
- Kuna masharti yaliyowekwa ya kuwahakikishia wananchi wote heshima bila kujali ukabila, dini, jinsi watu wanavyoishi ama mahali wanapoishi.
- Masharti ya uraia yana usawa baina ya wake na waume; yanatoa haki nyingi zaidi za uraia, zisizotegemea uamuzi wa warasimu.
- Masharti ya haki za binadamu ni mapana zaidi kuliko yalivyo kwenye Katiba ya zamani, yana shughulikia maendeleo ya kisasa katika ufahamu wa haki za binadamu, mikataba ya kimataifa kuhusu haki za binadamu, na masuala yaliyotolewa na wananchi kulingawa na fikira zinazohusu jinsi masharti ya Katiba iliyopo yalivyoteketeza, ama kutotekeleza kazi.
- Kuna sharti linalohakikisha utekelezaji wa masharti ya haki za binadamu, linalojumuisha mbinu maalumu zenye urahisi wa matumizi, pamoja na taratibu mpya zinazorahisisha huduma za mahakama – ukilinganisha na Katiba ya zamani iliyokuwa na utaratibu finyu na ambao ulitekelezwa hivi majuzi tu.
- Bunge litakuwa na kumbi mbili; Baraza la Taifa la wawakilishi na Baraza la Kitaifa la Wilava.

- Utaratibu wa uchaguzi utaunda bunge linalokaribia matarajio ya wananchi kuhusu vyama wanavyoviunga mkono, kuliko mfumo wa Aliyefika Mbele (first-past-the-post) uliotumiwa awali – ambao unaelekea kuunda serikali inayoungwa mkono na wapiga kura wachache. Mfumo uliopendekezwa bado una wabunge wawakilishi wa maeneobunge ili wananchi wahisi kwamba wanauhusiano na wale watu wanaofanya uamuzi utakaoathiri maisha yao.
- Si lazima mtu awe mwanachama ili aweze kugombea uchaguzi.
- Vyama vya kisiasa lazima vizingatie kanuni maalumu, za kidemokrasia na kuiheshimu Katiba ili vipate kusajiliwa na kupendekeza wagombeaji uchaguzi.
- Vyama vya kisiasa vitakuwa na haki ya kupokea kiasi fulani cha msaada wa fedha za umma; kwa dhamira ya kupunguza athari za ufisadi wa ufadhili wa kibinafsi. Itawalazimu pia kutaja hadharani misaada mingine ya kifedha waliyopata kutoka kwingineko na namna walivyoitumia.
- Bunge limeimarishwa; linaidhinisha uteuzi katika vyeo vingi muhimu, aidha lina wajibu mkubwa katika mambo ya nje, ya udhibiti wa bajeti na katika usimamizi wa serikali zaidi kuliko awali.
- Wabunge hawatakuwa na uwezo wa kujipangia mshahara wao wenyewe tena.
- Kuna utaratibu ambao unawawezesha wapiga kura katika maeneobunge kumfanya mbunge wao awache wadhfa wake afisini.
- Kutakuwa na kanuni za uongozi zitakazotawala tabia za wabunge na viongozi wengine; na asasi ya utekelezaji wa kanuni.
- Rais bado anachaguliwa na wananchi lakini lazima apate zaidi ya asilimia hamsini (50%) za kura ya walio wengi; na wingi wa asilimia ishirini (20%) katika mikoa mingi. Ikiwa hakuna mgombeaji atakayeupata ushindi huu, itabidi pawe na kura ya uamuzi-mkata baina ya wagombea wawili wenye kura nyingi zaidi. Mgombea atakayepata kura nyingi zaidi ndiye takayekuwa Rais.
- Rais anauwezo mchache zaidi kuliko wali; wadhifa wake unaelekea kufanana na wa Rais mstahiwa anayewakilisha taifa zima, na pia muhifadhi wa Katiba; anayehakikisha kuwa serikali haikiuki mipaka yake, na kuwa sehemu ya chombo kinachohakikisha kuheshimiwa kwa Katiba.
- Serikali inaongozwa na Waziri Mkuu katika utelekezaji wa shughuli za siku kwa siku. Huyu atachaguliwa kutokana na wabunge na atahitajika kuungwa mkono na wabunge wengi.
- Mawaziri si wabunge; wabunge wanapoteuliwa kuwa mawaziri, watalazimika kuacha uanachama wao wa bunge.
- Waziri Mkuu anaweza kutarajiwa kwamba ajiuzulu kwa kura ya kutokuwa na imani bungeni. Isipokuwa kuwe na kura ya kutokuwa na imani ama tatizo nyeti lisiloweza kutatuliwa na Rais, uchaguzi utawekewa tarehe yake muhimu.

- Kutakuwa na mfumo wa kupunguza na kusambaza mamlaka ya serikali mfumo huu umejuishwa kwenye Katiba na umejileta katika wilaya, ambazo pia zitaunda Baraza la mkoa. Tena ni lazima kuwe na mabaraza ya kata na mitaa.
- Utawala wa mikoani utafutiliwa mbali.
- Kutakuwa na mahakama ya juu katika uongozi wa mahakama itakayokuwa na majaji wapya.
- Patakuwa na mfumo mbamo Jaji waliopo watapewa fursa ya kufaidi kutokana na Mfuko wa Kustaafu. Wale wasiochukua watachunguzwa upya na watapelelezwa hasa kuhusu madai ya uhalifu. Wale watakaoendelea watalazimika kula kiapo cha kutii na kukubali kanuni za maongozi yaliyopo.
- Hadhi ya mahakama za Kadhi imeongezwa katika Katiba.
- Uhuru wa majaji na tume mbalimbali na afisi kama vile Tume ya Uchaguzi na Mhasibu-Mkuu utaongezwa zaidi.
- Kutakuwa na kikundi mashuhuri ambapo watu watakwenda moja kwa moja, kuwasilisha malalamiko yao kuhusu kutokuwa na umakinifu kazini, ufisadi na maonevu ya huduma za umma, na hata polisi.
- Polisi wa utawala watapoteza hali ya vikosi vyao
- Polisi wanatakiwa kushughulikia maslahi ya jamii zaidi na utawala wao utawashirikisho raia zaidi.
- Ardhi yote nchini itawekezwa (itahifadhiwa) katika Tume ya Ardhi inayosimamia ardhi hiyo kama amana ya taifa. Usimamizi wa ardhi wa mamalaka ya umma, lazima uwe lengo lake la kwanza ni kulinda haki za wananchi, na umuhimu maalumu lazima upewe haki zilizo-chini ya sheria za mila.
- Serikali lazima ichukue hatua za kulinda mazingira na kufanikisha maendeleo endelevu.
- Rasilmali za taifa lazima zitumiwe kilinganifu kwa njia itakayonufaisha taifa zima wala sio wateule ama sehemu fulani za nchi.

SURA PILI

MSWADA WA KATIBA
MAADILI, KANUNI, HAKI NA SERA

1. Utangulizi

Mawasilisho mengi yaliyotolewa kwa Tume yalihimiza kwamba Katiba mpya lazima iwe na utangulizi. Utangulizi wa Katiba kawaida hutumiwa kubainisha baadhi ya kanuni msingi za taifa, na kuthibitisha kwamba Katiba imejikita katika wananchi uwezo na kuwepo kwake pamoja na uwezo wa kisheria vyatokana na wananchi. Ni kawaida kurejelea kwa kiasi, vipengele vya kihistoria. Utangulizi lazima usisitize mambo yanayounganisha nchi. Rai yake itakuwa katika ujumuishi wake. Lazima ivutie hisia za uwajibikaji, kukiri mambo yaliyopita na matumaini ya nyakati zijazo, katika mtindo wa moja kwa moja, unaoashiria mtindo wa waraka wote. Utangulizi hauna haja ya kuwa mrefu – hasa kwa sababu kutakuwa na maelezo ya maadili na matumaini ya Katiba yatakayofuata.

Mawasilisho yadhihirisha kwamba yafuatayo lazima yatajwe:

- Wananchi katika wingi wa tofauti za kikabila, kidini na kitamaduni.
- Umuhimu wa wananchi kama msingi wa serikali.
- Historia ya taifa pamoja na kugombea uhuru, na nafasi ya waliopigania uhuru na majeraha ya kipindi cha baada ya uhuru.
- Kuendelea mbele katika nyakati zijazo.
- Maadili ya demokrasia, ukatiba na utawala wa sheria.
- Kumkumbuka Mungu.

2. Maadili Na Matumaini Ya Taifa

Miswada mingi ya Katiba iliyotayarishwa hivi majuzi ina kile kinachoweza kufafanuliwa kama ‘kanuni tekelezi za sera ya serikali.’ Mara nyingi, kanuni hizi zimetumiwa kutambulisha kiwango cha ulinzi wa haki za kiuchumi, kijamii na kitamaduni –lakini ulinzi huo si mwingi kama ule ambao ungapewa haki za kawaida za kijamii na kisiasa kama vile, uhuru wa kujieleza. Mswada wa Katiba ya Kenya haubainishi tofauti baina ya haki za kijamii, kisiasa kiuchumi na kitamaduni kwa njia hii. Haki kama zile za elimu, afya, na chakula (haki kamili za kiuchumi) zimependekezwa kufungamanishwa katika kanuni za jumla za haki ya binadamu.

Ingawaje hii haimaanishi kwamba hapana nafasi ya kueleza maadili ya kimsingi ya serikali na Katiba (lakini hizi zisiitwe “kanuni tekelezi za sera ya serikali.” Kwa sababu kifungu hiki kina maana ya wazi kwa mawakili) Mahali hapa ndipo panapofaa katika Katiba, kuziweka kanuni za kimsingi zilizoongeza matayarisho ya Katiba na ambayo yangeongoza serikali na taifa

Katiba katika kutekeleza Katiba. Jambo hili lisijaribu kutoa pingamizi kwa vyama vya kisiasa katika kuunda na kuendeleza sera na itikadi zao. Lakini ndilo la karibu linaloweza kupatikana kuhusu itikadi yoyote ile ya taifa. Katika hali ya kimaumbile itakuwa na hali bora ya kilimwengu: Kenya haikuumbwa pekee, hivyo siku zijazo uhusiano na nchi nyingine utaongezeka, hasa Wakenya wanatarajia uhusiano baina yake, muungano wa Afrika Mashariki na Umoja wa Afrika kuimarika zaidi.

Ni dhahiri kwamba ni katika sehemu hii ya Katiba ambamo mtu angetazama ili apate ufahamu wa kumbukumbu baadaye kuhusu maadili ya Katiba; kwa mfano vyama vya kitaifa lazima wafuate maadili hayo, na visisajiliwe ikiwa malengo yao yatakiuka na kuyageuza maadili. Rais, ama wale wanaoingia afisini watawajibika kumheshimu kikatiba – na huu si uwajibikaji wa kufuata orodha ya sheria hii, bali hata maadili pia

Jambo jingine ni lile linalohusika na matumaini na malengo ya taifa. Hili linadhihirisha aina ya jamii ambayo taifa imelenga kuifikia chini ya Katiba. Maadili yatakuwa maalumu zaidi ya yale yaliyo ndani ya utangulizi, isipokuwa kwa umuhimu wa yale yanayopatikana Katiba kanuni za Haki za Binadamu. Mswada uliopendekezwa unaelezea yafuatayo:

- Umuhimu (uhuru) wa wananchi.
- Umoja wa Taifa hasa ukirejelea Kiswahili na lugha nyinginezo.
- Usawa na thamani ya jamii zote.
- Demokrasia, utawala mwema na utawala wa kisheria.
- Haki ya binadamu
- Usawa uliolingana kwa watu wote; kujumlisha waume na wanawake;
- Kujibidisha ili kufanikisha mahitaji ya kimsingi.
- Kushiriki, na uwazi katika Katiba shughuli za umma.
- Uadilifu wa kibinafsi na kitaifa.
- Kuvumilia na kuheshimu maoni na imani za watu wengine.
- Mila na maadili ya Kenya?
- Kuuleta utawala karibu na wananchi
- Utatuzi wa mabishano kwa njia ya amani.
- Umataifa na umoja na Afrika?

Kuna jambo la mwisho kuhusiana na masharti haya katika sheria; ni wazi kwamba mengi ya masharti hayo hayawezi kufanywa mada za mabishano ya kisheria kama vile masharti ya haki na wajibu maalum. Katiba itaweka wazi kwamba maadili na kanuni hizi viongoze taifa na asasi zake, na kwamba asasi hizi ni pamoja na mahakama.

3. Watu wa Kenya

Masharti ya Katiba iliyopo sasa kuhusu mtu aliye raia wa Kenya yanatatanisha katika athari na lugha yake ya kisheria. Zipo njia kadha za

kuwa Mkenya; kwa kuzaliwa nchini na mzazi ambaye ni Mkenya, na kwa kuzaliwa nje ya nchi na baba ambaye ni Mkenya. Katika miktadha mbalimbali watu wana haki ya kusajiliwa kama raia wa Kenya ikiwa hawakuzaliwa hivyo, ama wanaweza kutuma maombi ya kutaka kusajiliwa kama raia, na katika muktadha mwingine, mtu anaweza kutuma maombi ya kutaka kuwa raia wa Kenya kwa njia ya utaratibu wa kuandikisha uraia. Masharti haya hutolewa kwa tahadhari-yanasema. Watu fulani "wanaweza" kupewa uraia. Hayamruhusu mtu kuwa raia wa Kenya na raia wa nchi nyingine kwa wakati mmoja. Hayatafakari uwezekano kwamba mtu anaweza kuwa na haki ya kuishi nchini Kenya, bila kuhitaji kupigisha upya kibali chake cha viza mara kwa mara bila kuwa raia wa nchi. Wanaruhusu kumwondolea uraia mtu ambaye hakuzaliwa Mkenya, bali si kwa mtu aliyezaliwa raia wa nchi hivyo kutofautisha kati ya aina hizi mbili za uraia. Hatimaye, wanabagua kati ya wanaume na wanawake; hasa kwa sababu, mke wake Mkenya, ana haki ya kuwa Mkenya, lakini kwa mke Mkenya, mume wake hawezi kupata uraia. Wake mwanamke mkenya hawezi kupata uraia. Mtoto aliyezaliwa nje ya Kenya na baba mkenya anakuwa raia moja kwa moja lakini mtoto aliyezaliwa nje ya Kenya na mama Mkenya hawezi kuwa raia. Sheria ya marekebisho ilichagua fani ya mwisho na kuieleza kwa njia maalumu.

Mawasilisho kwa Tume

- Walipendekeza kuondolewa kwa ubaguzi baina ya wanaume na wanawake.
- Maoni kuhusu uraia wa nchi mbili yaligawanyika; wale walioafiki walikuwa watu waliozaliwa na kuishi ng'ambo pamoja na raia wanaotoka katika jamii za wachungaji ama jamii nyingine wanaoishi mipakani na ambao mtindo wa maisha yao huwahitaji kuvuka mipaka ya kitaifa mara kwa mara.
- Baadhi ya watu walifikiria kwamba wote waliozaliwa nchini wangekuwa raia.
- Mapendekezo katika mswada wa Katiba ni kama yafuatayo (masharti ya kuwa raia yamo katika sanduku).
- Raia wote wako sawa katika kufurahia kwao haki za uraia. Hii ni pamoja na usawa wa kupoteza uraia. Kwamba wakazi nchini wanapewa haki na wajibu; kwamba serikali iwe ya usawa na isiyodhulumu.
- Kuna haki ya kupata kitambulisho na pasipoti (hati ya usafiri).
- Lazima kusiwe na ubaguzi kuambatana na jinsia.
- Uraia wa nchi mbili unawezekana.
- Lazima kupitishwa sheria inayotenga kundi la watu walio na haki ya uraia baada ya kuishi nchini kwa kipindi kinachotosheleza.

Raia Wa Kenya Ni Nani?

- Mtu aliyezaliwa Kenya ambaye mzazi wake yeyote yule ni raia wa Kenya.
- Mtu aliyezaliwa nje ya Kenya ambaye mzazi wake ye yote yule ni raia wa Kenya.
- Mume au mke wa raia wa Kenya anaweza kuwa raia pia.
- Mtu aliyechukuliwa na kulelewa na Mkenya anaweza kuwa raia.
- Mtoto anayepatikana nchini asiyejulikana asili yake ni Mkenya.
- Watu wasio na nchi kwa sababu ya historia na ambao wamezaliwa Kenya kabla ama baada ya uhuru ni Wakenya
- Wengine wanaweza kutuma maombi ya kutaka uraia.

4. Haki za Binadamu

Tangu wakati wa mapinduzi wa Marekani haki za binadamu zimekuwa sehemu muhimu ya Katiba. Masharti ya Katiba kuhusu haki ya binadamu yamekuwa sehemu muhimu ya Katiba. Masharti ya Katiba kuhusu haki ya binadamu zimeendelea kuwa tatanishi na pana. Masharti ya kitaifa kuhusu haki ya binadamu yamesaidiwa na kutiwa nguvu na mikataba ya kimataifa inayoweka majukumu ya mataifa na vitengo vinginevyo ili kupendekeza na kulinda haki, na kuanzisha utaratibu wa kimataifa, wa kusimamia utekelezaji wa kitaifa wa masharti hayo. Haya masharti ndiyo njia mojawapo muhimu za kutangaza maadili ya taifa na kufafanua madhumuni ya serikali. Leo, ni vigumu kufikiria Katiba bila sheria ya haki za binadamu.

Haki ni hali za kimaumbile katika binadamu na wala hazitolewi na kupewa serikali wakati watu wanapounda jamii ya kisiasa. Haki ni muhimu katika kuwawezesha wanadamu kuishi maisha ya uadilifu. Kufikia upeo wa uwezo wao, kutosheleza mahitaji yao ya kimwili na kiroho n.k; haki huwapa uwezo raia na wakazi; huwapa nafasi muhimu katika vyombo vya serikali na haki ya kuhusiana na kulinda maslahi yao dhidi ya kuvuja sheria kwa serikali, zinapunguza uwezo wa serikali na kuilinda dhidi ya uovu wa ziada wa waliowengi. Haki nyingi kama vile, haki ya kupiga kura, uhuru wa kujieleza na vyombo vya habari na kupata habari ni muhimu katika kustawisha na kulinda demokrasia, pamoja na uwajibikaji wa mamlaka ya umma. Haki hutoa ithibati ya kushughulikiwa kwa hali maalum za jamii za walio wachache na wasiobahatika. Haki hufafanua uhusiano uliopo baina ya serikali na wananchi; kwa hali hii, haki hutoa utaratibu wa Katiba yote.

Sheria ya marekebisho inazipa haki za binadamu umuhimu mkubwa. Inaelekeza moja kwa moja au kwa kuashiria kwenye ulinzi wa haki za binadamu na demokrasia (demokrasia kama inavyoeleweka leo haiwezi kuwepo bila haki – haki za kutangamana, kushiriki, kupiga kura na kuwa

wagombea uchaguzi, kujieleza, ulinzi wa walio wachache). Usawa wa kijinsia na masuala ya ubaguzi kwa jumla; kushughulikia mahitaji ya kimsingi ya wananchi kwa njia ya kuanzisha utaratibu wa usawa wa ukuaji wa kiuchumi na usawa wa matumizi ya rasilmali ya taifa, huleta usawa wa haki kwa wote na haki za mtoto.

Haki za binadamu ni muhimu katika Katiba iliyopo pia. Sheria ya haki za binadamu inawahakikishia watu haki zifuatazo:

- Haki ya uhuru na kuishi;
- Haki za kulindwa kutokana na utumwa; kazi ya kulazimishwa; mateso, hali ya kudunishwa;
- Ulinzi wa haki za kuwa na rasilmali ya kibinafsi;
- Haki za kulindwa dhidi ya kusakwa na upokonyaji;
- Kulindwa kwa haki za kuwaza, kujieleza, kutangamana na ushirika, na maendeleo;
- Haki ya kutobaguliwa kulingana na ujinsia, kabila, mahali, nchi uliyotika ama uhusiano mwingine nchini, maoni ya kisiasa, rangi au imani.
- Haki ya kustahiwa mbele ya mahakama huria iliyoundwa na sheria katika kesi ya ugaidi, pamoja na haki ya kuonekana kutokuwa na hatia hadi ithibitishwe hivyo, na haki ya kuwa na wakili.

Upana wa ulinzi wa haki za binadamu si mkubwa vile kulingana na wale wanaolindwa; na katika aina za haki zinazolindwa; na katika kadiri ya vipimo vya wale waliofungamana na majukumu yanayohusiana na haki. Hakuna masharti yaliyotolewa kwa haki za kiuchumi na kijamii; hakuna chochote kinachowahakikishia Wakenya mahitaji yao ya kimsingi. Hapana chochote kuhusu haki za umoja (amani, maendeleo ama mazingira). Haki za kitamaduni kama zilivyo zinadhulumu; katika hali ya sheria ya kimila, utamaduni unaruhusu vibadala vya haki za usawa ambavyo haviwasaidi wasichana na wanawake. Hakuna kanuni maalum kwa walio wachache; Katiba haisemi chochote kuhusu haki za mtoto, mzee wala watu walemavu; ulinzi dhidi ya ubaguzi upo tu kwa raia wa Kenya. Hata katika enzi ya haki za kijamii na kisiasa, si wote wanaolindwa; kwa mfano hakuna utambuzi wa ubinafsi ama haki za kisiasa au aina nyingine za ushirikiano wa wananchi; haki ya mshatakiwa kuhukumiwa bila upendeleo haiwajibishi serikali kumpatia mshtakiwa wakili hata katika kesi ambayo hukumu ya kifo yaweza kutolewa. Katiba nyingi mpya zimeweka wazi haki za sehemu maalum za jamii. Sehemu hizi kwa muktadha wa Kenya ni pamoja na jamii za wachungaji, watumizi, wafungwa, mahabusu, wakimbizi, na viongozi wa vyama vya wafanya kazi. Katiba hizi haziwapi raia haki ya kupata habari iliyohifadhiwa na utawala. Hii yapunguza nafasi za wananchi kuweza kuchunguza umakinifu wa utendaji kazi, uadilifu na uaminifu wa mamlaka ya umma. Inayawekea mashirika na sekta za kibinafsi majukumu machache kuhusu kuheshimu na kupendekeza haki za kimsingi. Katiba yenyewe

inaruhusu vipengele vikiukavyo kaida hata katika haki inayoziunda. Baadhi ya haki huwa zinaahirishwa wakati wa vita ama wakati wa kutangazwa kwa 'hali ya hatari'. Sheria inayopitishwa kwa kuchunga maslahi ya ulinzi, nidhamu za umma, uadilifu na afya ya umma au kuthibiti wananchi wanaohamahama,yaweze kuondolewa katika haki na uhuru wa kiKatiba. Ulinzi dhidi ya ubaguzi hautumiki kwa ulezi wa kupanga, ndoa, talaka, mazishi, ugawanyaji wa rasilmali wakati wa kifo ama mambo mengine ya sheria ya kibinafsi. Kwa kweli, sheria za kimila zinazobagua wanawake au wasichana, au mtu mlemavu hazimo katika masharti ya haki za binadamu.

Sheria ya haki ya binadamu ni hafifu kulingana na vigezo vya kisasa katika utaratibu wa utekelezaji na asasi; haina vyombo maalum vya kupokea malalamiko ama Tume ya Haki za Binadamu au utekelezaji wa haki; hapana chombo kisaidizi cha kisheria cha utekelezaji haki; kuna suluhu chache tu zinazofaa. Tangu sheria ilipoandikwa, utaratibu mpya wa kimataifa umeanzishwa kwa ajili ya kuendeleza utekelezaji wa haki za binadamu, na huu haudhihirishwi kwenye Katiba.

Mawasilisho mengi yaliyotolewa kwa Tume yalijikita zaidi ama kuashiria ulinzi bora zaidi wa haki za binadamu, bali si kwa manufaa ya wale wanaotoa mwasilisho peke yake. Wananchi walidai ulinzi bora wa haki zao wenyewe – hasa makundi yaliyobaguliwa kama vile wanawake, watu walemavu na makundi ya kikabila na kidini. Wanataka maslahi bora kwa watoto wa mitaani – na watoto kwa jumla, ikiwemo watoto wakimbizi, watoto walemavu na watoto wa kike. Mahitaji ya kimsingi ya jamii; chakula, maji na makao yanahitaji kutekelezwa.

Wakati mwingine haki hufikiriwa kwamba inajumlisha aina mbalimbali kama haki za kisiasa na raia; ulinzi wa maisha na uhuru, haki za uraia kama vile haki ya kushirikiana na kutangamana, uhuru wa kujieleza, haki za kisiasa, haki ya kupiga kura na haki ya kushiriki katika shughuli za umma, ndizo haki bora zaidi zilizoanzishwa na zinazojulikana. Kundi jingine ni kama vile haki za kijamii, kiuchumi na kitamadumi.

Mswada Wa Katiba Unawafanyia Nini Watoto?

- Yajaribu kuhakikisha kuwepo kwa amani na ufanisi kwa nyakati zijazo
- Yawapa watoto haki sawa kama watu wazima – isipokuwa pawe na sababu nzuri.
- Yafafanua jukumu la serikali kutoa elimu ya bure, kwa shule za msingi
- Inawapa haki ya kupiga kura wakipata umri wa 18, wanapoacha utoto.
- Katiba inajaribu kuhakikisha ufanisi na amani zaidi nyakati zijazo,
- Yafafanua jukumu la serikali kufanya kazi ili waweze kutoa mchango wa kugharamua elimu katika viwango vingine,
- Inalinda haki ya likizo ya zingizi (au ya kujifungua mtoto),
- Yasema kwamba watoto wa kupanga wanaweza kuwa Wakenya,
- Yawapa watoto haki ya kusajiliwa wanapozaliwa,
- Yafafanua majukumu ya wazazi na jamii, ya kulinda watoto,
- Yatoa haki ya kupata afya kwa wote,
- Yatoa haki ya kuwa na mazingira bora,
- Yatoa haki ya kuwa na chakula na maji (ambayo lazima serikali isiingilie bali ifanye kila juhudi kuilinda na kuhakikisha ipo.
- Watoto wasilazimishwe kuhudhuria mikutano ya kidini dhidi ya kupenda kwao ama kwa wazazi wao
- Kutoa jukumu la lazima kwa serikali la kutekeleza makubaliano pamoja na mkataba kuhusu haki za watoto.

Ufuatao ni uchunguzi mfupi wa masharti katika mswada wa Sheria za Haki za Binadamu:

- Haki zinazolindwa katika mswada wa Katiba zinajumlisha haki za utu, usawa, kutobaguana, utamaduni na dini. Zinashughulikia masuala ya kimsingi ya jamii; haki ya kushughulikiwa kwa usawa wa heshima miongoni mwa watu wengine katika jamii. Pamoja na hizi, tunaweza kuongeza haki ya faragha.
- Halafu kuna haki ya sehemu maalumu za jamii; wanawake, walemavu, watoto, wazee, wakimbizi. Hizi zinasisitiza kwamba makundi haya yana haki ya kupata haki hizi zinazosherehekewa na watu kwa jumla kutokana na hisia kwamba baadhi ya makundi haya yametengwa, pembeni mwa jamii. Basi masuala maalum yanayohusu makundi haya na majukumu ya jamii kuyahusu makundi hayo yanabainisha.
- Haki za ushirikiano wa kisiasa pamoja na haki ya kupiga kura, uhuru wa kutoa maoni, wa kujumuika na ushirika ni za kawaida katika Katiba. Tumeongeza haki ya hivi karibuni; ile ya kuweza kupata habari inayohifadhiwa na utawala, ambayo mara nyingine huitwa uhuru wa kupata taarifa.
- Haki za watu walioshitakiwa na makosa ya uhalifu, kwamba washughulikiwe bila maonevu wanaposhikwa na kuwekwa kizuizini, na halafu kuhukumiwa kwa njia ya haki pia kwa kawaida hupatikana katika Katiba. Pendekezo hilo linaimarisha haki hizi kwa kiwango fulani

Aidha, ongeza haki ya wafungwa ambazo ni nyongeza mpya katika haki za binadamu, na inashughulikia masuala nyeti yaliyojitokeza kwenye mawasilisho yaliyotolewa kwa Tume.

- Mswada pia unapendekeza kufutiliwa mbali hukumu ya kifo. Mawasilisho mengi yalipendekeza hatua hii.
- Haki za kuwepo kwa utu wa kimsingi inajumlisha si tu muelekeo wa kiheshima, lakini pia inahitaji kufikia viwango vya chakula, afya, malazi na elimu. Hapa jukumu la serikali ni katika kuheshimu, kupendekeza na kufanikisha haki.
- Muktadha wa kazi nao una baadhi ya haki; haki ya kuchagua kazi yako, haki ya kushughulikiwa bila mapendeleo kazini, ujira wa sawa kwa mume na mke, na kwa vigezo bora vya afya na usalama kazini. Katika muktadha wa familia pia kuna haki ya kuchagua kuolewa (kuoa) ama kutoolewa, (kutooa) na haki za usawa za kifamilia.
- Mbinu ya utekelezaji wa haki za binadamu ni thabiti kuliko ilivyo katika Katiba iliyopo. Kutakuwa na Tume ya Haki za Binadamu itakayopokea malalamiko ya kibinafsi kuhusu ukiukaji wa haki za binadamu. Itakuwa na uwezo wa kusuluhisha mabishano kwa kupatanisha makundi husika na pia kwa kupendekeza fidia. Hakuwa na wajibu wa uwekaji wa sheria na sera za serikali zinazorekebishwa – pamoja na kuzingatia. Sheria iliyopangwa – kuona ikiwa wametoshelezwa na viwango vya haki za binadamu. Katiba pia inaruhusu kwamba masharti ya haki za binadmu yanapotumiwa, mahakama na watu wengineo lazima wajaribu kufikia lengo la haki za binadamu. Ni lazima watazame jinsi haki za binadamu zilivyoendelea kwingineko.
- Kenya inashiriki katika baadhi ya mikataba ya kimataifa ya haki za binadamu (kama ile ya haki za mtoto na uangamizaji wa ubaguzi dhidi ya wanawake). Chini ya mikataba hii Kenya yatakikana yenyewe binafsi kuripoti mara kwa mara kuhusu utekelezaji na mafanikio yake katika kuvifikia vigezo vilivyowekwa. Mashirika nchini pia yana nafasi ya kutoa maoni kuhusu utekelezaji na mafanikio ya utawala kuhusu haki za binadamu. Ripoti ya utawala halafu itajadiliwa katika kamati ikiyoundwa kusimamia kila mkataba. Juhudi za Kenya katika kufanikisha jukumu hili la kuripoti zimekuwa za kutoridhisha. Ripoti ya serikali halafu itajadiliwa katika kamati iliyoundwa kusimamia mkataba.

Katiba imefanya utekelezaji wa jukumu hili kuwa sheria nchini Kenya – pia kuwezesha ripoti zake ziwafikie wananchi na kutoa nafasi ya kutosha kwa mjadala nchini.

- Mwisho, Katiba ina jambo la kusema kuhusu miktadha inayoruhusu upunguzaji ama kuwekwa kando haki kwa muda, kulingana na maslahi ya umma. Ni muhimu sana kwamba uwezekano huu uwe mchache sana ama kutakuwa na hatari ya Katiba kutoa haki kwa mkono mmoja na kuondoa kwa mkono mwingine. Kwanza kuna uwezakano kwamba haki zilizotolewa ni chache kuambatana na maslahi ya jamii, au katika maadili mengine yanayohitaji kulindwa. Mfano rahisi ni kuwa uhuru wa kutoa

maoni hauwezi kuwekwa bila kuwa na mipaka – ni lazima uheshimu sifa za watu wengine. Ingawaje hali ya kimsingi ya haki hiyo lazima iheshimiwe. Imependekezwa kuwe na kanuni ya jumla inayosema, haki zinaweza kuwekewa mipaka lakini masharti yake ya dhati yanahitajika: yenye busara na halali katika jamii ya kidemokrasia na wazi kuambatana na utu wa kibinadamu, usawa na uhuru, kwa kuzingatia hoja zote zinazofaa. Hoja za kimsingi yabidi zibainishwe ili ziongoze mahakama.

- Halafu kuna uwezakano wa kutangaza hali ya hatari. Baadhi ya haki zitahitaji kuahirishwa (kuwekwa kando) wakati wa hali mbaya ya hatari ya kitaifa vita, ama mkasa. Mswada wa Katiba unaweka vikwazo kuelezea miktadha ambayo tangazo la hali hatari laweza kutumiwa, wakati linapoweza kutumiwa na wale wanaoweza kulitangaza (ni lazima liwe chini ya usimamizi wa Bunge), na zile haki ambazo zitapungua wakati wa hali hiyo. Aidha, uangalifu maalumu wahitajika kwa watu waliotiwa kizuizini wakati kama huo.

5. Ardhi, Mazingira, Uchumi na Maliasili

Ardhi ni msingi wa uchumi wa Kenya na ni maslahi ya watu wengi moja kwa moja ama kwa kuashiria. Shunguli za watu wengi Kenya ni kilimo na ufugaji. Mauzo yake muhimu katika nchi za nje ni chai, kahawa, maua na kilimo cha bustani. Watalii huja kwa sababu ya mbuga za wanyama na ufuo wa pwani. Maisha ya wakulima, wachungaji na wanaoishi misituni yamefungamana kijumla. Hali hii haikutofautiana sana na ile ya wavuvi.

Ile tajriba ya wakati wa ukoloni watu walipopokonywa ardhi yao yote, na wengi kupokonywa haki zao za kumiliki ama kuishi au kutumia sehemu za ardhi zilizokuwa za mababu zao, yaongeza mielekeo mipya –mmoja ni hadi ya kuendeleza hisia za unyanyasaji kuhusu suala la ardhi. Maendeleo baada ya uhuru yameshindwa kushughulikia kunyimwa kwa wengi ambapo mbinu mpya za kuhodhi ardhi kwa watu wachache, uharibifu wa ardhi na watu wengine, zimeoudwa na kuimarishwa. Wengi wasio ardhi wanahisi kuwa kupata ardhi ndilo tumaini lao la pekee. Wengine ambao pengine wana ardhi, hawawezi kutosheleza haja zao kwa sababu ploti zao ni ndogo sana, ama mapato ya ukulima ni machache zaidi. Ardhi, ukabila kujitambulisha na hali za maisha vimefungamana sana. Kwa wengine ni hasira, kuleta hali ya wasiwasi baina ya makabila, na wakati mwingine mashambulizi. Nchini kwa jumla na katika jamii nyingi masuala ambayo hayajatupiliwa yanaleta ugumu wa kuendelea mbele.

Sheria ya marekebisho yasema kwamba katika kurekebisha Katiba, wananchi wa Kenya:

> Watachunguza na kurekebisha nafasi ya mali na haki za ardhi, zikiwa ni pamoja na ardhi ya kibinafsi, ardhi ya serikali na ardhi wakfu katika utaratibu wa Katiba na sheria ya Kenya, na kupendekeza uboreshaji

utakao hakikisha hali ya kufurahia manufaa ya ardhi na haki nyinginezo za mali ya asili.

Sheria pia inataja usawa wa kufikia rasilmali za kitaifa kama mbinu ya kuyafikia mahitaji ya kimsingi na maendeleo ya uchumi. Huu ni utaratibu anao huunganisha masuala ya mazingira na maliasili.

Chini ya Katiba ya Majimbo ya 1963, haki zote za serikali za ardhi zilikabidhiwa wilaya zilizokuwa na ardhi hiyo; yaani hii ni pamoja na 'ardhi ya serikali' ardhi uliyokuwa huru na ardhi iliyokodishwa kwa mkataba (mkataba ya kukodi unapomolizika, ardhi hurudi serikalini). Ardhi yote katika "makonde ya wenyeji' ilibadilishwa ikawa "Ardhi wakfu" na ilishikiliwa na mabaraza ya wilaya. Mabaraza yatakikana kushikilia ardhi hii kwa manufaa ya wale walioishi ndani yake, na walihitajika kutambua haki chini ya sheria ya kimila iliyomiliki ardhi hiyo wakati masharti ya Katiba yaliyohusu upunguzaji na ugawanyaji wa uwezo yalipofutwa, Ardhi wakfu ilibaki na mabaraza ya wilaya, lakini haki za ardhi zilizokuwa zimepewa wilaya zilihamishwa na kupewa utawala mkuu. Hali hii bado ipo, lakini Katiba sasa imenyamaza kuhusu ardhi isipokuwa ile ardhi wakfu.

a.) Mambo ambayo Tume Iliambiwa na Wananchi Kuhusu Ardhi

- Watu wengi walisema kwamba masuala mengi ya usimamizi wa ardhi yangeshughulikiwa ni vyombo vya kieneo (mashinani).
- Walilalamika kuhusu unyakuaji wa ardhi: ardhi iliyotengwa kwa matumizi ya umma/jamii ilipewa wananchi wa tabaka teule; hii ni pamoja na kuwapa watu nafasi iliyotengewa mabarabara ama kunyakuliwa (hali inayofanya ujenzi wa barabara, nyakati zifazo kuwa mgumu), maeneo ya misitu yameondolewa katika machapisho ya magazeti ya serikali na kupewa watu binafsi ambapo misitu imekatwa bila kujali mazingira na rasilimali ama jamii zinazoishi humo, masoko, makaburi ama vyoo vya umma vimepewa watu binafsi.
- Walilalamika kwamba watu wengi waliokuwa na haki ya kupata hati ya kumiliki ardhi hawajaweza kupata nyaraka muhimu zinazohitajika. Athara za kunyanganywa ardhi wakati wa ukoloni bado zinahisiwa na baadhi ya jamii. Baadhi ya jamii wamepokonywa fursa ya kufika katika seheme zenye umuhumu wa kitamaduni. Watu walilalamika kwamba mabaraza ya wilaya yalitoa ardhi wakfu kwa watu binafsi. Sehemu chache za jamii zilitoa wito wa kurudisha haki za ardhi za jamii.
- Kulikuwa na malalamishi mengi kuhusu matatizo ya ardhi yaliyokuwepo kwa miaka mingi ya nyuma – mara nyingi matatizo hayo yalirejelea enzi za ukoloni. Kwa mfano, ambapo Wamaasai wanalalamika kuwa walipokonywa urathi wao wa ardhi wakati wa malaka ya kikoloni, Wapokot wanalalamika kwamba kwa upande wao walipokonywa ardhi na Wamaasai.
- Kuna sehemu kubwa ya ardhi isiyofanyiwa chochote. Ambapo watu wengine wanalilia uwezekano wa kuwa na ardhi, wengine hushikilia ardhi

kama kipengele chao cha uwezo, badala ya kutumia kwa usalishaji. Watu wengi waliomba kiwango cha juu zaidi cha ardhi ambacho kinaweza kumilikiwa na mtu binafsi ama shirika.

- Si matatizo yote yaliyo mashambani. Asilimia sitini na tano (65%) ya wakazi wa Nairobi na wengineo katika miji tofauti huishi kwenye mitaa ya vibanda.Wakati mwingi hawa ni maskwota wasiokuwa na haki zo zote, ama vifaa muhimu, na bila kichocheo cha kuwafanya waboreshe hali ya maisha. Unyakuaji wa ardhi ni tatizo kila mahali.
- Wasiwasi mwingi ulionyeshwa kuhusu uharibifu mbalimbali wa mazingira. Sababu za malalamiko ni kama vile uchafuzi wa ardhi, hewa na maji, kukata misitu, matatizo ya kutupa uchafu na maendeleo ya ujenzi wa makao yasiyo na mpango kamili.
- Lalamiko moja juu ya rasilimali lililotokeza kwa wingi lilihusu matumizi ya ardhi kama mbuga za wanyanya kwa manufaa ya taifa, lakini yakiwatenga wananchi wa eneo hilo. Sehemu ya Taita-Taveta ina takribani asilimia sabini na tano (75%) ya ardhi iliyo kwenye mbuga wa wanyama za taifa na ardhi nyingine iliyobaki iko mikononi mwa watu wachache sana, wakati wenyeji wakimiliki asilimia kumi na moja (11%) ya ardhi.. Ni kinaya kwamba takribani asilimia tisini (90%) ya wanyama nchini iko nje ya mipaka ya mbuga. Huu ni mfano wa kipekee unaohisika mahali pengi (eneo kubwa): kwamba wamepokonywa usimamizi wa rasilmali na hali za maisha yao.
- Mwisho: kuhusu uchumi kwa jumla, kulikuwa na mawasilisho kuhusu umuhimu wa kuhimiza maendeleo ya kisayansi na kiteknolojia na kulinda haki za watu wanaoendeleza sayansi na ufanisi mwingineo. Uhitaji wa kuzingatia mahitaji ya maendeleo ya nchi ulitajwa mara kwa mara katika sehemu zote za nchi.

Haitawezekana kwamba Katiba itatoa mpango wenye maelezo mengi utakaoshughulikia masuala ya ardhi kwa undani. Kinachoweza kufanywa na Katiba - na hiki ndicho kinacho pendekezwa na Tume – ni kuandaa kanuni ambazo ni lazima zitumiwe kama misingi wa sera ya ardhi na sheria katika nyakati zijazo. Kanuni hizi ziko sandukuni.

6. Mazingira

Kuhusu mazingira, baadhi ya kanuni za kimsingi zimeingizwa kwenye mswada wa masharti ya haki za binadamu: haki ya kuwa na mazingira masafi na kanuni za kimsingi za maendeleo endelevu. Maendeleo endelevu yanajumlisha wazo la kuwa na usawa wa maendeleo mongoni mwa watu walio hai ulimwenguni hivi leo, lakini pia, haki za vizazi vijavyo za rasilimali za ulimwengi lazima ziheshimiwe. Mawazo haya yataendelezwa kwa dhati katika sura ya Ardhi tukirejelea kwa kiasi fulani ile sheria ya Usimamizi na Uratibu wa Mazingira.

- Wale wanaofanya uamuzi na kutunga sheria lazima wazingatie kanuni zifuatazo za maendeleo endelevu; kushiriki kwa umma; kanuni za kitamaduni na jamii zinazotumiwa kwa kawaida na jamii yoyote nchini

kwa usimamizi wa mazingira ama mali ya asili; kanuni ya usawa baina ya vizazi vya sasa na vizazi vijavyo na baina ya wale wanaoishi wakati mmoja; kanuni ya mchafuzi hulipa na kanuni ya kutahadharisha.

- Serikali lazima iwalinde wanyamapori, maliasili za kimaumbile na kibaiolojia, na uchumi Kenya; kuhifadhi misitu, kuhimiza na panapowezekana haya yote yawepo.

Kanuni za Ardhi Katiba

1. Ardhi yote ni wa wananchi wa Kenya.
   - Watu watapata ardhi hiyo kulingana na mifumo ya umiliki kama ilivyo katika sheria.
   - Raia wa kigeni nchini Kenya hawatakabuliwa kumiliki ardhi isipokuwa iwe ni kupitia mfumo wa kukodi ardhi.
2. Ardhi nchini Kenya itaainishwa kama ya umma, ya binafsi, na ardhi ya jumuia.
3. Ardhi ya umma itafafanuliwa na kuwekwa kama ardhi amana kwa wananchi nchini Kenya kwa misingi ya kisheria anayoelezea aina ya amana hiyo.
4. Ardhi ya kibinafsi inaweza kumilikiwa na watu binafsi au watu wengine walioruhusiwa kisheria kwa mujibu wa mifumo ya umiliki iliyofafanuliwa na sheria.
5. Ardhi ya jumuia imetengwa na inamilikiwa kwa niaba ya jamii au mawakala wao, kwa mujibu wa mifumo ya umiliki iliyofafanuliwa na sheria.
6. Haki za kumiliki mali kisheria italindwa na zinaweza kugawanywa bila ubaguzi wa kijinsia, ila tu kwa masharti yaliyomo kwenye mfumo wa umiliki wa ardhi.
7. Ardhi yoyote inayomilikiwa inategemea uwezo wa kimsingi wa taifa wa kuitwaa au kuitolea masharti kwa maslahi au manufaa ya umma.
8. Kutaundwa Tume ya Ardhi itakayotekeleza majukumu yafuatayo:
   (a) Kumiliki ardhi ya umma.
   (b) Kufanya marekebisho ya mara kwa mara ya sera na sheria za ardhi.
   (c) Kuandaa kanuni za matumizi na usimamizi wa ardhi.
   (d) Kutekeleza majukumu ya kiutawala kuhusu ardhi isiyomilikiwa.
9. Bunge litatunga sheria katika kipindi cha miaka miwili ya awamu yake ya kwanza chini ya katiba hii na kutoa utaratatibu ufuatao-
   (a) Kujumuisha kanuni zilizotajwa hapo juu.
   (b) Kuunda mbinu za kutatua mizozo ya ardhi chini ya umiliki tofauti tofauti wa ardhi.
   (c) Kuunda mfumo wa haraka kugawanya ardhi na usio wa gharama ya juu (kupokezana umiliki wa ardhi.

10. Haki za kumiliki mali kisheria utalindwa na zinaweza kugawanywa bila ubaguzi wa kijinsia, ila tu kwa masharti yaliyomo kwenye mfumo wa umiliki wa ardhi.
11. Ardhi yoyote inayomilikiwa inategemea uwezo wa kimsingi wa taifa wa kuitwaa au kuitolea masharti kwa maslahi au manufaa ya umma.
    (a) Kumiliki mali ya umma.
    (b) Kufanya marekebisho ya mara kwa mara kwa mara na sheria za ardhi.
    (c) Kuandaa makanuni za matumizi na usimamizi wa ardhi.
    (d) Kutekeleza majukumu ya kiutawala kuhusu ardhi isiyomilikiwa.

12. Bunge litatunga sheria katika kipindi cha miaka miwili ya awamu yake ya kwanza chini ya katiba hii na kutoa utaratibu ufuatao:

a) Kujumuisha kanuni zilizotajwa hapo juu.
b) Kuunda mbinu za kutatua mizozo ya ardhi chini ya umiliki tofauti tofauti wa ardhi.
c) Kuunda mfumo wa wa haraka kugawanya ardhi na usio wa gharama ya juu (kupokezana umiliki wa ardhi).
d) Ugawaji sawa wa ardhi pamoja na kutatua matatizo ya wasio na ardhi, na kuongezeka maradufu kwa utafutaji wa makazi katika maeneo ya mijini.
e) Kuchunguza na kutatua madai ya kihistoria hasa katika mikoa ya Pwani, Bonde la Ufa, na Kaskazini Mashariki miongoni mwa maeneo mengine.
f) Kuanzisha utozaji wa kodi kwenye ardhi isiyotumika na ile isiyotumika kikamilifu.
g) Kuratibu na kurahisisha sheria za ardhi.

- Serikali lazima iwalinde wanyama pori, maliasili za kimaumbile na za kibaiolojia, uchumi Kenya, kuhifadhi misitu, kutenda, kuhimiza na panapowezekana haya yote ya uwezo.
- Kupunguza uharibifu na urejeleaji, uhifadhi wa maji, matumizi na maendeleo ya nishati ya teknoknolojia ya kufaa na matumizi ya vianzo vya nishati zinazoweza kurudishiwa upya.
- Serikali lazima iunde na kuhakikisha utendakazi bora wa utaratibu wa kutathmini taathira za mazingira na ukaguzi wa mazingira, na kufuatilia; na kuhakikisha kwamba vigezo vya kimazingira vinaimarishwa nchini Kenya kwa ajili ya kutoa uwezo wa kwenda

KANUNI ZA MAENDELEO ENDELEVU

Maendeleo yanatimiza mahitaji ya kizazi kilichopo wala si kufanya maelewano na uwezo wa vizazi vya baadaye kupata mahitaji yao.
Usawa katika vizazi
Usawa kati ya vizazi
Kanuni za tahadhari
Kanuni za kuzuia
Malipo bandia (hewa/ufisadi
Ushiriki wa umma

sambamba na vigezo endelevu vya kimataifa.

- Madini yote na rasilimali ya maji ni mali ya watu wa Kenya. Tume ya Kitaifa ya Ardhi inashikilia maliasili hizo ambazo wamewekezewa kirasmi ama wanazozisimamia kama amana ya wananchi wa Kenya, lakini kiasi cha mapato lazima kipewe watu wanaomiliki ardhi hiyo.

- Kwa kadri inavyowezekana, utawala wa mali asili lazima uwashirikishe jamii bila kukosa kuona haja ya maliasili kulindwa na kustawishwa kwa manufaa ya taifa kwa jumla
- Sheria lazima iruhusu bunge kwa ambavyo hili linalinda haki za raia, lishauriwe kuhusu uamuzi muhimu unaoshughulikia matumizi ya ardhi na rasilimali ya taifa.

b.) Uchumi

Katiba haiwezi kutoa masharti ya maagizo marefu kuhusu usimamizi wa kiuchumi wa nchi.
Kanuni muhimu za kijumla tu ndizo zinazoweza kuhusishwa katika:

- Kuhimiza ujuzi na ufahamu ufaao wa kisayansi na kiteknolojia kupitia njia ya elimu na mbinu nyinginezo za maendeleo
- Kanuni za maendeleo yaliyosawazishwa nchini
- Ulinzi wa rasilimali ya uwezo wa kiakili
- Kulinda na kuendeleza ujuzi wa kiasili
- Kuhimiza uhusiano wa kibiashara barani Afrika
- Usaidizi katika sekta mbali mbali za kiuchumi zikiwepo sekta za kilimo na ufugaji wanyama

7. Fedha za Umma

Ni dhahiri kwamba uchangishaji na matumizi ya fedha za umma ni shughuli zinazohitaji kanuni zilizotungwa kwa uzingatifu, hasa katika nchi kama ya Kenya ambamo wananchi wengi ni maskinin hawangeweza hata kidogo kupoteza fedha zao ama za umma. La muhimu zaidi ni kwamba pamekuwa na maoni ya ukosoaji wa matumizi ya fedha za umma.

Sheria ya Marekebisho (Sehemu 17 (d) inaeleza kwamba moja wapo ya majukumu ya Tume ni kuhakikisha kuwa Wakenya: …(viii) wanachunguza na kurekebisha usimamizi na matumizi ya fedha za umma na kupendekeza uboreshaji wake; …

Wakenya waliiambia Tume kwamba:

- Hatua zitachukuliwa kuhakikisha kwamba kila anayehitajika kulipa ushuru analipa; kwa mfano, ikiwa ulipaji ushuru umeondolewa, jambo hilo lingetangazwa hadharani, Katiba iweke kanuni za usawa na uadilifu na utoaji ushuru
- Bunge na wananchi washirikishwe zaidi katika matayarisho na kuidhinisha bajeti
- Udhibiti na utaratibu wa bajeti lazima uwekwe kikwazo kwa njia mbalimbali
- Uhuru na uwezo wa Mhasibu-Mkuu lazima uongezwe
- Lazima kuwe na udhibiti bora wa mapato ya nchi yaliyo nje ya bajeti
- Lazima utaratibu wote huo uwe wazi
- Kazi mbili: kudhibiti bajeti na kuhasibu lazima zifanywe ni vyombo tofauti
- Katiba yabidi kuanzilisha afisi ya Gavana wa Benki Kuu na ipewe usalama wa awamu ya kazi na uhuru wa utenda kazi.

Katiba ya sasa ina kanuni za kawaida kuanzisha mifuko maalum ya akiba ambamo pesa za umma zitawekwa ili kuwezesha uwekaji wa taratibu za kupitisha sheria zinazoongeza kodi na matumizi ya pesa, na kuwezesha uundaji wa cheo huria cha Mhasibu Mkuu ili ahasibu hesabu za fedha za umma. Kuna njia tofauti ambamo kanuni hizi zinaweza kuimarishwa ili kutekeleza udhibiti mwema wa masuala ya fedha. Pili ni kulitilia Bunge vizuizi vikali hasa katika uundaji wa sheria za kuhusu matumizi ya fedha za umma au kupendekeza mabadiliko katika makadirio ya pesa. Tatu utaratibu huu wote utaeleweka kwa umma. Ukweli ni kuwa, kwa wakati wa sasa, suala zima la utaratibu wa makadirio ya pesa limo katika mikono ya mamlaka ya nchi. Bunge wala wananchi hawaelewi taratibu za makadirio wala kinachopangiwa. Hawapewi habari za kutosha wala muda wa kutosha wa kutathmini mipango ya mamlaka ya nchi.

Mswada wa Katiba una kanuni muhimu zifuatazo:

- Kauli ya kwamba taratibu za kimakadirio ni lazima ziwe za wazi na pia ni lazima uhusishe ushiriki wa wabunge na raia kadri iwezekanavyo; ni lazima wadumishe uwajibikaji na usimamizi bora wa fedha kwa ajili ya kuzingatia uchumi, madeni na sekta ya umma.
- Utaratibu wa kuandaa makadirio ya mwaka ni lazima uwe wa wazi na uwezeshe ushiriki wa wengi hasa ushiriki wa Bunge. Ili kuyawezesha haya:
    - Maandishi kuhusu makadirio yanayowasilishwa Bunge ni yawe yale yatawawezesha washiriki kuelewa na kuweza kuchangia katika mijadala kuhusu bajeti.
    - Bajeti ya mwaka maalum isiwasilishwe peke yake bali ionyeshe ni wapi ambako mapato yatatoka na pia ambako matumizi yatahitajika

katika muktadha wa mwaka uliotangulia, na pia mipango ya mwaka utakaofuatia.
    - Mawasilisho ya bajeti ni lazima yatayarishwe na kuwasilishwa BungeNI katika tarehe itakayowekwa na sheria ambayo itawapatia muda wa kutosha wa kuwa na mijadala ya manufaa, na ambayo ni lazima iwepo kabla ya mwanzo wa mwaka unaofuatia.
    - Ni lazima Bunge liunde kamati ya kushughulikia makadirio na kuipatia vifaa vyovyote muhuimu vinavyohitajika.
    - Kutakuwa na udhibiti mkubwa wa matumizi ya fedha.
    - Kiasi cha fedha zinazotolewa mwanzo wa mwaka wa fedha lakini kabla ya kukubalika kwa bajeti kipunguzwe (hivi sasa ni asilimia hamsini – 50% ya bajeti iliyopangwa)
    - Kutakuwa na udhibiti mkubwa wa hali za matumizi ya fedha za dharura
- Kutakuwa na masharti makali ya kuhusu uwezo wa serikali kukopa pesa – udhibiti utakaofanywa na bunge na uwazi wa utaratibu huu utaongezeka
- Mswada wa Katiba unaeleza kwa wazi kuhusu umuhimu wa aina zote za kupandisha ushuru kupata idhini ya bunge.
- Inaagiza kuwa kauli ya kupuuza ulazima wa kutoa ushuru itolewe na bunge.
- Kutakuwa na afisi ya Msimamizi wa Bajeti – ambaye atakuwa na majukumu ya kuidhinisha matumizi ya mifuko ya serikali ili kuhakikisha kuwa yanazingatia sheria na yanalenga matumizi yaliyopangiwa – tofauti na Mhasibu Mkuu ambaye hivi sasa ni afisi yake ambayo inayatekeleza majukumu haya japo haina uwezo wa kuyatekeleza vizuri.
- Kuna kanuni za wazi kuhusu muda unaowekwa wa kuwasilisha Ripoti za Mhasibu Mkuu.
- Uhuru wa afisi umeongezeka.
- Mhasibu Mkuu anaripoti moja kwa moja kwa bunge
- Banki kuu imetambuliwa katika Katiba na Gavana wake amepewa usalama/ulinzi wa muda anapohudumu (ili kumlinda kutokana na uwezekano wa serikali kumlazimisha kuongeza pesa katika matumizi au kwa mfano kuruhusu mfuko wa Jumla kuwa na deni katika akaunti ya benki (Overdraft).

8. Kenya na Ulimwengu

Kenya ni raia wa jumuia ya kimataifa. Ni mshiriki wa Umoja wa Mataifa, wa Umoja wa Afrika na Jumuia ya Afrika Mashariki. Imekubali kutii mikataba mingi ya kimataifa ikiwemo haki za binadamu na mazingira. Labda habari hizi zinaonekana kuwa za ajabuajabu kwa wengi. Zinamaanisha nini kwa mkenya wa kawaida? Zina manufaa yoyote kwa maisha yake ya kila siku? Je zinahusisha serikali - na kwa hivyo raia mlipa ushuru – katika matumizi ya pesa? Je Kenya ni raia mwema wa jumuia ya kimataifa? Haya yote ni maswali ambayo yanahitaji kuwa na majawabu ya moja kwa moja – lakini hayana.

Mswada wa Katiba utayaweka haya yote katika hali ya kueleweka na umma. Lakini, mwanzo, ni muhimu kueleza machache kuhusu utendakazi wa sheria ya kimatiafa. Mikataba ya kimataifa inaweza kuwekwa kufuatia makubaliano baina ya mataifa mawili au baina ya mataifa kadha. Mkataba unaweza kufadhiliwa na shirika la kimataifa (kama vile Umoja Wa Mataifa). Mkataba unaweza kuwekwa na serikali lakini ni lazima 'uidhinishwe' nchini; Mambo ya kuzingatiwa katika uidhinishaji yatategemea ama sheria za nchi au kanuni za mkataba wenyewe. Nchini Kenya, mikataba huidhinishwa kwa kuwekewa sahihi na Raisi. Sheria ya kimataifa inaweza pia kutokana na mazoea ya mataifa (mazoea yanayoitwa Sheria Ya Mila Ya Kimataifa – (Customary International Law) au inaweza pia kuwekwa na mahakama ya kimataifa ambayo hufafanua mikataba, kama vile mahakama ya haki ya kimataifa iliyo Hague (ya Uholanzi). Sheria ya Mila Ya Kimataifa ni kipengele mojawapo cha sheria ya Kenya – japo Katiba haiyasemi haya. Katika sheria ya Kenya, mkataba hauwi sheria ya bunge la Kenya ipitishwe ili kushirikisha sheria mpya za kimataifa katika sheria za nchi. Haya yanaweza kuchukua miaka mingi kabla ya kutimizwa. Kwa hakika yakwamba Kenya imekubali jukumu la kimataifa haimaanishi ya kwamba inalazimu haki ya kuwepo nafasi ya raia wa Kenya hata pale ambapo mkataba ulilenga kuwafaidi Wakenya.

Mapendekezo ya Tume yataufanya mfumo uwe wazi zaidi, na kuuweka kwa kiasi kikubwa chini ya udhibiti wa bunge linalowakilisha wananchi

- Katiba inasema kwamba sheria ya desturi ya kimataifa (isipokuwa ikiwa inakinzana na katiba au sheria iliyopitisha na Bunge) na mikataba inayoihusisha Kenya ni sehemu ya sheria za Kenya.
- Serikali inafanya mapatano na kuweka sahihi mikataba – kama sehemu ya majukumu ya madaraka ya serikali
- Kabla mkataba haujaidhinishwa kabisa. Ni lazima uidhinishwe na Bunge (na angalau nusu ya Wabunge wote na ikiwa mkataba unahitaji kubadilishwa kwa Katiba lazima uwe na asilimia sawa na inayohitajika kwa badiliko la kiKatiba). Bunge sharti ipewe muda wa kutosha wa kujadili mkataba huo.
- Mikataba mingine huenda ikaanza kutekelezwa nchini Kenya bila sheria – hii inategemea kanuni za mkataba wenyewe na inaruhuriwa na mswada.
- Mikataba iliyopo ambayo haijatekelezwa nchini kupitia Sheria ya Bunge sharti ianze kutekelezwa kwa muda wa mwaka mmoja baada ya kuidhinishwa kwa Katiba mpya.

Kuna jambo jingine linalopaswa kushughulikiwa na Katiba: uwezekano wa Kenya kutangaza vita au kuamuru majeshi yake (kwa mfano, jeshi la kuimarisha – amani), ijapokuwa Katiba mpya hazisemi chochote kulihusu.

- Muswada wa Katiba umeagiza kwamba Tangazo la Vita hutolewa na Rais, baada ya kushauriana na Baraza la Majeshi la Taifa, lakini

panahitajika uinidhishaji wa awali wa angaa thuluthi mbili ya Bunge kwa muda wa majuma mawili

- Majukumu mengine ya Majeshi ya Taifa nje ya mipaka ya nchi yahitaji kuidhinishwa na Bunge kwa wingi wa kura kamili.

SURA YA TATU

MSWADA WA KATIBA
UTARATIBU NA ASASI ZA SERIKALI

Uamuzi bora katika uundaji wa Katiba hugetemea muundo wa mfumo wa serikali. Mfumo wa serikali huamua umbo la mamlaka ya taifa na taratibu za matumizi ya mamlaka yenyewe. Huamua yule anayeweza kupewa mamlaka na rasilimali za taifa. Pia inarekebisha uhusiano wa kitaifa kati yao, vyombo vyake na wananchi. Muundo wa serikali huathiri siasa, muungano wa vyama, jinsi ukabila unavyothaminiwa ama unavyoendeshwa, jinsi serikali ilivyo imara, na namna ambavyo watu wanajishirikisha kwayo. Hutegemea maoni ya wananchi kama pengine wanahisi wamehusishwa ama wametengwa katika shughuli za serikali.

Katika mataifa mengi, siasa zimehusisha pakubwa umiliki wa vyombo vya madaraka ya taifa, kutosheleza ajenda za kibinafsi na za kikabila. Lakini mfumo wa serikali unaweza kuundwa ili kupata na kuboresha thamani ya nchi, kutangaza demokrasia, kuimarisha umoja wa nchi, kuhakikisha ufanisi wa usimamizi bora, kufanikisha maendeleo ya kiuchumi na kuimarisha uwajibikaji wa serikali na viongozi wake. Hili ndilo pigo lililoloukumba utaratibu wa marekebisho. Hapa tunayachunguza maagizo ya Bunge na mfumo wa uchaguzi, muungano wa mamlaka ya nchi na Mahakama: Mikondo mitatu ya kawaida ya serikali. Sheria ya marekebisho ilielekeza kwamba utaratibu huo uzingatie ugawaji wa mamlaka na uundaji wa vipimo na visawazishi katika vyombo huria vya serikali.

Sura hii pia inahusisha mapendekezo ya Tume ya Marekebisho ya Katiba ya Kenya **(CKRC)** yanayohusu upunguzaji na usambazaji wa madaraka – sura nyingine iliyoagizwa na sheria ya marekebisho. Pia kuna majadiliano kuhusu vyama vya kisiasa na jinsi ambavyo vinavyoweza kuendeshwa ili kuboresha utaratibu wa utendakazi wa serikali.

1. Bunge Na Wabunge

Hivi sasa bunge lina baraza la wawakilishi na Rais. Kirasmi si kwamba Rais ni sehemu ya bunge bali ni mwanachama wa eneobunge la baraza la wawakilishi. Wakati huu nchini Kenya, baraza la taifa la wawakilishi lina chemba moja maalum: Kuna wanachama 222 ambao 210 kati yao wamechaguliwa moja kwa moja kutoka kwenye maeneobunge, na 12 wamechaguliwa na vyama vya kisiasa kulingana na uchaguzi wa viti vyao, kuwakilisha “maslahi maalum” na kufikia kiwango fulani cha usawa wa kijinsia.

Spika na Mkuu wa Sheria ni wanachama kwa mujibu wa ofisi zao. Watu walipotoa maoni yao kwa Tume walipinga sana jinsi bunge linavyoendesha

shughuli zao na hali halisi ya muundo wake. Kwa jumla kukata tamaa huko kulijitokeza kuambatana na maoni yafuatayo:

- Wabunge wawe wa kudumu
- Kuanzisha uadilifu na maadili ya kitaaluma mema kwa wagombeaji
- Baadhi yao walisema wazidishiwe viwango bora vya kimasomo hasa lazima mbunge awe na shahada
- Tume huru iamue mishahara ya wabunge na vikao vya bunge vionyeshwe kwenye vyombo vya habari (ili watu wajue vyema jinsi wabunge wao wanavyotekeleza majukumu yao).
- Kuzidisha akidi za wawakilishi wa baraza la bunge
- Wengi walihitaji kupewa uwezo wa kutupilia mbali agizo la wabunge wasiotekeleza majukumu yao.

Kwa upande mwingine, imani kuu kwa lengo la wawakilishi wateule iliyotolewa ilidhihirisha wazi kupitia mapendekezo, ilionyesha kwamba mamlaka ya bunge ni muhimu kuboreshwa:

- Ni muhimu kudhibiti matumizi ya fedha za taifa: hali kadhalika pawe na kamati ya makadirio ambayo itachunguza mapendekezo ya makadirio ya mapato na matumizi; mfumo bora wa kamati;
- Bunge lijadili na kuidhinisha uteuzi maalum unaofanywa na Rais
- Bunge liwe na uwezo wa kuvunja serikali kupitia kura ya kutokuwa na imani.
- Bunge liweze kudhibiti kalenda yake

Kuhusu Muundo wa Bunge:

- Palikuwa na haja ya chemba ya pili, ijapokuwa ulitokea mchanganyiko wa maoni kuhusu majukumu na umbile lake.
- Chemba cha pili kiliungwa mkono japo maonikuhusu dhima na muundo wake yalitofautiana.
- Aidha: Dhana ya wabunge wateule haikuungwa mkono, na waliounga mkono dhana hiyo walidai kwamba wabunge hao wawakilishe maslahi ya vikundi maalum (kama vile wanawake, walemavu na wakulima).
- Vikundi vingi vya kina mama – na pia wanaume - walidai kwamba pawe na asilimia maalum ya wanachama wanawake.

Wengi wao walisema kuwa Rais asiwe na uwezo wa kuvunja bunge – suala ambalo halilengi mamlaka ya bunge pekee bali hata uwezo wa serikali ili kuendesha mfumo wa kisiasa.

Tume imetoa mapendekezo yake na inaamini kwamba itatimiza malalamiko na shauku ya umma, kwanza kabisa katika uwajibikaji:

- Viwango vya juu vya elimu na uadilifu wa kinidhamu vitahitajika kwa wagombeaji.
- Habari kuhusu wagombeaji inahitaji iwafikie wananchi.
- Masharti kwa wabunge yatakuwa magumu zaidi hasa kwa wale wasio na nidhamu – ikiwa ni katika uvunjaji wa sheria ama kanuni za uongozi ambazo lazima zianzishwe.
- Wabunge watapoteza viti vyao watakapokosa vikao fulani vya bunge.

- Kutakuwa na utaratibu fulani wa kuwaondoa kazini wabunge ambao hawakutekeleza wadhifa wao kikamilifu.
- Mbunge atakayegura chama kwa tikiti ya chama kilichomteua lazima ajiuzulu
- Bunge lazima liwe na vikao vya idadi fulani kwa mwaka.

Kuna uwiano kati ya mfumo wa serikali na wadhifa wa wabunge. Mswada wa katiba unahusisha mgawanyiko kati ya mawaziri na bunge. Hii ni kwa sababu ya kuwafanya wabunge kujihusisha zaidi na wajibu wao kama vile; mawaziri hawahitajiki kuwa wabunge kabisa.

Tatu, kuna kiwango cha idadi ya mawaziri. Hii ni kati ya kanuni zao kwamba lazima wabunge washike majukumu yao kikamilifu, na akubali kuwa hiyo ni kazi ya kudumu na si njia tu ya kuwa Waziri.
Kuna mapendekezo fulani yaliyoundwa ili kuzidisha uwezo na taathira za bunge:

- Wabunge watapewa mafunzo
- Uwezo wa utafiti wa bunge lazima uimarishwe
- Lazima pawe na usaidizi wa usimamizi bora.
- Bunge lazima liunde kamati fulani (sehemu ambayo kazi ya bunge hufanyika zaidi: mbali na majaribu ya "utekelezaji" na wakati ambapo wabunge wa vyama tofauti watafanya kazi pamoja kwa maslahi ya nchi).
- Bunge lazima likubali uteuzi wa maafisa maalum kama Majaji, na Mhasibu Mkuu.
- Bunge litakuwa na jukumu kubwa la kutayarisha makadirio ya mapato na matumizi ya nchi.
- Bunge litakuwa na jukumu katika kuunda mapatano.

Na inapendekezwa kwamba pawe na jukumu la wananchi:

- Kutakuwa na haki ya kulalamikia bunge;
- Vikundi ama raia wana haki ya kuhudhuria kamati za Bunge, wakijadili na kuchunguza masuala fulani;
- Sehemu moja ya kamati ya Bunge itaboresha na kutoa uwezo wa kuhusika kwa wananchi kupitia kwenye mambo kama mikutano ya umma jijini Nairobi na maeneo mengine nchini.

a.) Ukumbi mmoja wa Bunge ama Kumbi Mbili?

Katika suala la chemba ya pili (Katika Katiba ya 1963, hii ilikuwa seneti), Tume ilijadili kwa mapana na marefu. Hatimaye, wakapendekeza kwamba ziwe kumbi mbili. Shabaha kuu ni kukinga utaratibu wa kuvunja serikali, lakini ina malengo mengine pia. Tume inafahamu kuwa si uamuzi rahisi -na ina imani kuwa akiba ya taifa na ukuaji wa uwekezaji na uzalishaji, kama matokeo ya utawala bora utakuwa mkubwa zaidi ya gharama ya chemba ya pili. Kwa kutambulika lengo kuu la Bunge jipya, katiba inapendekeza kwamba liitwe Baraza la Kitaifa. Majukumu yake ni:

- Kuwa mbinu ya kukuza uhusiano baina yatawala za wilaya na serikali kuu.
- Kupima na kusawazisha shughuli za ukumbi mdogo (wa chini).
- Kuwakilisha maslahi ya mikoa, wilaya na walio wachache.
- Kuhusika katika utaratibu wa kisheria .
- Kumjaribu Rais katika mashtaka ya utenguzi ambayo yanawasilishwa na Ukumbi Mdogo.

Itakuwa na takriban wanachama mia moja (100)
- Mmoja aliyechaguliwa na wakazi wake kutoka kila wilaya.
- Wengine thelathini (30) wa kutoka mikoani watawakilisha maslahi ya wanawake.

Mswada wa Kisheria unaweza kuanzishwa katika kumbi zote. Wasipoelewana kuhusu mswada huo, lazima pafanywe mikutano ya kamati za kumbi zote mbili zitakazojadiliana hadi kuafikiana. Wasipoafikiana basi Bunge litaamua – ila tu kwa usawa wa marekebisho ya katiba ikiwa masharti fulani yataelekezwa katika kuathiri wilaya.

2. Uwakilishi wa Wananchi: Utaratibu wa uchaguzi

Maoni mengi yaliyofikishwa kwa Tume yalielekezwa katika kutotosheka kwa utaratibu wa sasa wa uchaguzi. Watu walieleza maoni yao kuhusu uchaguzi wa bunge na kwa Rais:
- Walieleza wazi kwamba Rais achaguliwe moja wa moja
- Na Rais lazima apate zaidi ya asilimia hamsini (50%) ya wingi wa kura.
- Lazima pawe na uchaguzi wa uamuzi - mkata kama hakuna yeyote atakayepata ushindi katika kura ya awali.
- Baadhi ya maoni yaligawanyika huku wengine wakiuliza kama Rais atahitajika kuwa na asilimia ishirini na tano (25%) kwa mikoa mitano kwa kuungwa mkono: Baadhi waliliunga hili mkono, na wengine wakapendekeza asilimia ishirini (20%) katika kila mikoa minne, huku wengine wakidai kwamba zaidi ya asilimia hamsini (50%) ya umma ya kuunga mkono ilitosha.
- Rais asiwe mamlakani kwa awamu ya zaidi ya vipindi viwili, kila awamu ikichukua miaka mitano.

Kuhusu Uchaguzi katika Maeneobunge walisema::
- Maeneobunge hayana usawa wa ukubwa.
- Ni vigumu kusajiliwa kama mpigakura.
- Ni vigumu kuteuliwa kana mgombeaji.
- Kura ziliibiwa
- Tume ya uchaguzi haina uhuru
- Wanataka pawe na uwezekano wa wagombeaji huria.
- Wana lazima ya uwakilishi wa wanawake, walemavu, vijana na vyama vya wafanyikazi

- Mapendekezo mengi yenye misingi ya zaidi ya uwakilishi, hasa uanataaluma n.k. (watu amao huenda wasishiriki siasa).
- Wengi walisema kwamba kunahitajika utaratibu unaofaa wa uwakilishi.
- Usajili wa wapiga kura unahitaji kuendelea mfululizo.
- Baadhi ya vijana waliomba umri wa kupiga kura upunguzwe.
- Kura zihesabiwe katika vituo vya upigaji kura.
- Masanduku ya kura lazima yawe angavu.

Suala kamili linahusu utaratibu wa uchaguzi: jinsi ambavyo kura zinavyochangia katika viti vya bunge. Malalamiko kuhusu mfumo uliopo (unaofahamika kama "Mfano waliyefika Mbele**"-(FPTP)** ni kwamba idadi ya wabunge ambayo chama kitapata haitawakilisha hali ya kuungwaji mkoni kote nchini – ni wazi na kawaida chama tawala kinapata chini ya nusu ya kura zote. Unaweza kusema kwamba zaidi ya nusu ya wananchi **hawakutaka** watawale! Mfumo bora kabisa wa uwakilishi wenye uwiano ungekuwa ule wa taifa lote kuwa eneobunge: kila chama kinaorodhesha wagombeaji wake, na mpiga kura anaweza kupigia kura chama kimoja pekee. Mfumo huu unatekelezwa nchini Namibia na Afrika Kusini, na pia Israel. Matokeo yake ni kwamba hakuna mbunge atakayechaguliwa na eneobunge maalum. Ni wazi kuwa Wakenya wengi walitarajia kubaki na wabunge wa maeneobunge, ijapokuwa kwa njia bora za kuchunguza uwajibikaji wao – jambo ambalo limejadiliwa kwenye sura iliyotangulia.

Ili kuyapatanisha maoni haya, mswada wa katiba umeiga **Mfumo wa Uwiano Mseto wa Wanachama** (Mixed Member Proportional) katika uchaguzi wa Bunge na mabaraza ya wilaya. Wanachama 210 watachaguliwa katika maeneobunge ya uanachama mmoja kwa mgombea atakayekuwa na kura nyingi kwa wakati ule. Ili kupata Bunge lenye uwiano bora, wanachama waliochaguliwa bila kupingwa wanaoanishwa na wanachama waliotolewa kwenya orodha ya wagombeaji wa vyama vya kisiasa wanaogombania (idadi ya wanachama kama hao itakuwa tisini (90). Lengo la wanachama hawa wa ziada ni kuhakikisha kwamba chama kinapata idadi ya viti kwa uwiano wa kura zote nchini. Wapiga kura watapiga kura mbili, moja ya mgombeaji na nyingine ya chama. Kama chama hakitapata idadi ya viti vya maeneobunge ikiwiana na kura yake ya kitaifa, kitapata wanachama zaidi kutoka kwenye orodha ya chama. Utaratibu huu unachanganya ubora wa eneobunge la uanachama mmoja, unaotoa mshikamano wa karibu kati ya mbunge na eneobunge lake, na uwiano wa jumla wa kataifa, ili kila chama kiwe na usawa wa uwakilishi. Kama maeneobunge ya ukubwa usiolingana yamebuniwa kwa sababu maalum, ama mipaka imeundwa kupendelea chama fulani maalum, hali hiyo ya uwiano kwa kiwango kikubwa itafutilia mbali hila katika kuweka mipaka ya maeneobunge (kuongeza mipaka ya uchaguzi).

Kuna manufaa mengi ya utaratibu huu wa uwiano mseto wa wanachama (MMP). Jamii ya walio wachache wana uwezekano wa kuwakilishwa hata kama hawakushinda kiti cha eneobunge (ikiwa tu, chama chao kimepata

asilimia tano (5%) ya kura ya taifa) – Katika uchaguzi wa mwisho huko Lesotho walipoendesha kwa mara ya kwanza utaratibu huu wa uwiano mseto wa wanachama (MMP), chama cha upinzani hakikushinda hata kiti kimoja cha eneobunge na wakapata karibu asilimia ishirini (20%) ya viti kufuatia kanuni za uwiano wa kura za kitaifa. Njia nyingine ambayo walio wachache wanaweza kuchaguliwa kwayo ni, wanachama wake kuwekwa katika orodha ya chama – wanawake na wanaume watachagua mmoja baada ya mwingine, na walemavu na walio wachache pia wataorodheshwa.Vyama vitapata fursa ya kukampeni hadi katika maeneo wasiyotarajia kupata kiti cha eneobunge. Kila kura watakayopata itakuwa ni akiba ya kipindi cha uwiano. Utaratibu huo wa uwiano mseto wa wanachama (MMP) uliungwa mkono na vyama vyote vikuu vya kisiasa na Tume Ya Uchaguzi. Rais atachaguliwa kupitia kura ya kitaifa na itabidi mshindi awe na kura nyingi bila tashwishi, pamoja na kuungwa mkono na wingi wa asilimia ishirini (20%) ya kura katika mikoa mingi. Kama hakuna wagombeaji watakaotimiza masharti haya, patakuwa na uchaguzi wa uamuzi mkata baina ya wale watakaoshikilia nafasi ya kwanza na ya pili kwa wingi wa kura: mgombezi atakayepata kura nyingi ndiye atakayekuwa Rais.

Utaratibu huu umeundwa ili kuhakikisha kwamba Rais anaungwa mkono na kuheshimiwa katika maeneo mengi nchini, na pia anafurahia, uungwaji mkono na Wakenya wengi. Kiwango hicho cha uungwaji mkono na uhalali, vingehitajika katika kutekeleza majukumu ya kirais na utangazaji wa umoja wa kitaifa na kuihami katiba. Uwezo wa tume ya Uchaguzi ni kuhakikisha uchaguzi huru na wa haki na kuimarisha kanuni za sheria. Utaratibu wa uchaguzi utakuwa wazi na haki ya wagombeaji haitatupiliwa mbali kupitia udhaifu wa usimamizi ama taratibu za kuchokesha katika usajili wa wagombeaji.

Tume ya mipaka ya maeneobunge itateuliwa mara kwa mara ili kubainisha wazi mipaka ya uchaguzi kwa uchaguzi katika ngazi za mashinani na za katikati. Itahusisha idadi ya watu na mambo ya kijiografia.

Uchaguzi huwa muhimu katika upokezanaji bora wa uwezo kutoka kwenye serikali moja na bunge kwa nyingine (jambo ambalo sheria ya marekebisho inalielekeza kwa Tume ya Marekebisho). Uchaguzi utakaofanywa chini ya mswada wa katibu unahitajika kufanywa siku 45 kabla ya kumalizika kwa awamu ya Bunge na Rais. Hii ina maanisha kwamba waliofaulu kama wagombeaji watafahamika mapema. Hatimaye, Bunge likifanya kikao litaanza kazi moja kwa moja. (sio kama wakati huu ambapo linakutana kidogo tu na kuahirishwa kwa muda mrefu).
Haki ya kila mpigakura lazima iwekwe wazi, ilindwe katika mswada wa katiba. Masharti kamili ni:

- Haki ya kupiga kura ya uchaguzi wa siri inahakikishwa.
- Umri wa kupiga kura ni miaka 18
- Usajili wa wapigakura uwe wa kuendelea.

- Usajili hutegemea kuwa na kitambulisho ama paspoti.
- Wafungwa walio rumande (ambao hawajahukumiwa) waweze kupiga kura.

Uadilifu wa utaratibu unaimarishwa kwa masharti yafuatayo**:-**

- Kuhesabiwa kwa kura lazima kufanyike katika vituo vya upigaji kura na iwe mbele ya watazamaji wa vyamani na wananchi.
- Masanduku ya kura lazima yawe angavu
- Watu walioshtakiwa baada ya kupatikana na kosa la uchaguzi kuondolewa kwenye ugombeaji kwa kipindi fulani.
- Uwezo uliopo wa Rais wa kuyaondoa masharti ya kumtoa mtu aliyepatikana na kosa la uchaguzi katika kujisajili kama mpigakura ama mgombeaji umetupiliwa mbali.

3. Vyama Vya Kisiasa

Vyama vyetu vya kisiasa vinatekeleza jukumu muhimu sana katika siasa na usimamizi, lakini haitasemwa kwamba wamechangia katika siasa ya amani na ya kutegemewa au kutangaza kiini cha demokrasia na uwajibikaji. Umuhimu wa vyama kwenye mfumo huo, aghalabu ulikiukwa na waundatume wa awali – hapakuwa na kutajwa kwa vyama kwenye kati ya 1963, na kwa uchache sana vimetajwa kwenye katiba iliyopo na hakuna masharti kabisa ya utendakazi wa vyama.

Mengi ya maoni yaliyopelekewa Tume yalizua shauku kuhusu vyama vya kisiasa na jinsi vinavyoendeshwa humu nchini Kenya, na yakapendekeza baadhi ya mabadiliko yafuatayo:

- Watu wengi walilalamika kwamba wingi wa vyama vya kisiasa umeleta mfarakano na wakapendekeza pawe na idadi fulani ya vyama; maoni yalipishana kidogo baadhi wakitaka vyama viwe viwili na wengine wakitaka vinne.
- Vyama viungwe mkono kote nchini; baadhi yao walisema kwamba kila chama kiwe na takribani wanachama 10,000 katika kila mkoa.
- Vyama visiundwe kwa kutegemea ukabila.
- Vyama visiwe ndiyo asasi ya pekee ya kuwateua wagombeaji.
- Wengi wao walisema kwamba vyama vidhaminiwe na rasilimali ya taifa; lakini chama kitapata udhamini huo wa rasilimali ya taifa ikiwa tu kinaungwa mkono; wengine walitaka vyama kusaidiwa kwa vikwazo fulani wakizingatia taratibu za kidemokrasia.
- Usajili wa vyama haufai kutekelezwa na ofisi ya Msajili wa Vyama (Registrar of Societies) bali kufanywa na Tume ya Uchaguzi (hasa katika hali ya kuhusu wale watakaoshiriki ugombezi). Wengine waliona kwamba vyama visisajiliwe hata ikiwa hivyo,watahitaji kufahamishwa.
- Vyama ambavyo havifanyi kazi vyema na vile ambavyo havikushinda katika viti vya bunge viondolewe kwenye orodha ya usajili.
- Kenya liwe taifa lisilo na chama chochote cha kisiasa.
- Katiba itoe hakikisho la kudumu kwa mfumo wa vyama vingi; kanuni hii isiweze kubadilishwa.

- Vyama vidhibitiwe ili kuhakikisha demokrasia na uwajibikaji.
- Vyama visiruhusiwe kuwa katika mabaraza ya wilaya.

Linaloonekana kuwa muhimu zaidi ni kulinda haki za kuanzisha vyama; lakini kuzingatia usimamizi wake wa ndani na wadhamini wake. Watahitajika kuchunga na kulinda kanuni za katiba na ili kuwezesha kiwango cha udhibiti huo, ni lazima pawepo na mfumo wa usajili wa vyama vinavyoazimia kugombea viti. Hatukubali pendekezo la kuchuja idadi ya vyama – ijapokuwa tunatambua kuwa watu wengi kupendekeza hivyo.

Kwa hakika, ni mataifa machache mno yaliyowahi kuwa na kanuni hii ya kikatiba (pengine iwe pana chama kimoja pekee). Nchi nyingine ambazo zina vyama vichache huwa navyo kwa sababu ya jinsi mfumo wao wa kisiasa unavyofanya kazi, si kwa sababu ya idadi ya vyama kwa mujibu wa sheria. Tuna imani kwamba vyama vichache vitaundwa wakati ambapo kutakuwa na uwezekano wa mgombeaji huria atakayesimama uchaguzini.

Mswada wa katiba unaeleza kwamba:

- Haki ya kuunda na kujiunga na vyama vya kisiasa imelindwa.
- Chama cha kisiasa kinaweza kuundwa na Tume ya Uchaguzi kupitia usajili wa muda na wa kudumu.
- Kwa jumla vyama vyote vina uhuru wa kuendesha shughuli zake, na serikali sharti iwe na msimamo wa usawa kwa vyama vyote vilivyosajiliwa. Lazima pawe na usawa wa kufikia vyombo vya habari vya kitaifa na vile vya kibinafsi
- Ili kusajiliwa kushiriki katika uchaguzi, chama cha kisiasa lazima kiwe na makbala wa kitaifa, kisiundwe kwa misingi ya kidini, lugha, kabila, rangi, jinsia, shirika na msingi wa kieneo lazima kiambatane na kanuni za demokrasia. Vyama lazima viheshimu Katiba na sheria, na haki za binadamu pamoja na usawa wa kijinsia.
- Vyama visijihusishe ama kuchochea ghasia au kutisha waungaji mkono wake ama washindani wake. Na visianzishe au kuwa na vikundi vyenye hadhi ya kijeshi ama mashirika kama hayo.
- Lazima viweke vyema hesabu. Vyama huria na vya kisiasa lazima wachapishe manifesto zao kabla ya uchaguzi.
- Vyama vya kisiasa vinaweza kuteua wagombeaji wa uchaguzi wa serikali za wilaya.

Sababu kubwa ya ufisadi katika vyama vya kisiasa inatokana na haja ya kuchangisha pesa za uchaguzi na wakati mwingine pia kwa gharama ya uendeshaji wa shughuli za chama. Aghalabu, vyama vinavyounga mkono watu wenye uwezo na nguvu vinaweza kuchangisha pesa kwa urahisi ili kufanya mabadiliko makubwa katika kampeni. Mashirika kama hayo hupewa mapendeleo fulani kama vile, kandarasi kama njia ya hisani. Nchini Kenya matatizo ya fedha za chama yanaongezwa na umaskini wa watu, hivi kwamba uanachama sio mahali kamili pa chama kuchangia fedha. Ili kuondoa

mapendeleo ya vyama baadhi ya mahitaji yatolewa na serikali waziwazi; kwa usawa na haki. Udhamini utakuwa halali wakati ambapo vyama vya kisiasa vitakapokubali kufuata masharti yanayobainisha uwazi, uwajibikaji na maadili mema. Udhamini huo wa taifa utakuwa kama mbinu ya kusimamia na kudhibiti. Kwa mfano, nchi nyingine huzuia malipo ya vyama vilivyoungwa mkono na watu wachache mno katika uchaguzi uliopita. Tume inapendekeza kwamba masharti mengine kama hayo ni muhimu ili kulinda kuongezeka kwa vyama ambavyo maslahi yake kuu ni fedha. Kwa upande mwingine, vyama vipya au vya walio wachache vinakosa kunufaika kwa njia hiyo, na uhiari wa kisiasa kwa umma huwekewa vikwazo, na maoni mapya yanapata ugumu wa kusambazwa.

Mswada wa Katiba:

- Umeagiza kuwe na udhamini wa Serikali – kufuatana na muundo wa kuzingatia uungwaji mkono wa chama katika uchaguzi uliotangulia (vyama vipya vya kisiasa vipewe haki ya malipo kuzingatia siku zilizopita na jinsi ambavyo vyama vilivyofaulu).

Udhamini huo utakuwa wa:

- Gharama ya uchaguzi
- Elimu ya uraia kuhusu demokrasia na utaratibu wa uchaguzi
- Pamoja na kuwepo kwa fedha zisizozidi asilimia kumi (10%) ya gharama hizi, zitakazotolewa ili kuendesha shughuli na gharama ya vyama.

Tume inapendekeza pia katika mswada wa katiba:

- Vyombo vya mashirika ya nje vizuiliwe kutoa misaada au rasilimali kwa vyama. Mchango wa watu binafsi uwekewe mipaka fulani ili ipangwe na Tume ya Uchaguzi.
- Tume ya Uchaguzi lazima iwe na majukumu yanayodhihirisha demokrasia na inayosimamia vyama vya kisiasa.
- Tume ya Uchaguzi iweke wazi kiwango cha pesa ambazo chama ama mgombeaji anaweza kutumia wakati wa kampeni za uchaguzi.

4. Rais, Waziri Mkuu na Mawaziri:

Sasa tutazame yale ambayo hufikiriwa kuwa kama "Serikali"; jambo lenye umuhimu usiohitaji kuelezewa. Sheria ya Marekebisho haiagizi Tume juu ya utaratibu maalum wa kufuatiwa. Inaelezea pia kuhusu uamuzi wa wengi na kufafanua umuhimu wa kuhusika kwa watu.

Ujumbe mkuu uliofikishwa kwa Tume kutoka kwa wananchi ukiwa wazi na safi – ni kwamba katiba ya sasa inampa Rais uwezo mkubwa kupindukia. Maoni ya ziada yalieleza kwamba:

- Wengi walidai kuwa walipendelea serikali ya "mseto".
- Wengi walipendelea mfumo wa Bunge zaidi ya mingine yote (huu ndio uliokuwa mfumo wakati wa uhuru).
- Baadhi yao walitarajia mfumo uliopo uendelee lakini uwezo wa Rais ukiwa mdogo, na mabadiliko mengine.

- Watu wengine – pamoja na vyama vyama vya kisiasa walitaka mfumo ulio na Rais na Waziri Mkuu, wakiwa na mgawo wa uwezo na mamlaka baina yao.

Kulikuwa na maoni mbali mbali kuhusu mifumo inayowezekana. Mfumo ambao una Rais na Waziri Mkuu uliungwa mkono na vyama vingi vya kisiasa. Hii ni njia ya kugawanya mamlaka. Kwa upande mwingine, Rais akipewa tu mamlaka ya ustahiwa, Waziri Mkuu anaweza kuwa na uwezo kama ule ambao Rais wa Kenya amekuwa nao kwa miaka mingi. Rais ambaye ni Mstahiwa tu, atahitajika kushauriwa kila wakati na Waziri Mkuu (kama utawala wa Kifalme katika Katiba ya Kifalme nchini Uingereza). Tume inapendekeza utaratibu ambamo Rais na Waziri Mkuu wana uwezo 'maalum'. Mfumo huu unafahamika katika nchi za bara Ulaya, na koloni zao za kitambo, na pia umeigwa na nchi ya Sri Lanka.

Kuna matatizo katika utaratibu aina hii na yamejitokeza hasa katika nchi za Ufaransa na Sri Lanka. Aghalabu, matatizo hayo hutokea kwa sababu Rais na Waziri Mkuu ni wa vyama tofauti vya kisiasa. Wanaweza pia kutofautiana kibinafsi. Rais akiwa na uwezo kamili, hasa ikiwa ana majukumu ya kuwa kama kipimo cha serikali na Bunge, hasa pale ambapo serikali na Bunge vitaonyesha dalili yo yote ya kukiuka mamlaka yake, mgogoro unaweza kutokea. Ili kujikinga na mgogoro huu, Katiba ieleze wazi majukumu kamili ya Rais na Waziri Mkuu ni yapi na jinsi ya kusuluhisha mzozo, ama kutofautiana.



Hivyo basi, kama kuna hatari ya migongano, kwa nini Tume inapendekeza utaratibu huu? Shabaha kamili ni kusambaza mamlaka – hata kati ya vyama. Maoni mengi yaliyotolewa kwa Tume yalionyesha kupendelea serikali ya "mseto". Hii ina maana ya uundaji wa Serikali ya vyama vingi. Kuna mfano wa serikali kama hiyo katika Katiba ya Fiji – chama chochote kinachoshinda kwa asilimia zaidi ya kumi (10%) kinaweza kuwa na Waziri au Mawaziri katika Serikali. Hili linaweza kuonekana kama wazo zuri sana: lakini lina matatizo yake. Kwanza kabisa, serikali inaweza kuundwa na mawaziri walio na maoni tofauti sana kuhusu sera – na hatimaye huenda isifaulu. Hatari zaidi ni kuwa, mawaziri hao hawako pale kwa sababu wameamua kufanya kazi pamoja, lakini kwa sababu ni amri ya Katiba! Mfano mbaya wa hatari hizi

katika nchi ya Fiji ulitokea mwaka wa 2000 wakati Waziri Mkuu aliposema kwamba chama cha pili kikuu itakuwa bora kikiwa upande wa upinzani, na kiongozi wa chama hicho akasema kuwa atajiunga na serikali ili awe mpizani katika serikali. Bila shaka si mfano mwema serikali cha Muungano! Lakini kuna ubora wa kuunda mseto kati ya vyama – hii inaweza kufanywa kupitia mfumo wa uwakilishi wenye uwiano kama inavyopendekezewa nchi ya Kenya. Na kama wabunge walivyo, itakuwa rahisi zaidi kama watapewa mamlaka licha ya kuwa "mawaziri wa kawaida". Kwa hivyo, uwezekano, wa kuwepo 'Naibu Waziri Mkuu' huenda ni jambo la thamani sana. Hii sio kufanya mabezo kisiasa lakini wapiga kura huenda wakaikubali kwa wepesi. Jukumu la Waziri Mkuu katika mfumo huu ni kuwa Mkuu wa Serikali. Anawateua Mawaziri; na yeye na Baraza lake la Mawaziri wanatunga sera.Waziri mkuu shrti aungwe mkono na wawakilishi – yaani Bunge. Kwa jinsi hii mfumo huu ni sawa na ule wa Ulaya. Kwanza, Waziri Mkuu lazima awe Mbunge.

Wengi wamedai kwamba hawajapendelea mfumo wa kuwateua Mawaziri. Hivi sasa, Waziri lazima awe Mbunge. Matokeo yake ni kwamba wananchi wa kutoka eneobunge la waziri na hawamuoni mbunge wao – hawahudumiwi mno na mbunge wao wakilinganishwa na maeneobunge mengine. Na kama eneobunge litafaidika kwa sababu mbunge wao ni "mkubwa" – Waziri – kama wachaguzi wanavyojua hii ni njia mojawapo ya faida za kifisadi. Na kwa sababu uamuzi wa Rais wa kuteua mawaziri ni wa Rais anayeteua kutoka miongoni mwa wabunge, na nafasi hizo zitawaendea wananchi ambao wameonyesha uaminifu wa kisiasa, kuna uhakika kuwa hakuna sifa nyingine inayozingatiwa ili kumfanya mtu waziri.

Baadhi ya watu walidai kwamba mawaziri sharti wawe na sifa fulani ili kushikilia nyadhifa hizi; yaani hii ni kusema kwamba Waziri wa Afya awe ni Daktari, Waziri wa elimu awe ni mwalimu n.k. Kuna tatizo katika mpangilio wa namna hii: Jukumu la Waziri ni sawa na lile la mwanasiasa. Anahitajika kuelewa mambo katika misingi ya kisiasa na wala sio katika misingi ya kitaaluma. Utaaluma ni wa wafanyikazi wa umma. Kama Waziri anajua- ama anahisi anajua hii itatibuka na kuzua mgogoro kati yake na wahudumu wa umma. Anaweza kudhoofisha pakubwa umaarifu wake kisiasa. Kwa upande mwingine, kuna kitu cha kusifu kuhusu waziri mwenye sifa za kielimu, licha ya kuwa muungaji mkono mwaninifu. Pendekezo la tume ni kwamba, Waziri Mkuu atawateua mawaziri wake kutoka nje ya Bunge. Hii ina maanisha kuwa nafasi ya uamuzi na kuchagua ni pana zaidi. Uteuzi wa mawaziri ni sharti uidhinishwe na bunge. Ili kuhakikisha kwamba Waziri Mkuu ananufaika kwa upana, Muswada wa Katiba unaeleza kwamba mawaziri watateuliwa kwa misingi ya uzoefu wao na ujuzi watakaokuja nao. Kama waziri ni mbunge, lazima aache kiti hicho na pafanywe uchaguzi mdogo. Ina maana kwamba,kuteukiwa waziri kuna hatari zake kwa wabunge kwa sababu ikwa watafutwa na waziri mkuu hawatakuwa na kiti cha uwaziri na kile cha ubunge.

Mswada huu pia unapendekeza kuwa mawaziri wawe wachache kuliko jinsi ambavyo wamekuwa. Mawaziri wasizidi 15 na manaibu wao pia wasizidi 15 ikiwemo afisi za Manaibu wa Waziri Mkuu. Jukumu la Naibu wa Waziri ni kuwakilisha na kuitetea Wizara yake Bungeni. Mawaziri lazima wahudhurie Bunge wakati ambapo sheria muhimu na kauli za wizara zinawasilishwa, ama kama kamati itawataka kufanya hivyo. Ni muhimu pawe na manaibu wawili wa Waziri Mkuu. Bunge lazima limuunge mkono waziri mkuu wakati anapoteuliwa. Itakuwaje ukikosa imani Bungeni? Panaweza kuwa na kura ya kutokuwa na imani? Jawabu ni ndio. Hii itamfuta Waziri Mkuu kazi – lakini haimaanishi kwamba patafanyika uchaguzi mkuu. Rais atajaribu kuchagua mtu ambaye anahisi ataweza kukishika kiti hicho vizuri na uwe ukakamavu bungeni. Atafanya hivyo kupitia ushauri wa viongozi wa vyama. Kama watashindwa kuunda serikali mpya baada ya siku 30 basi uchaguzi mkuu utafanywa.

a.) Rais

Si ajabu kwamba taarifa nyingi tulizopokea ama zilizotumwa kwa Tume hii, zilieleza zaidi kuwa Rais wa Serikali ya Kenya amekuwa ndiye muhimu sana katika serikali ya Kenya kwa miaka mingi. Miongoni mwa maoni waliyotoa ni:

- Rais awe kielelezo cha umoja wa taifa.
- Rais asiwe na uwezo wa kutoshtakiwa.
- Rais aendelee kuchaguliwa moja kwa moja.
- Sifa za Rais zihusishe umri wa kiwango cha chini na kiwango cha juu, kiwango fulani cha sifa za kielimu, na awe ameoa/ameolewa.
- Rais asiwe mbunge na wagombeaji wa urais hawawezi kusimama bungeni.
- Makamu wa Rais sharti awe “mgombea mwenza” wa Rais.
- Bunge liwe na uwezo wa kumtengua Rais.
- Awamu ya kipindi cha afisi ya Rais iwe ni miaka 5 kwa vipindi viwili, kama ilivyo sasa.

Maoni na mapendekezo ya Tume yaliohuishwa kwenye mswada wa Katiba yanafanana na mapendekezo (ijapokuwa hatukuafiki suala la Rais kuoa/kuolewa).
Masharti mengine yanayohusu uteuzi ni:

- Wagombeaji wanaweza kuteuliwa na chama cha kisiasa kilichosajiliwa ama wawe wagombea huria
- Wagombeaji wa urais lazima wawe na umri usiopungua miaka thelathini na mitano (35) na wasizidi miaka sabini (70)
- Wagombeaji wa kiti cha urais lazima wawe na uadilifu wa hali ya juu.
- Wagombeaji wa urais hawawezi kugombea kiti cha ubunge.
- Mgombeaji lazima asimame na mwenza wake, ambaye atakuwa makamu wa Rais endapo mgombeaji huyo atashinda.

Baadhi ya sifa za mfumo kama huu inavyomhusu Rais zimeshajadiliwa hapo awali ikiwemo hatari za kuhusian na uchaguzi.

Jukumu la Rais ni lipi katika mfumo ulio na Waziri Mkuu ambao unapendekezwa na Tume? Tumeona wajibu mmoja tu - ule wa kumchagua Waziri Mkuu. Rais hana uhuru wa kujiamulia. Kimsingi atamchagua Waziri Mkuu anayeongoza chama kutokana na kuungwa mkono na wengi. Pale ambapo hakuna maongozi ya chama, kimoja, jukumu la kumtambua Waziri Mkuu linategemea viongozi wa vyama. Lakini Rais anaweza kuwa na jukumu muhimu – uthabiti wa chaguo la Rais utategemea mno pakubwa heshima aliyo nayo.

Jukumu la kimsingi la Rais kama ilivyokisiwa katika mswada wa Katiba ni lile ya kuwa kielelezo cha taifa. Lakini jukumu lenyewe si la kiishara tu. Kutakuwa na majukumu ambayo yameainishwa ili kuifanya serikali iwajibike kufuatia maongozi ya Katiba. Mswada wa katiba unaeleza kwamba jukumu la Rais linahusisha: Rais anaashiria na kubainisha umoja wa taifa. Lazima ajiuzulu kutoka kwenye uongozi wa chama chochote cha kisiasa.

- Rais lazima alinde uhuru wa taifa.
- Rais lazima aheshimu wingi wa kitaifa na ulinzi wa haki za binadamu
- Rais lazima alinde Katiba na atetee kanuni za sheria

Jukumu muhimu linalohusu sheria:

- Idhini ya Rais inahitajika katika kukubalika kwa miswada ya kisheria na kanuni zake. Rais anaweza kurejesha muswada ama kanuni ili kufikiriwa upya. Lazima aweke sahihi ama kupitisha mswada ukirudishwa kwake, pawe ama pasiwe na marekebisho, ila tu ikiwa Rais ameona kwamba haufuati kanuni za kikatiba, hili likitokea, ataagiza mswada huo kufikishwa katika mahakama ya juu kwa maoni na ushauri zaidi.

Majukumu mengine muhimu ambayo Rais anatekeleza bila kufuata ushauri wa yeyote ni:

- Rais ana uwezo wa kuomba Mahakama ya Juu ushauri katika suala la kikatiba.
- Rais ana haki ya kuhutubia Bunge.
- Rais atahakikisha kuwa asasi zinazoundwa ili kulinda na kukuza haki na demokrasia zinapata ufadhili wa fedha unaostahiki.
- Rais anaweza kupendekeza hatua za kisheria ili zijadiliwe na Baraza la Mawaziri

Ili Rais atekeleze majukumu yake:

- Ni lazima Waziri Mkuu amfahamishe Rais kuhusu shughuli za kiutawala mara kwa mara.

Kisha kuna majukumu mengine ya kiishara lakini ambayo ni muhimu:

- Ni Mkuu wa majeshi na msimamizi wa Baraza la Usalama wa Taifa (National Security Council).
- Kutangaza Hali ya Hatari baada ya kushauriana na Waziri Mkuu na Baraza la Usalama wa Taifa na kuidhinishwa na Bunge katika muda wa wiki mbili
- Rais atakuwa na uwezo wa kutangaza vita baada ya kushauriana na Baraza la Mawaziri na kudhihirishwa na Bunge.
- Kuteua mahakimu kulingana na mapendekezo ya Tume ya Huduma za Mahakama na kukubaliwa na Kamati ya Mahakimu wa Bunge.
- Rais ana uwezo wa kuanzisha taratibu za kuwaondoa mahakimu wasio waadilifu.
- Kuidhinisha kirasmi mikataba ambayo imewekwa na serikali na kukubaliwa na Bunge na atahakikisha utekelezaji wake; atazidi kufahamishwa kuhusu mashauriano yote ya mikataba
- Kuwapokea Mabalozi
- Kuteua Mabalozi na maafisa wengine mashuhuri, Tume huria na maafisa katika misingi iliyowekwa na kanuni za katiba.
- kutoa misamaha kirasmi n.k.
- kutoa tuzo ambazo zimewekwa na sheria ya Bunge kufuatia mapendekezo ya Baraza la Mawaziri.
- Kuongoza ufunguzi rasmi wa Bunge

Masharti yamewekwa ili kuhakikisha kwamba uwezo wa Rais unatokana na Katiba pekee.

Mlinganisho Mfupi kati ya Rais na Waziri Mkuu ilivyo Katika Mswada wa Katiba

Rais	Waziri Mkuu
♦ Anateuliwa moja kwa moja na wananchi ♦ Anahudumu kwa muda usiozidi awamu mbili ♦ Anaweza kutenguliwa na Bunge mbele ya Baraza La Taifa. ♦ Lazima asiwe mbunge ♦ Si mshiriki katika Baraza la Mawaziri ♦ Ana majukumu muhimu anayotekeleza kwa busara yake, kwa mfano, anaweza kurudisha mswada kwa Baraza la Taifa ili ufikiriwe upya ♦ Ana majukumu mengi ya kistaha ♦ Anaweza kuhutubia Taifa au Bunge	♦ Anateuliwa kirasmi na Rais lakini ni lazima aungwe mkono na Ukumbi wa Wabunge ♦ Hakuna makadirio ya kikatiba ya muda wake wa kuhudumu ♦ Anaweza kutolewa kupitia kura ya kutokuwa na imani ♦ Anawachagua Mawaziri na ni mwenyekiti wa Baraza la Mawaziri ♦ Anaendesha serikali katika maswala ya siku baada ya siku ♦ Sharti ahudhurie Bunge

Ijapokuwa Rais hatakuwa na uwezo mwingi kama ilivyo hivi sasa, huenda pakatokea hali ambapo Rais anatuhumiwa kuhusika katika ufisadi, au ni mgonjwa mno hivi kwamba hawezi kutekeleza wajibu wake, au anazuia utekelezaji wa shughuli za serikali. Ikiwa panatokea hali ambayo shughuli za taifa zimesimama kwa sababu Waziri Mkuu na Rais hawasikilizani, hatimaye tatizo hilo halina budi kusuluhishwa na Bunge. Wakihisi kwamba tatizo linatokana na Waziri Mkuu wanaweza kupiga kura ya kutokuwa na imani. Wakihisi kwamba tatizo linatokana na Rais, wanaweza kuanzisha utaratibu wa kumtengua:

- Rais anaweza kufanyiwa utaratibu wa kutenguliwa kwa kuvunja katiba au sheria au utovu wa nidhamu wa hali ya juu kutokana na mashtaka yaliyowasilishwa na wanachama wengi wa Bunge na kuamuliwa na Baraza la Taifa kupitia wingi wa kura wa thuluthi mbili.

5. Serikali Ya Uwezo Uliopunguzwa na Serikali ya Wilaya

Jambo hili- pamoja na kuwepo kwa Ukumbi wa pili Bungeni – ndilo lililokuwa suala nyeti zaidi kwenye Tume, pamoja na nchini. Kwa hakika, masuala yote mawili yanaingiliana: jukumu la Ukumbi wa juu mara nyingi ni kulinda mfumo wa serikali iliyopunguziwa na kusambaziwa uwezo wake. Mapendekezo tuliyotoa yanadhamiriwa kufanikisha malengo fulani:

- Kuleta serikali karibu na umma- ili hasa kuvipa nguvu vyombo vinavyoweza kuchangia ugawanyaji wa haki wa rasilmali, na kuwa na maamuzi yaliyotolewa na watu wanaoheshimiwa na wanajamii.
- Kutumia vyombo vinavyoeleweka na wananchi na wanavyoweza kuona kama wanavielewa: ndiyo sababu ya kusisitiza wilaya na vijiji, na matumizi ya mikoa na kata.
- Kuimarisha utenganishaji wa madaraka na kwa hivyo kupunguza mazoea, ya kulundikiza mamlaka miongoni mwa wachache, na kuimarisha uwajibikaji

Kutakuwa na viwango vitatu vya kuchagua baraza moja kwa moja:
- Wilaya (miji mikuu na manispaa itakuwa katika kiwango hiki, na mabaraza yake yatakuwa mabaraza ya mji au mabaraza ya manispaa, kulingana na hali ilivyo).
- Kata (miji na vituo vya soko vitakuwa katika kiwango hiki).
- Vijiji

Wilaya zitaunda Baraza la Mkoa ili kusaidia uratibishaji wa shughuli. Nairobi itakuwa na hadhi yake maalumu kama Jiji la Taifa. Mabaraza ya Wilaya na Mabaraza ya Mikoa yatakuwa na madaraka ya kutunga sheria. Mabaraza ya viwango vya chini yatakuwa na uwezo wa mamlaka tu ya kutekeleza sera zilizotungwa na viwango vya juu, lakini yatakuwa na madaraka ya juhudi za wanajamii kuleta maendeleo, na madaraka kutengeneza sheria ndogo ndogo kwa ajili ya masuala ya mitaani na kutekeleza hasa sheria zilizoundwa katika viwango vya juu..

Kuunda Sheria katika Viwango Tofauti

Kutakuwa na orodha ya uwezo utakaoiwezesha serikali ya kitaifa tu kutungia sheria. Orodha hii inahusu masuala kama vile usalama wa taifa, uhamiaji, uraia, fedha, viwanja vya ndege vya kimataifa, biashara ya kimataifa n.k. Kutakuwa na orodha ya masuala ambayo wilaya zinaweza kutungia sheria. Maswala haya yatajumuisha elimu ya shule ya msingi, kliniki, barabara za wilayani, utoaji wa maji, kulinda sheria na utangamano n.k. Kutakuwa na orodha ya tatu ya masuala ambayo yanaweza kushughulikiwa na serikali zote, serikali ya kitaifa na ya wilayani. Masuala haya yatajumuisha kilimo, elimu ya sekondari, hospitali, ardhi na mazingira. Mabaraza ya Mkoani yatakuwa na uwezo mdogo wa kutunga sheria kuhusiana na majukumu yao ya kuratibu.

6. Uchaguzi wa Rais, Bunge, Baraza la Kitaifa na Mamlaka Zilizosambaziwa uwezo

Utaratibu wa uchaguzi unaohusu afisi na asasi hizi umejadiliwa tayari. Idadi kubwa ya watu ilitufahamisha kwamba uchaguzi wa urais na ubunge unapasa kufanywa wakati tofauti. Ingawa hii inaweza kuzidisha gharama, tunaidhinisha maoni haya na kupendekeza kwamba uchaguzi wa makundi yote yaliyotajwa hapo juu ufanywe wakati tofauti.

7. Mahakama na Mfumo wa Mahakama

Mahakama ni sehemu muhimu sana ya mpangilio wa kikatiba wa nchi. Nyingi ya taasisi na kanuni zilizojumuishwa katika msuada wa Katiba zitakuwa tu na uwezo wa kutenda kazi iwapo mahakama na taratibu nyingine hazitapendelea upande wowote, zitatekeleza kazi haraka, zitakuwa za kuaminika na kuweza kufikiwa na wananchi. Kijumla, mahakama:

- Zitoe ufafanuzi wenye uwezo wa sheria, bila kuagizwa au kushinikizwa na mamlaka ya nchi au upande wowote ule
- Zitatue mizozo zinayowasilishiwa
- Kwa kutatua mizozo kuambatana na sheria, na kwa ujumla kutekeleza kanuni ya sheria au utawala wa kisheria zinasaidia kuleta udhabiti na kuhakikisha kuwepo kwa amani na hali inayofaa kwa watu kufanya mikataba na makubaliano ya kibiashara
- Zihakikishe ukuu wa Katiba kupitia njia tofauti, ikiwa ni pamoja na kuondoa sheria zinazokinzana na Katiba, kuandaa kaida za kiKatiba na kusaidia katika kuzifanyia marekebisho kutegemea mabadiliko ya hali ya kijamii na kiuchumi, kusisitiza heshima kwa utaratibu wa Katiba na maadili kwa njia moja, kupitia uamuzi wa kishawishi na kitaalauma, kuweka bunge pamoja na mamlaka ya nchi katika uwezo wao kisheria na kuzuia uholela na mienendo isiyofaa, na kulinda haki na uhuru wa wananchi pamoja na maslahi ya umma.

Katika kutambua umuhimu wa majukumu yake mahakama inapewa heshima kuu na upendeleo wa aina fulani; ukosoaji wa mahakama hata kama ni wa kweli unazimwa; majaji wanapewa usalama wa kazi kuwawezesha kuwa uhuru na kutopendelea upande wowote, na masharti yao ya kazi yanalenga kuwahakikishia utulivu na kuondoa majaribu ya kukabali kupokea pesa au vishawishi vingine ili kuwapendelea wanaohusika kesini.

Tume inahitajika kutoa mapendekezo kuhusu mahakama kwa jumla na hasa kuanzisha na kuweka mamlaka ya kisheria ya mahakama, kulenga hatua za kuhakikisha uwezo wa kutenda kazi, uwajibikaji, ubora wa kutenda kazi, nidhamu na uhuria wa mahakama (sehemu 17(d)(v)). Inahitajika kujumuisha utaratibu wa kupunguza na kusambaza madaraka kati ya mahakama, bunge, mamlaka ya serikali, na vipimo na visawazisho ‘kuhakikisha uwajibikaji wa serikali na maafisa wake kwa wananchi wa Kenya’ (sehemu 3(c)) Hii inatambua mahakama kama chombo muhimu cha taifa na jukumu lake la kuwa kama kipimo cha madaraka ya bunge na mamlaka ya serikali hasa kuhusiana na kanuni za kiKatiba).

a.) Matumaini

Kwa hivi sasa mahakama yako sambamba na wanasiasa na polisi kama sekta zinazokosolewa zaidi na Wakenya. Miongoni mwa Wakenya wa kawaida, masuala ya kuchelewesha kesi, gharama na ufisadi ndiyo masuala yanayowatia hofu zaidi. Kwa upande wa wanasheria kuna hofu kuhusu uwezo wao wa kutenda kazi, na kukosa kujisimamia kutokana na ushawishi wa serikali.

- Watu wengi walitufahamisha kuwa wamepoteza imani na mahakama na walitaka mizozo yao kusuluhishwa na wazee au njia nyingine za kitamaduni.
- Wengi walipendekeza kuanzishwa kwa mahakama ya kiKatiba au mahakama ya juu.
- Utaratibu wa kuwateua majaji unapaswa kutoa nafasi kwa wote, uwe wazi na wa kuwajibika. Wengi walipendekeza kuwa majaji wachaguliwe na tume ya Huduma ya Mahakama iliyopanuliwa na iliyo huru, kwa kuwajumuisha wawakilishi kutoka chama cha wanasheria, vitivo vya sheria na pia umma, na kwamba wanaochaguliwa kuteuliwa kama majaji wachunguzwe na bunge.
- Watu wengi walisema kuwa ni lazima jaji awe na shahada kutoka chuo kikuu (kinyume na mafunzo ya kitaaluma pekee), au hata shahada ya uzamili (*masters*), huku wengine wakisema sifa za watakaofuzu kuteuliwa kuwa majaji zinapasa kujumuisha maadili yao.
- Wengi walitaka kubadilisha utaratibu wa kuwaondoa majaji; baadhi walipendekeza kuwa raia yeyote anapaswa kuwa na haki ya kufikisha malalamiko mbele ya Tume za Huduma za Mahakama ya kumtaka jaji kuondolewa
- Watu wengi na mashirika, kama vile Chama cha Wanasheria, walipendekeza kuwa majaji wa sasa wanapaswa kuondolewa.

Ni muhimu kusisitiza kuwa Tume ya Marekebisho ya Katiba haisemi kuwa majaji wote hawana uwezo wa kutenda kazi au ni wafisadi. Pili, Tume inakubali kuwa mfumo wa mahakama unajumuisha watu wengi ambao si majaji: wasajili, makarani, n.k. na kuwa baadhi ya watu hawa pia wamechangia katika kuharibu sifa ya mfumo wa mahakama nchini Kenya. Tatu, ufisadi huhusisha pande mbili, wanasheria na wateja wanaotoa hongo, au mipango isiyo halali pia inaweza kulaumiwa. Hali ni kama hivyo hata kuhusu uingiliaji kati wa serikali: waziri anayeingilia kati kumtaka jaji kufanya uamuzi wa kesi kwa njia fulani pia ana hatia kama alivyo jaji anayekubali shinikizo zake. Wanasheria wanaokosa kuelezea wazi misimamo yao, ushahidi na mamlaka ya kisheria kwa kesi zao pia wanapaswa kuwajibika kwa uamuzi usioweza kutetewa. Na hatimaye, kuna hali kuhusu mfumo mzima wa mahakama- inayofanana na hali nyingine- ambayo ni ya mbali, ya kushangaza, na ya kigeni.

Kutokana na unyeti wa suala hili, Tume ilialika kamati ya majaji maarufu kutoka mataifa ya Jumuia ya Madola kufanya uchunguzi na kupendeza baadhi ya hatua zinazopasa kuchukuliwa. Katika ripoti yake, kamati hiyo ilisema: 'Huku majaji wengi nchini Kenya wakiendelea kutekeleza wajibu wa nyadhifa zao kwa imani ya viapo vyao kwa mujibu wa misingi ya mahakama, imani ya wananchi kuhusu uhuru na uwezo wa mahakama kutopendelea upande wowote imetoweka kabisa.' Kundi lilioalikwa na Serikali kutoa ushauri kuhusu suala la ufisadi na kutoa ripoti yake mapema mwaka 2002 lilisema, 'Kulikuwa na maafikiano kati ya watu wote waliohojiwa kuwa mahakama hazina uadilifu na ni fisadi. Maoni hayo yalitolewa na wanasiasa, wafanyibiashara, jamii ya kidini, na makundi mengine husika. Jaji Mkuu hakukubaliana na maoni hayo.' Kundi hilo pia liliarifiwa na duru za kuaminika kuwa wakati majaji walipofikiriwa kuteuliwa kuongoza Mamlaka ya Kupambana na Ufisadi (KACA) ilibainika kuwa ni majaji watatu pekee waliotambuliwa kutokuwa na doa kutokana na ufisadi.

Mswada wa Katiba unapendekeza:

- Kifungu cha kufafanua kanuni za mfumo wa mahakama ulio na haki kujumuisha:
    - Kutopendelea upande wowote, kufikiwa;
    - kuundwa kwa mahakama kunapaswa kujumuisha kanuni ya usawazisho ili kuangazia kuwepo kwa tofauti mbali mbali nchini na usawazisho wa jinsia.
    - ni lazima majaji wawe huru na mfumo uwajibike.
    - haki haipaswi kucheleweshwa.
    - majaji wanapaswa kuchukulia kuendeleza sheria kuwa jukumu lao na kutofungwa sana na kielelezo cha jambo lililowahi kutokea au utaaluma, panapaswa kuwepo na haki ya kukata rufani katika kesi zote isipokuwa kesi fulani maalum.
    - kikawaida mahakama zifanye vikao vya wazi.
    - zinapaswa kutoa fursa ya kuhimiza mapatano.
    - kikanuni kuhusishwa kwa wananchi katika utoaji wa haki unapaswa kuhimizwa.
    - mfumo unapaswa kuwa kamilifu na
    - taaluma ya mahakama inapaswa kujiona kama ambao umetekeleleza majukumu ya kufanikisha maadili haya na malengo, ukizingatia majukumu muhimu kwa wateja na jamii.
- Taarifa kuwa uwezo wa mahakama unatekelezwa na mahakama.
- Mahakama mpya katika kilele cha mfumo: Mahakama ya Juu itakayokuwa na majaji wapya kabisa. Mahakama ya Juu isikize kesi za rufani kutoka kwa mahakama zilizo chini yake, na iwe na uwezo maluum wa kiKatiba. Majukumu yake ni kuanzisha viwango vipya vya uadilifu na ubora katika utoaji wa haki – sio tu katika masuala ya kiKatiba lakini kijumla.
- Kanuni kuwa jaji mkuu zaidi wa Mahakama ya Juu ateuliwa kuwa Jaji Mkuu wa mfumo mzima wa mahakama (kutegemea masharti maalum kuhusu uteuzi wa awali).

- Jaji mkuu zaidi wa Mahakama ya Rufani ndiye Rais wa Mahakama ya Rufani.
- Jaji mkuu zaidi wa Mahakama Kuu ndiye Jaji Mkuu wa Mahakama Kuu/Rais wa Mahakama Kuu.
- Masharti ya kufikiwa kwa mahakama yafafanuliwe: kufikiwa kimahali hasa kwa wale walemavu, matumizi ya breli na lugha-ishara ya Kenya na maadili ya huduma ya umma na masuala ya malipo

Uhuru wa mahakama ndio thamani ya kimsingi inayotolewa kwenye Katiba. Kanuni katika mswada wa Katiba zimeimarishwa sana ikiwa ni pamoja na njia zifuatazo:

- Tume ya Huduma za Mahakama inayowateua majaji iundwe upya ili kuifanya kuwa huru zaidi na kuwahusisha watu wengi zaidi wasio wanachama wa mfumo wa kisheria.
- Lazima uteuzi fulani wa Mahakama uidhinishwe na Bunge
- Kuna taarifa kuwa mahakama zitakuwa huru, kuongezea kwa hili kwa kusema kwamba
    - Mishahara n.k haitapunguzwa wakati jaji anapokuwa bado anashikilia mamlaka, kwamba afisi haiwezi kuvunjwa wakati jaji anapokuwa mamlakani.
    - Kwamba gharama ya mahakama itatoka katika hazina ya jumla.
    - Kwamba lazima mishahara na masharti ya kazi yaweza kuhimiza uadilifu na msimamo wa kujisimamia (au kutopendelea upande wowote
    - Kuhakikisha kwamba majaji hawatawajibika kiraia au kisheria kwa makosa ya jinai, kwa yale wanayotenda wakitekeleza wadhifa wao kama majaji (ni muhimu kufafanua kuwa, haya hayahusu ufisadi); hili lina madhumuni ya kuhakikisha kuwa majaji wanapata uhuru wa kutoa maoni yao ya dhati kuhusu sheria na kesi zinazofikishwa mbele yao.
- Kama vile masharti ya kawaida ya kuhitajika kuwa umehudumu katika taaluma ya sheria kwa miaka mingi, kabla ya kuteuliwa kuwa jaji wa mahakama za viwango vya juu, panapaswa kuwapo kauli kuwa ni lazima majaji wawe na kiwango cha juu cha uadilifu kisichoweza kutilika shaka.

Mifumo mipya ya Mahakama



b.) Mahakama za Kadhi

Katiba iliyopo inatoa nafasi ya mahakama za Kadhi kutumia sheria ya kiislamu kuhusiana na masuala ya kibinafsi, ndoa, talaka, na urithi, katika kesi ambapo pande zote mbili zinafuata imani ya dini ya Kiislamu (5.66). Hadhi ya kikatiba ya mahakama za Kadhi ina msingi wake katika mapatano yaliyozihusisha Uingereza, Kenya na Zanzibar, mnamo mwaka wa 1963, ambapo Sultani wa Zanzibar alikubali kukomesha utawala wake wa eneo la pwani, na kuikabidhi Kenya eneo hilo. Kwa upande wake, serikali ya Kenya ilikubali kuchukua hatua za kulinda masuala yaliyokuwa muhimu, ukiwemo mfumo wa sheria za kiislamu na mahakama.

Tume ilipokea mapendekezo kadhaa kuhusu upanuzi na marekebisho ambayo yanapaswa kufanyiwa mamlaka yake kisheria, pamoja na muundo wake, hasa kutoka kwa jamii za Kiislamu. Walishikilia kwamba Kadhi, pamoja na mahakama zao, hawaheshimiwi na kutambuliwa ipasavyo. Walielezea matatizo kadhaa katika sheria na utekelezaji wake kuhusiana na matumizi ya sheria ya Kiislamu. Mahakama za Kadhi bado hazijajumuishwa ipasavyo katika mfumo wa kitaifa wa kisheria, au kupewa muundo na mfumo kamili wa msonge wa madaraka, na pia kukosa kubainisha kati ya jukumu la kisheria la Kadhi Mkuu na jukumu lake kama kiongozi wa kidini. Kwa mfano, kesi za rufani kutoka Mahakama ya Kadhi huwasilishwa katika Mahakama Kuu iliyo na majaji wachache mno wanaofahamu sheria ya Kiislamu. Kanuni za utaratibu au ushahidi bado hazijafanywa kuwa sheria, na kwa hivyo sheria ya ushahidi ndiyo hutumiwa ijapokuwa sheria hiyo inaeleza wazi wazi kwamba haipaswi kutumiwa katika Mahakama za Kadhi. Sheria ya Kiislamu kuhusu masuala ya kibinafsi haijapangwa kitaratibu, na suala hili huachiwa mahakama binafsi kulishughulikia kwa njia yake. Kukosa kuwapo kwa ripoti ya uamuzi kumetatiza kukua kwa falsafa ya sheria ya Kiislamu.

Hasa jamii ya Waislamu iliomba Tume kuhakikisha kuwepo kwa mahakama za Kadhi za kutosha kote nchini; kuwa mamlaka yao kisheria yapanuliwe ili yajumuishe masuala ya kiraia na kibiashara, kuwa sifa za kielimu za makadhi zipandishwe ili kuimarisha ubora wa utendakazi, na kuwa utaratibu mpya wa sheria za Kiislamu wa kukata rufani uanzishwe. Ilikuwa muhimu kuhakikisha kuwa baadhi ya makadhi wanateuliwa kutoka jamii ya Washia katika kujali maslahi yao. Jamii ya Waislamu itakiwe kushauri kuhusu uteuzi wa Kadhi Mkuu, na Makadhi wengine.

Baada ya kutafakari kwa makini kuhusu uwezekano wa mvutano kati ya lengo la umoja wa taifa na kutambua kuwepo kwa dini mbalimbali, Tume ilikubali marekebisho mengi yaliyotolewa kama ifuatavyo:

- Panapaswa kuwepo idadi fulani ya mahakama za Kadhi ili Waislamu wote waweze kuzifikia.

Mfumo wa msonge wa madaraka katika mahakama za Kadhi utakuwa ifuatavyo:

- Mahakama ya Kadhi ya Wilaya kama mahakama ya kwanza ikisimamiwa na jaji mmoja
- Mahakama ya Kadhi ya Rufaa ikisimamiwa na Kadhi Mkuu na makadhi wawili.
- Mahakama ya Kadhi ya Mkoa, ikisimamiwa na Jaji mmoja
- Mahakama ya Kadhi ya Rufaa ikisimamiwa na Kadhi Mkuu na makadhi wawili, (kwa sababu wilaya nyingi zenye idadi kubwa ya uislamu ziko mbali na Nairobi, ambako mahakama kuu ya Kadhi ya Rufani itakutana. Kanuni zilitaja mahakama kwenda kwa wilaya mara kwa mara.
- Mahakama kuu ya kushughulikia kesi za Rufani kutoka Mahakama ya Kadhi ya Rufaa kuhusu Katiba pekee.

- Mahakama za Kadhi zitakuwa na mamlaka ya kisheria kushughulikia masuala yanayohusu sheria ya kiraia na kibiashara ikiwa pande zote husika zinafuata imani ya dini ya Kiislamu, kupitia utaratibu wa mahakama ndogo ndogo za malalamiko (zinazotarajiwa kuundwa hivi karibuni), bila kuathiri haki ya pande husika kwenda katika mahakama nyingine au mahakama maalum zilizo na mamlaka ya kisheria kuhusu masuala hayo.
- Kadhi Mkuu atakuwa na hadhi, fursa na kinga sawa na jaji wa Mahakama Kuu, kinga maalum, kama Hakimu Mkuu, naye Kadhi kama Hakimu Mkazi.
- Kadhi Mkuu na Makadhi wengine watateuliwa kwa kufuata utaratibu sawa na majaji wengine. Licha ya Kadhi Mkuu atakayekuwa mwanachama wa Tume ya Huduma za Mahakama, makadhi wengine watateuliwa na chama cha kitaifa cha Waislamu.
- Sifa za makadhi watakaoteuliwa ni pamoja na kuwa na shahada katika Sheria ya Kiislamu kutoka chuo kikuu kinachotambulika na kuwa wakili wa Mahakama Kuu, na, kwa upande wa Kadhi Mkuu, uzoefu wa miaka isiyopungua kumi, na kwa makadhi wengine tajriba ya miaka isiyopungua mitano kama wakili wa Mahakama Kuu.
- Makadhi watakuwa maafisa wa mahakama kikamilifu na hawatahitajika kutekeleza wajibu wa kidini.

Jamii ya Waislamu pia iliomba Tume kuzipa mahakama za Kadhi mamlaka ya kisheria kusimamia mali ya Wakf. Ingawa Tume inaonelea kwamba Waislamu wenyewe wanapaswa kupewa jukumu la kusimamia mali ya Wakf, haiamini kuwa mahakama zinafaa kukabidhiwa jukumu hili, na kwa hivyo inapendekeza kuwa mapendekezo yafanyiwe Sheria ya Makamishna wa Wakf na kujumuisha matarajio ya jamii ya Waislamu. Mivutano ya kisheria kuhusu mali ya wakf inayohusu mivutano ya sheria ya Kiislamu itashughulikiwa na mahakama ya Kadhi.

c. Uwajibikaji na Udhibiti

Ni kanuni muhimu kikatiba kwamba majaji wawe na usalama wa kazi. Wakati mmoja, majaji hawakuhitajika kustaafu, lakini siku hizi mataifa mengi yameweka umri ambapo majaji wanapaswa kustaafu. Mswada unaeleza kuwa:

- Umri wa kustaafu kwa majaji na mahakimu wote ni miaka 65. Ni muhimu pia kuwa na mfumo unaotoa utaratibu wa majaji kuondolewa kutokana na utendakazi duni na tabia mbovu lakini pia ni muhimu kuwa kuondolewa huko kuwe kugumu zaidi. Kwa mujibu wa mswada:
- Mfumo wa kuondolewa kwa majaji unapaswa kuwa kwa misingi iliyopendekezwa na kamati ya wataalamu:

    - Katiba itatoa uwezo wa mtu yeyote au asasi, chama au kundi la watu kuwasilisha malalamiko dhidi ya jaji yeyote kwa tume ya Huduma za Majaji.
    - Tume ya Huduma za Mahakama ichunguze malalamiko na kumuomba Rais kuteua mahakama maalum ya majaji iliyo na majaji mashuhuri, kusikiza malalamiko hayo.
    - Mahakama maalum iwasilishe matokeo ya uchunguzi na mapendekezo yake kwa Rais ambaye ni lazima achukue hatua kuambatana na mapendekezo hayo.
- Kuondolewa kutekelezwe tu iwapo jaji ameshindwa kutekeleza majukumu yake kama jaji kutokana na udhaifu wa mwili au akili au kwa kuwa na tabia mbovu, mienendo mibovu, au kushindwa kujimudu kikazi kufikia kiwango ambapo jaji anakuwa hapaswi kushikilia wadhifa wake.
- Ni lazima Tume ya Huduma za Mahakama itayarishe kanuni za maadili ya Mahakama, na kuyatangaza vya kutosha ili majaji wenyewe, wafanyikazi wa mahakama na wananchi wote kwa jumla wafahamu vyema mwenendo bora kwa majaji.

d.) Hatua za Mpito

Suala gumu zaidi kuhusu mahakama ambalo Tume ya Marekebisho ya Katiba ya Kenya imekabiliana nalo ni, kuhusu kitakachofanyiwa majaji waliopo. Mapendekezo ya Jopo la Wataalamu yalikuwa kwamba majaji waliopo wasiondolewe wote kwa pamoja. Lakini Chama cha Wanasheria kilipendekeza kuwa hatua hii inapasa kuchukuliwa. Tume ya Marekebisho ya Katiba ya Kenya inaamini kuwa ikiwa hatua muhimu na kali hazitachukuliwa, basi huenda uKatiba nchini Kenya ukawa hatarini. Mahakama ni mojawapo ya vyombo muhimu katika utendakazi bora wa Katiba.

Na bado kuna ushahidi wa kutosha kuwa majaji wameteuliwa kwa sababu zisizofaa, na wengi wameonekana kukosa uwezo wa kutenda kazi kwa uadilifu. Hata hivyo tumeamua kutochukua hatua kali kama kuwaondoa majaji wote waliopo. Kimataifa hatua kama hiyo itachukuliwa kama kuingilia kati uhuru wa mahakama. Humu nchini, hatua hiyo inaweza kufifisha ‘mwiko’ dhidi ya kuwaondoa majaji. Aidha, majaji waaminifu watachukulia kwamba wanalengwa pamoja/sawa na majaji walio na hatia. Kwa hivyo, tunapendekeza:

- Majaji wastaafu wakitimiza miaka sitini na tano (65)
- Majaji watakaochagua kustaafu Katiba mpya ikianza kutekelezwa wapewe fungu la kustaafu.
- Majaji wanaokataa kuchukua fedha hizo na kustaafu wanaweza kuchunguzwa kuhusu iwapo wanafaa kushikilia wadhifa wao, kutegemea habari zinazowahusu kutoka kwa Idara ya Mkuu wa Sheria, Chama cha Wanasheria, Jaji Mkuu, Kitengo cha Polisi cha

Kukabiliana na Ufisadi na Mamlaka ya Kupambana na ufisadi (KACA) iliyokuwapo zamani.

- Majaji wote watakaobaki watapimwa kwa misingi ya Katiba mpya na kanuni ya uongozi na wale wasiohitimu watafutwa kazi.

8. Mambo Mengine Kuhusu Mfumo wa Sheria

Majaji si kiungo cha pekee cha mfumo wa mahakama unaotenda kazi. Katiba iliyopo ina upungufu kadhaa kuhusiana na hoja hii. Tume inapendekeza hatua zifuatazo zinazolenga kuimarisha uhuru wa mfumo wa mahakama:

- Mkurugenzi huria wa mashtaka ya umma.
- Mlinzi wa Umma – afisa wa kikatiba asiyeegemea upande wowote atakayetoa usaidizi wa kisheria kwa yeyote anayekumbana na kesi ya jinai au uhalifu kwa mara ya kwanza.
- Masharti ya Katiba ya kuunda sera ya mashtaka – na hii ni lazima itangazwe kwa watu wote. Uwezo wa kushtaki (au kutoshtaki) ni muhimu sana. Wananchi wanapaswa kujua mwelekeo utakaochukuliwa na mamlaka kuhusu uhalifu. Wanapaswa pia kujua hatua itakayochukuliwa dhidi ya watu muhimu kisiasa.
- Mashtaka ya kibinafsi yaendelea kukubaliwa (kuidhinishwa na mahakama).
- Uwezo wa kutupilia mbali mashtaka (nolle prosequi) (alio nao Mkuu wa Sheria hivi sasa wa kuchukua mashtaka yaliyowasilishwa na wengine na kuyatupilia mbali) irekebishwe kwa kuihitaji mahakama kuidhinisha matumizi yake.
- Kamati huru kuamua iwapo msamaha au kutupiliwa mbali kwa mashtaka kutatekelezwa, na kamati hiyo inapasa kumpendekezea Rais anayepaswa kutekeleza pendekezo linalotolewa.

9. Mfumo wa Kuadhibu

Ni wazi kabisa kutokana na mawasilisho ya umma kwamba mambo katika mfumo wa kuadhibu si mazuri. Udhalimu wa polisi umeghusiwa katika kijitabu cha Haki za Binadamu, kama vile lilivyo suala la haki za wafungwa. Suala la kuwataka polisi kuwa na uwajibikaji pia lilijadiliwa. Tume inafahamu kuwa ripoti za hivi karibuni zaonyesha kuwa sera ya kuunga mkono jela badalia – hasa huduma kwa jamii – inaanza kutoa matunda kupitia kupunguka kwa idadi ya wafungwa. Hii ni hatua inayopasa kukubalika na mahakama kupongezwa kwa kuwa tayari kubadilika kutegemea mahitaji yaliyopo. Tume ilipokea idadi kubwa ya maoni kuhusu hukumu inayotolewa kwa wahalifu wakuu – hasa makosa ya ngono. Kuna malalamishi kama hayo katika mataifa mengi. Vilevile, wakati mwingine kutoa hukumu kutegemea malalamishi ya umma husababisha hukumu kali zaidi kutolewa. Hii inaweza kwenda kinyume na Katiba kama kutozingatia kanuni ya kimsingi ya kuwapo kwa usawazisho, kati ya kosa na hukumu inayotolewa (ingawa hii inaweza kuwa haipo kwenye Katiba). Pili kulazimisha hukumu nyepesi ambazo ni kali mno kunaweza kuzifanya mahakama zisitoe hukumu ikiwa hazina budi kutoa hukuma inayochukuliwa kuwa si ya haki. Shinikizo za kukabiliana na

uhalifu pia zinaweza kusababisha kutumiwa kwa sheria kali kama zile za Marekani za "kutimuliwa baada ya makosa matatu". Hatua kama hiyo pia inaweza kuchukuliwa kwenda kinyume na Katiba, na pia inaweza kufanya magereza kujaa zaidi na kushindwa kutekeleza majukumu yake ya kimsingi. Vilevile inatokea mara nyingi sana kwa mahakama kutoa hukumu tofauti kabisa kwa makosa yanayofanana. Aidha, kwamba watu kutoka matabaka tofauti ya kijamii hushughulikiwa kwa njia iliyo tofauti na mahakama. Mojawapo ya suluhisho la matatizo haya linalotumiwa sasa na mataifa mengi ni kuunda Baraza la Kutoa Hukumu, linalotoa utaratibu au kanuni zinazofuatwa na mahakama. Tatizo jingine la kikatiba limekuwa kwamba, katika mataifa mengine, sheria inatoa fursa yao kuhusishwa kwa waathiriwa. Inapendekezwa kwamba ili kufanikisha kuundwa kwa sera za kuhukumu zilizo thabiti na zisizokinzana na Katiba, utaratibu kuhusu yafuatayo unaweza kuzingatiwa:

- Sheria inayohusu hukumu na utekelezaji wake inapasa kulenga kuafikia malengo yafuatayo:
    - Usawazisho kati ya kosa na lawama anayopasa kupata mkosaji.
    - Kukosekana ukinzano kati ya mahakama na makosa.
    - Kuambatana na hali au muktadha halisi alimokuwa makosaji.
    - Kurejeshwa kwa haki za waathiriwa.
    - Kuulinda umma.
    - Kumrejesha mkosaji kwa jamii pakiwa na uwezekano mdogo zaidi wa kurejelea tena makosa aliyofanya.
- Ili kufikia malengo haya, ni lazima taifa liunde halmashauri ya kuunda taratibu za kutoa hukumu.

10. Huduma kwa Umma, Polisi na Jeshi la Ulinzi

a.) Huduma kwa umma

Huduma kwa umma ni sehemu muhimu sana ya mfumo wa serikali katika taifa lolote lile, na huduma hiyo bado si wazi kwa umma, wanaofahamu polisi, shule na hospitali, lakini ambao kwa kawaida ni nadra kwao kukutana na wahudumu wengine wa umma na kufahamu kazi yao japo kijuujuu. Huduma kwa umma iliyo thabiti, iliyosawazishwa na iliyo huru kutokana na kuingiliwa kati kisiasa ni muhimu kwa utoaji wa huduma kwa umma, uundaji wa sera na kwa umoja wa taifa na uhuru. Watu wengi wanakumbana tu na serikali kupitia wafanyikazi wa umma; na ikiwa watatambua mabadiliko yoyote, ikiwa mabadiliko yatatokea, baada ya Katiba mpya, itakuwa ni kupitia sekta ya Huduma kwa Umma.

Muundo na utendakazi wa viungo mbalimbali vya huduma kwa umma, na mwingiliano wake na sehemu nyingine za mifumo ya kiserikali na kisiasa, na pia umma, ni muhimu katika kufikia malengo mengi ya utaratibu wa marekebisho; utawala mwema (s.3(b)), uwajibikaji (s.3(c) na s. 17(d)(i)), kushiriki kwa umma (s. 3(d)) na vipimo na visawazishi (s. 17(d)(i)) pamoja na, kutimiza mahitaji ya kimsingi ya watu (s. 3(f) na kuimarisha umoja wa taifa (s.3 (h)).

Mawasilisho kwa Tume pamoja na duru nyingine zaonyesha kuwa huduma kwa umma ina matatizo mengi zaidi. Baadhi ya matatizo hayo yanaweza kuhusishwa na huduma yenyewe, na mengine kuhusishwa uingiliaji kati kisiasa.

- Utafiti wa kitengo cha Polisi cha Kukabiliana na Ufisadi ulionyesha kuwa asilimia sitini ya (60%) ya Wakenya wamewahi kuathiriwa na ufisadi, na kwamba asilimia hamsini (50%) kati yao walitoa hongo ili kuhudumiwa na mfanyikazi wa umma.
- Waliohitaji kuhudumiwa na maafisa wa uhamiaji wamelalamika kuwahusu.
- Barabara zinahitaji kuwepo, lakini hakuna barabara zinazofaa kuitwa barabara.
- Huduma katika hospitali za umma ni ya kusikitisha
- Kuna shule ambazo hazina madawati na viti, na ambazo paa zake huvuja
- Katika kiwango cha serikali za wilaya watu hulipia huduma za kuokota taka, lakini taka hizo haziokotwi.
- Mashirika ya serikali yameporomoka, na hivyo kutatiza biashara na kilimo vilivyokuwa vikiyategemea.
- Baadhi ya viwanda vimebinafsishwa kwa kuuziwa watu ambao nia yao kuu ilikuwa kunyakua rasilmali.
- Watu walisema mara nyingi kuwa matatizo yanayokumba huduma kwa umma yanatokana na uamuzi wa kuwaruhusu wafanyikazi wa umma kufanya biashara.
- Mtu mmoja alipendekeza kuwa wafanyikazi wa umma wanapaswa kuwa na sare rasmi.

Matatizo hayahusiki tu na huduma inayotolewa kwa umma. Kuna pia matatizo makubwa kuhusu uteuzi na shughuli za ndani za huduma kwa umma.

- Inafahamika kuwa waalimu wana malalamiko makubwa kuhusu jinsi swala la mishahara yao lilivyoshughulikiwa, na pia kuwa ni kweli kwamba wanalipwa vibaya.
- Hali ni vivyo hivyo kwa polisi.
- Kuna ufisadi, ubaguzi, na upendeleo wa ndugu katika utaratibu wa uteuzi.
- Kwa ujumla, utaratibu mzima unaonekana kukosa uwazi.
- Kupandishwa cheo wakati mwingine ni kwa mapendeleo
- Uchekechaji umetekelezwa ‘bila kuzingatia ubinadamu.’

Katika kuitikia mapendekezo kutoka kwa umma Tume inapendekeza mabadiliko kadhaa. Kwa kiwango fulani mapendekezo haya yanatokana moja kwa moja na baadhi ya mapendekezo yaliyotolewa katika muundo wa serikali; Rais atakuwa na uwezo uliopunguzwa zaidi ya hivi sasa. Lakini hii si kwamba uwezo huo utaondolewa tu mikononi mwa Rais na kukabidhiwa

wanasiasa wengine kama vile Waziri Mkuu na Bunge. Mapendekezo katika mswada wa Katiba yanajumuisha:

- Tume ya Huduma za Umma pia utawajumuisha walimu na polisi, itakuwa huru zaidi na kuangazia zaidi uhalisia wa jamii.
- Tume ya Huduma za Walimu itaingizwa katika Katiba
- Uhuria wa Tume hizi utasisitizwa katika Katiba
- Mapendekezo ya kuundwa kwa Tume ya Haki za Binadamu na za Kiutawala na Haki ya Utawala wa Haki, yaliyotolewa katika mswada wa Katiba pia ni muhimu.

Kuna utaratibu unaotekeleza wazi wajibu wa kimsingi wa huduma kwa umma:

- Huduma zitatekeleza majukumu yake kuambatana na Katiba na sheria.
- Zitalinda haki za wananchi.
- Zitahakikisha utawala wa haki.
- Zitateuliwa kutegemea ubora.
- Uteuzi utazingatia kanuni ya usawazisho kutegemea unuwai wa jamii ya Wakenya
- Katika viwango vyote angalau theluthi moja ya wanaoteuliwa wawe wanawake na angalau theluthi moja wanaume (na marupurupu ya uhitaji wa haja kutegemea gredi na taaluma) na Tume ya Huduma za Jamii itajitahidi kuzingatia na kudhihirisha kanuni hii katika kupandishwa vyeo.
    - Tume ya Kuajiri lazima ihakikishe kuwa huduma za umma ni za kitaalam na za kuwajibika na kuchunguza kwa uaminifu masharti yao ya sheria na ya kanuni zinazohusika za maadili.
    - Watumishi wa umma wasiadhibiwe kwa kufanya kazi zake chini ya Katiba pamoja na kulalamika au kuripoti maswala au hoja kwenye vyombo vya walalamishi ama kwenye Tume ya Haki za Binadamu
    - Huduma za Umma ifanye kazi katika msingi ambapo mwananchi anaelewa ni nani anayeshughulika naye anapokuwa na tatizo lake maalum.

Baada ya muda fulani idhini ya kuwaruhusu watumishi wa umma kujihusisha katika biashara lazima iondolewe. Ni wazi kuwa watumishi wa umma lazima walipwe vizuri. Kuna Tume Maalum iliyoundwa kushughulikia mishahara ya watumishi wakuu wa umma, pia kuna mahakama ya kushughulikia maafisa wengine wa umma.

b.) Huduma za Usalama

Huduma za Usalama ni pamoja na Polisi, Polisi wa Utawala, Jeshi la Ulinzi: jeshi la wanamaji, jeshi la wanahewa na kikosi cha upelelezi. Pia kuna hudumu za wanaovaa sare: Huduma za Askari wa Magereza, huduma nyingine za Askari wa Forodha na kisha kuna Vijana wa Huduma kwa Taifa. Viungo hivi havionekani sana katika Katiba iliyopo sasa. Rais ndiye huteua Kamishina wa Polisi (Kifungu cha Sheria Na 108) ambapo maafisa wengine

wakuu huteuliwa na Tume ya Umma ya Kuajiri (PSC). Mbali na kifungu kinachotangaza Rais kuwa Amirijeshi Mkuu (Kifungu cha Sheria Na 4) hakuna masharti mengine ya jumla kuhusu vikosi vya ulinzi, sheria yoyote ambayo kwayo vinarekebishwa na Bunge la kawaida, ila kwa sharti moja kuu linalozuia kuchukuliwa kwa hatua za kinidhamu chini ya sheria na heshima kwa jeshi la ulinzi; polisi, askari magereza, na hata Vijana wa Huduma Kwa Taifa linalopingwa kwa mujibu wa baadhi ya masharti ya haki za binadamu (Kifungu cha Sheria Na 86(2)). Hii ni hali tofauti kabisa na ile iliyotokeza wakati wa uhuru. Katika mwaka 1963, Katiba ilitaja wazi wazi kwamba jeshi la polisi liundwe kisheria . Kulikuwa na Tume ya Huduma za Polisi tofauti (Kifungu cha Sheria Na 160). Kulikuwa na Baraza la Usalama la Taifa (lililokuwa na Waziri; Mwenyekiti wa kamati ya Sheria na Amri ya kila Baraza la Kieneo) ili kuhifadhi marekebisho ya masuala ya mpango, usimamizi na utekelezaji wa Jeshi la polisi (Kifungu cha Sheria 157) Inspekta Mkuu wa Polisi (sawa na Kamishina) aliteuliwa na Mkuu wa Serikali kufanya kazi kwa mapendekezo ya Tume ya Huduma za Polisi (Kifungu cha sheria 162). Gavana Mkuu alikuwa Amiri Jeshi Mkuu, lakini hiki kilikuwa hasa cheo staha kwa sababu alitekeleza kazi zake zote kwa ushauri wa Baraza la Mawaziri au Waziri (Kifungu cha Sheria 79).

Mawasilisho mengi kwa Tume yalihusu jeshi la polisi. Haya yalihusiana zaidi na ukatili pamoja na ufisadi.

- Moja kati ya hoja za mara kwa mara katika maoni zilihusu ukatili wa polisi
- Katika uchunguzi wa hivi karibuni wa Shirika la Uwazi la Kimataifa (Transparency International, Kenya) polisi walikuwa wa kwanza (juu zaidi) katika ulaji rushwa nchini.
- Watu waliotoa maoni kwa Tume, walisema kwa mfano polisi humkamata mtu ijumaa bila sababu yoyote maalum wakitegemea kuwa kuwekwa kwake korokoroni wikendi nzima kungeleta hongo kubwa.
- Kuna wazo kuwa polisi watapuuza wakati raia wanapotishwa – mfano halisi ni pale ambapo Kitengo cha Huduma ya Jumla (General Service Unit - GSU) iliposhindwa au lilipokataa kutokeza mara moja kuwasaidia watu walipokuwa wakiuawa na Mungiki huko Kariobangi ambako ni karibu sana na makao Makuu ya GSU.
- Kuna baadhi ya maafisa wa polisi wanaohusika katika shughuli za uhalifu – kama vile kuteka nyara magari au ujambazi.
- Watu walipendekeza kwamba majeshi yatumike katika shughuli za maendeleo – kama vile ujenzi wa barabara, jinsi inavyofanywa katika nchi zingine na ilifikiriwa katika Mradi wa Kupunguza Umaskini.
- Polisi, hasa Polisi wa Utawala, wanatumiwa na wanasiasa kwa maslahi ya vyama vya kisiasa.

Kanuni zifuatazo (zimetolewa kwenye Katiba za mahali pengine, pamoja na nyaraka zinazohusiana na udhibiti wa uwazi kwa mujibu wa majeshi ya usalama) zinaweza kutumika kwa jumla na jeshi la usalama:

- Kutofungamana na pande zo zote kisiasa
- Udhibiti wa raia
- Kutoegemea upande wowote kisiasa
- Kudhibiti raia
- Kuheshimu kanuni za sheria, demokrasia na haki za binadamu
- Uwazi na uwajibikaji
- Kuongozwa na sheria
- Jeshi la ulinzi pekee
- Kutotii amri isiyo ya kisheria
- Kujihusisha na vitendo vya kuleta manufaa kiuchumi
- Kulinda uhuru na kusaidia katika dharura
- Kuwa na nidhamu na uzalendo

Hali za usimamizi wa kiraia zitatofautiana kulingana na wajibu wa jeshi. Lakini kiwango fulani cha usimamizi hutokea katika huduma zozote na hupatikana katika sheria na Katiba za nchi nyingine- hata kuhusu huduma za usalama. Kwa hakika, kuna mifano ya usimamizi wa kiraia nchini Kenya, ama kupita sheria (kama vile kikosi cha upelelezi) an kwa vitendo (ilivyo kwa jeshi la ulinzi).

Hasa kulingana na polisi, Kanuni za Maadili za Umoja wa Mataifa ni pamoja na:

- Utumiaji wa nguvu lazima usawazishwe kulingana na hali ilivyo sasa.
- Utumiaji wa silaha uwe tu mahali inapobidi kuwa lazima kutumia.
- Kujali afya za walio kizuizini.
- Kuepuka ufisadi.
- Kushukua hatua kwa wanaowakosea wengine.

Tume inapendekeza katika mswada wa Katiba kuwa hatua zifuatazo zichukuliwe kuhusiana na matumizi mbalimbali ya nguvu za jeshi la usalama:

- Maelezo ya maadili na kanuni zinazohusu majeshi yote ya ulinzi
- Maelezo maalum kwa kila huduma kupanga kanuni zake na wajibu wa kikatiba
- Taarifa za maadili na kanuni kuhusu kwa majeshi yote ya ulinzi
- Taarifa maalum kwa kila huduma kuelezea kanuni zake na wajibu kiKatiba
- Huduma kuu zimepewa majina mapya:
    - Huduma ya Polisi wa Kenya
    - Majeshi ya Ulinzi
    - Huduma za Adhabu
    - Jeshi la Polisi wa Utawala liache kuwa jeshi linalojitenga pekee.
- Mifumo ifuatayo ya ukaguzi wa Kiraia:
- Kwa jeshi la Polisi
    - Utawala kwenye ngazi ya kitaifa inayokuwa na Bodi/Tume yenye wabunge na waheshimiwa wanachama wa shirika

- Ambayo utashauri na kuhimiza polisi kwenda karibu zaidi na kuchanganyika na raia au jamii, viwango vya juu n.k. uwazi, kiwango kiasi cha sera (ambacho ni wajibu wa Serikali) na usimamizi wa kila siku na kufahamisha Bunge.
- Vyombo vya wilayani vinavyofanya kazi sawa na na kufahamisha Baraza la Wilaya.
- Kamati za mawasiliano katika kiwango cha mashina zinazohusu viongozi wa kijamii, wanawake na makundi yaliyoathiriwa.

- Kwa ajili ya Majeshi ya Ulinzi
  - Sheria zitateua chombo au vyombo vya kuishauri Serikali kuhusu masuala ya ulinzi, kuunda kanuni muhimu, kuajiri n.k
  - Kamati ya Bunge yenye wajibu masuala ya ulinzi lazima ichunguze bajeti ya jeshi la ulinzi, irekebishe sheria zilizitungwa kuhusu jeshi la ulinzi, ipokee ripoti za kila mwaka kutoka kwa jeshi la ulinzi n.k.

- Kwa Huduma ya Upelelezi
  - Sheria iliyotungwa lazima izingatie kuwepo kwa kamati ya Wabunge, bila kuwahusisha Mawaziri, pamoja na wanachama wa Serikali na upinzani na ambayo itachunguza kazi ya huduma za upelelezi na bajeti yake, na kufahamisha bunge. Sheria lazima izingatie kuwepo kwa ushirikiano mkubwa baina ya huduma za upelelezi na Kamati, na kuweka siri inapotakikana
  - Sheria lazima izingatie utaratibu huru wa kupokea malalamiko

Mabadiliko mengine yatakuwa muhimu katika mfumo wa kuajiri na utaratibu wake, hasa kwa ajili ya polisi. Mswada wa Katiba una kanuni kwa ajili ya haya na kwa ajili ya matumizi kamili, pamoja na mafunzo ya polisi, na kutoa kwa wananchi kanuni za utendaji. Kutakuwa na chombo cha walalamishi kama sehemu ya Tume kuhusu Haki za Binadamu na Haki za Utawala.

Tena inapendekezwa- na ni wazi kuwa- mbali na majeshi/huduma zilizotajwa hakuna majeshi mengine ya ulinzi yatakayoanzishwa. Mswada wa Katiba pia unahitaji kupitisha sheria ya kusajili kampuni za usalama, kubainisha malengo yake, na kuweka baadhi ya vigezo kuonyesha ni nani awezaye kuajiriwa kama mlinzi wa usalama.

SURA YA NNE

UKATIBA

Sura hii inajaribu kujibu maswali haya kwa kupendekeza asasi na taratibu za kufuata:

- Kwa kuzingatia wepesi na mapana ya mabadiliko Katiba ya 1963 ni vipi inavyoweza kuzuia katiba mpya isipatwe na tukio kama hilo?
- Tunaweza kuzuia vipi uharibifu wa asasi za kiKatiba na vyombo vya serikali unavyotokea kwenye asasi hizo kupitia Katiba iliyopo?
- Tunawezaje kuwa na hakika kwamba mabadiliko yanayoletwa na Katiba mpya yatatekelezwa?
- Tutahakikisha vipi kuwa uwezo unaotolewa chini ya Katiba mpya hautapuuzwa?
- Tutafanya nini ili mawaziri na watumishi wa umma wawajibike kisiasa katika vitendo vyao?
- Ni vitulizo vipi vitakavyopewa watu wakivunjiwa hak zao?
- Tutakuwa na hakika gani kuwa majaji watatafsiri au watafafanua na kuamua kesi bila upendeleo?
- Tutahitaji kufanya nini kuhakikisha kuwa tuna uchaguzi huru na wa haki?
- Tutalinda vipi thamani za kiKatiba kama vile kuwaza, kushiriki kwa watu, uhuru na rasilmali a afisi za kikatiba na mashirika?
- Tutaondoaje ufisadi ambao ndicho chanzo cha kunyimwa haki nyingi na ndiyo sababu kuu ya ufukara au umaskini wetu?

Sheria ya Marekebisho inahitaji Katiba mpya iliyo na masharti yafuatayo ambayo ni nyenzo za kuanzisha na kuhifadhi “uKatiba”.

- Mtindo wa kuhifadhi sana ukatiba na utawala wa (kifungu cha Sheria 3 (b))
- Kupunguza na kusambaza, na vipimo na visawazishi ‘kuhakikisha uwajibikaji wa Serikali na maafisa wake kwa wananchi wa Kenya (Kifungu cha Sheria 3(c))
- Ushirikishaji wa watu (kifungu cha sheria 3 (d))
- “Kuchunguza na kupendekeza uboreshaji wa Tume zilizoko za kiKatiba, asasi na afisi na uanzilishi wa ziada, kuboresha utawala wa kiKatiba na heshima kwa haki za binadamu na usawa wa kijinsia kama usioepukika na sehemu muhimu sana ya mazingira yafaayo kwa ajili ya maendeleo yakiuchumi, kijamii, kidini, kisiasa na kitamaduni” (Kifungu cha sheria 17 (d) (iii))
- Kutoa mapendekezo kuhusu mahakama kwa jumla na hasa, uanzilishi wake na mamlaka yake, ili kuweka ya mahakama, kulenga vipimo muhimu vya kuhakikisha uwezo, uwajibikaji, utendaji bora wa kazi,

nidhamu na uhuru wa mahakama ya kisheria (Kifungu cha Sheria 17 (d) (v)).

Vyombo vya kulinda thamani na masharti ya kikatiba ni pamoja na:

- Kuhitaji kwamba utumiaji wa aina fulani wa madaraka ya serikali yenye uwezo juu ya utumiaji wa haki na mfumo wa kisiasa na mtindo wa kiutawala kama vile kutekeleza sheria, kuajiri watumishi wa umma, sera za fedha na kanuni za uchaguzi, sharti zizuliwe kutoka kwenye ushawishi wa kisiasa. Hii itatimizwa kwa kuzipatia uwezo asasi huru na Tume.
- Kuyapa mahakama uwezo wa kurekebisha na kutangaza sheria au sera zisizo za kikatiba na kuzitupilia mbali.
- Kuongezea mahakama asasi nyingine kwa ajili ya kupokea, kupeleleza na kuyashughulikia malalamiko ya umma dhidi ya utawala, maana ni vigumu kufikia mahakama na ni ghali na utaratibu wa mashtaka ya sheria huchukua muda mrefu.
- Pamoja na mwelekeo uliotangulia ni kuunda asasi za "shughuli zote" kwa minajili ya kulinda haki za kila mtu au za kikundi fulani maalum cha watu (kama vile wanawake). Asasi hizi zitapokea na kupeleleza malalamiko, lakini pia kuimarisha elimu na heshima kwa haki za binadamu na kutoa kanuni za kudumisha haki.
- Kuanzisha asasi za kuhakikisha uwajibikaji wa mamlaka ya umma, zitakazochukua hatua, bila kungojea malalamiko kutoka kwa umma. Anayejulikana zaidi hapa ni Mhasibu Mkuu mfano wa hivi karibuni ni vyombo vya kupambana na ufisadi.
- Kuanzisha mfumo huru wa kisheria imara na wenye nguvu na imara, kwani ni kupitia kanuni za sheria pekee ambako utumiaji wazi mbaya zaidi wa uwezo unaweza kuzuiliwa. Mfumo unaofaa wa kisheria unahitaji Mkuu wa Sheria, ambaye ni kiongozi wa mfumo wa sheria na mashauri mkuu wa kisheria serikali, awe huru. Pia huhitajika mfumo huru wa mashtaka. Huhitaji mtaalamu wa kisheria mwenye nguvu na uwezo wa utendaji. Ili kuwawezesha watu kutafuta msaada wa mahakama kuimarisha haki zao, msaada wa kisheria lazima utolewe kwa wanaouhitaji.
- Mwisho, lazima watu wawe walinzi wa Katiba. Na kutekeleza kazi hii ni lazima watu waielewe Katiba na kujua haki zao. Lazima wajue jinsi ya kutumia utaratibu Katiba na sheria ili kufanya mamlaka ya Umma kuwajibika. Pia wafanye kazi kama wakala wa uwajibikaji Kwa mfano, kwa:
    - Kutoa bajeti badalia au uchambuzi wa mswada wa bajeti ya serikali
    - Kuchapisha ya tathmini za mwaka rekodi za serikali na mashirika ya haki za binadamu, haki za kijamii, mazingira na mifumo ya maliasili n.k.
    - Kutoa ripoti badalia kwa wasimamizi wa kimaeneo na kimataifa wa haki za binadamu kuhusu rekodi ya kitaifa

- Kuanzisha mashtaka ya kikatiba ili kuzuia serikali au watu binafsi kutoka na kukiuka Katiba au sheria.
- Kwa kuwa kila mtu anafanya kazi na wengine, jukumu ambalo mashirika ya umma na yasiyo ya kiserikali yanaweza kutekeleza wakati mwingine hutambuliwa na kulindwa na Katiba, kama vile ilivyo huko Ufilipino.

Rasilimali muhimu kwa shirika la umma ni kupata habari iliyokusanywa, iliyoagizwa an iliyohifadhiwa na mamlaka ya umma – Nchi nyingi zinahusu kupatikana huku.

1. Mambo Ambayo Wakenya Waliiambia Tume

Baada ya kuona Katiba ya 1963 ilivyohasiwa na mfumo ulioanza punde tu nchi ilipopata uhuru, Wakenya walionyesha nia yao za kutoa maoni kwa Tume kuwa Katiba mpya isibadilishwe juu juu tu, na pia sharti iheshimiwe.

- Moja katika mfululizo wa maoni yalikuwa ni kuhusu Mpokeaji malalamiko – afisi ambayo kwayo wananchi wanaweza kwenda kulalamika kuhusu wanavyotendewa na huduma za umma, bila kulipa ada, nayo itapeleleza malalamiko na kutoa maoni kwa kurekebisha hali na kuleta haki na kuboresha huduma kwa umma baadaye.
- Wanawake walitaka Tume ya Jinsia – ambayo itapokea na kupeleleza malalamiko kutoka kwa wanawake kuhusu kupuuzwa kwa haki zao, na sheria na sera ambazo zina madhara kwa wanawake.
- Mawakili wa watoto walitaka Tume ya Watoto.
- Makundi mengi yalitaka Tume Huru ya Haki za Binadamu. Watu waliolalamika juu ya Polisi walitaka Tume ya Malalamishi ya Polisi.
- Wengine walitaka Tume ya Ufisadi (Kama Tume ya Kenya dhidi ya na Ufisadi ambayo mahakama ilitangaza kuwa haikuundwa kiKatiba mwaka 2001).

Itakuwa wazi kwamba kutakuwa na imani katika uadilifu au wema wa vyombo huria vya kuchunguza malalamiko. Pengine pia itaonekana kuwa kuna hatari ya kuundwa kwa tume nyingi. Hakuna kitu kati ya hivi kitakachofanyika bila gharama na baadhi ya mambo utekelezaji na kazi zitafanana miongoni mwa tume mbalimbali.

Pia kuna shughuli nyingine zitakazohitaji uundaji au idhinisho wa tume: kuendesha uchaguzi ni mfano wazi ambao utaendelea kuwa kazi ya Tume ya Uchaguzi. Nyingine ni Mkaguzi Mkuu wa Fedha za serikali: anaweza kusikika kama mtu binafsi lakini kwa ukweli afisi inahitajika watumishi wengi na kazi nyingi kama tume.

Tajriba au uzoefu wa Uganda na Afrika Kusini hutuonya dhidi ya kuwa na asasi nyingi huria. Ni ghali, ni vigumu kuzitafutia pesa, na si rahisi kuzipa watu wenye ujuzi muhimu wa kuzihudumia. Kazi zao huingiliana; hii ni

rahisi kuleta mkanganyiko miongoni mwa pande mbili za umma ambao ungekuwa na tashwishi kuhusu uhakika wa mahali pakupeleka malalamiko yao (kwa mfano, je kitendo cha afisa wa umma kinachoonyesha ubaguzi dhidi ya wanawake kiwasilishiwe Tume ya Jinsia au Tume ya Haki ya Binadamu? Na maafisa pia huenda wakatatizika – tume mbalimbali huenda zikawa na taratibu tofauti kushughulikia masuala sawa. Na, kwa bahati mbaya, ni vigumu kujiepusha na mashindano baina ya tume, hasa ikiwa kazi zaidi italeta rasilimali bora.

2.) Vyombo Vya Kikatiba Vilivyopendekezwa

Kwa hivyo tunapaswa kuzuia idadi ya asasi mpya. Tume ya Marekebisho ya Katiba ya Kenya (CKRC) inapendekeza vyombo vifuatavyo, vingine vikiwa vipya:

a.) Tume Mbalimbali za Huduma

- Tume ya Huduma ya Umma
- Tume Ya Huduma ya Mahakama
- Tume ya Huduma ya Bunge
- Tume ya Vyombo vya KiKatiba na Maafisa Wake
- Tume za kikatiba na Tume za kikatiba za huduma za afisini.

Hii inaweza kuonekana kama ukiukaji wa kanuni ya kutokuwa na Tume nyingi, lakini kihalisia baadhi ya vyombo hivi tayari vipo. Maelezo ya kina kuvihusu yanapatikana katika sehemu zinazohusika za ripoti hii.

b.) Tume Ya Haki Za Binadamu na za Kiutawala

Tume hii inaweza kujumuisha majukumu ya mpokeamalalamishi, Tume ya Jinsia/Usawa, Tume ya Haki za Binadamu, na uwajibikaji pamoja na malalamiko dhidi ya majeshi. Muundo wake utakuwa wa "kishirikisho" – kila mwanatume atakuwa na majukumu na rasilimali maalum (pamoja na majukumu maalum) – jinsia, watoto, ulemavu, 'waliowachache', mienendo ya polisi na majeshi, malalamiko dhidi ya utawala, n.k). Asasi zinazopendekezwa kuunganishwa hivi zina majukumu yanayoiniliana. Zina wajibu sawa. Wajibu huu unahusu haki za binadamu; ni pamoja na elimu ya haki za binadamu, uteteaji, ushawishi, kuweka viwango, kupokea na kushughulikia malalamiko, kushauri. Kazi ya mwanzo ya Tume ya Haki za Binadamu na za Kiutawala itakuwa kushughulikia malalamiko ya kusumbuliwa na kudhulimiwa. Manufaa ya mpango huu ni:

- Uchumi
- Uratibu bora
- Kujumulisha rasilimali – maktaba, makao, magari, maafisa wa utafiti
- Kuandaa kituo kamili: mtu mwenye malalamiko au pendekezo hatakosa huduma eti kwa sababu ameenda asasi isiyoshughulikia malalamiko yake (itakuwa ni jukumu la Tume kuelekeza malalamiko kwa tume na kitengo kinachofaa zaidi); kutakuwa na afisi moja ya nyanjani katika kila wilaya

au eneobunge itakuyotoa ushauri na kupokea malalamiko, na kadhalika, na kwa hivyo kuongeza ushirikishaji nchini.

- Ushawishi bora zaidi
- Kuweza kulinda uhuru na rasilimali zake
- Ina maana kuwa majukumu na shughuli hizi zitaanza mara moja pindi Tume itakapoanzishwa – inawezekana kwamba ikiwa kutakuwa na Tume nyingi, baadhi zitachukua muda mrefu kuazishwa (kama ilivyo katika mataifa mengi).

c.) Tume ya Maadili na Uaminifu

Chombo hiki kinapendekezwa ili kushughulikia masuala nyeti na magumu yanayohusiana na ufisadi na uaminifu katika maisha ya umma. Tume hii itahusika na utekelezaji madhubuti wa Kanuni ya Maadili ya Uongezi. Kanuni ya Maadili itatokana na ushauri wa vyombo vingine, pamoja na Tume ya Haki za Binadamu na za Kiutawala. Tume itakuwa pia na wajibu wa kushughulikia madai ya ufisadi – utakaokuwa uvunyaji wa kanuni za Maadili ya Uongozi na Sheria ya Jinai.

Kutakuwa na maingiliano yasiyoepukika baina ya Tume hii na Tume ya Haki za Binadamu, na utaratibu wa uratibu italazimu utayarishwe baina ya tume zote mbili. Zote zitapokea malalamiko kutoka kwa wananchi na zitakuwa na wajibu muhimu wa kuelimisha wananchi na wahudumu wa jamii. Lakini Tume ya Haki za Binadamu na za Kiutawala itahitaji mtindo wa upatanisho katika utendakazi wake, ikizuia mtafaruku baina ya wananchi na huduma ya umma na baina ya Tume yenyewe na huduma ya umma. Mtindo wa kufanya kazi wa Tume ya Maadili na Uaminifu utakuwa tofauti. Kanuni ya Maadili ya Uongozi itawahitaji viongozi wa siasa na wahudumu wa umma wa aina mbali mbali, katika kiwango cha juu, kutangaza rasilimali zao. Na itachunguza madai ya makosa makubwa ya jinai. Ni vigumu kutekeleza wajibu huu kupitia mtindo wa kiupatanishi. Patahitajika uwezo wa hali ya juu wa kuchunguza; patahitajika uweza wa hali ya juu wa kuweka siri; na shughuli za Tume ya Maadili ya Uongozi na Uaminifu huenda zikakabiliwa na hasira za wanasiasa na watumishi wa umma. Vyombo vingine ulimwenguni vinavyojumuisha mtindo wa shughuli za ‘mpokeamalalamishi’ na mtindo wa shughuli za uchunguzaji wa ufisadi mara kwa mara vimegundua kuwa mtindo wa uchunguzi wa ufisadi hushinda nguvu mtindo wa mpokea malalamishi – kupitia muda na rasilimali zinazotolewa, au kwa sababu vyombo vya habari huzingatia zaidi upande wa ufisadi.

d.) Tume Ya Uchaguzi

Hii itaendelea kuwepo ijapokuwa itakuwa ndogo zaidi. Mwenyekiti wake sharti awe Jaji wa Mahakamu Kuu aliyehitimu na wanachama lazima wawe na uaminifu uliothibitika.

e.) Kamati Ya Mishahara na Malipo

Chombo hiki kitateuwa mara kwa mara, kwa mfano kila baada ya miaka minne, kurekebisha mishahara na malipo ya Rais, mawaziri, wabunge, majaji, maafiso wa Kijeshi wenye vyeo vya juu, maafisa wanaojitegemea, wanatume wanaofanya kazi kila siku, na kadhalika.

Tume ya Hazina ya Upunguzaji na Usambazaji Madaraka

Itakuwa na wanachama watatu walioteuliwa na Baraza la Taifa kuwakilisha wilaya, na watatu walioteuliwa na serikali kuu. Itatoa ushauri kuhusu ugawaji wa misaada na usawazishaji wa misaada katika wilaya ambazo hazijaendelea sana.

g.) Tume Ya Katiba

Chombo hiki kitakuwa hasa na jukumu la kusimamia utekelezaji na Katiba, kimejadiliwa chini ya *Mpito*, hapo chini.

h.) Mahakama

Jaji Mkuu na Majaji wa Mahakama ya Juu, Mahakama Kuu (pamoja na Kadhi Mkuu)

i) Mkuu wa Sheria

Atakayetoa ushauri huria wa kisheria kwa serikali na kulinda sheria

j) Mkurugenzi wa Mashtaka

Atakayekata kauli na kuongoza mashtaka bila ushawishi wa kisiasa.

k.) Wakili wa Umma

Afisi hii itatoa uwakilishi wa kisheria kwa watu wasioweza kulipa gharama ya kuwakilishwa kisheria; itagharimiwa na umma; itakuwa na matawi mikoani

l.) Gavana Wa Benki Kuu
Atakayehakikisha usimamizi wa fedha kwa mujibu wa kanuni za kiuchumi.

m.) Msimamizi wa Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fedha

Msimamizi na Mhasibu Mkuu na Afisi ya Taifa ya Uhasibu (na Tume ya Uhasibu)…
Sheria ya majuzi inapendekeza kuundwa kwa Tume ya Uhasibu itakayoshirikisha Mhasibu Mkuu, Wenyeviti wa Kamati za Hesabu za Umma Bungeni, Taasisi ya Wahasibu wa Umma wa Kenya, Tume ya Huduma ya Umma na Mkuu wa Sheria. Chombo hiki kitapitisha makadirio ya Tume ya Uhasibu (ili kuikinga kutokana na mashirika yanayochunguzwa na Tume ya Uhasibu) na kukata kauli kuhusu malipo na kanuni za kazi za maafisa wake.

n) Mhasibu mkuu na Afisi ya Kitaifa ya Uhasibu

Kuhasibu hesabu za vyombo vya umma na kuleta ufisadi na ukiukaji mwingine wa sheria mbele ya bunge na Mkurugenzi wa Mashtaka ya umma.

o.) Mkurugenzi wa Shirika Kuu la Takwimu

Ili kuhakikisha, pamoja na mengine, hesabu ya watu, na ukusanyaji na uchunguzi wa habari nyeti.

p.) Tume ya Ardhi

Chombo hiki kitalinda ardhi kama amana kwa niaba ya wananchi wa Kenya na kuendeleza sera za ardhi ambazo, pamoja na mengine, zitaheshimu kanuni za Katiba.

3. Kanuni Zinazoongoza uundaji wa Tume Huria

Ni sharti kanuni fulani zizingatiwe katika kuunda tume hizi na vyombo hivi (kanuni hizi hazina nguvu sawa kwa vyombo vyote).

- Lazima zihakikishiwe mapato ya fedha
- Ziweze kujitegemea wala sio kuelekezwa na serikali
- Ziwe na usalama wa kipindi cha kazi
- Kila tume isiwe kubwa mno
- Zidhihirishe kuwepo kwa tofauti za jinsia, ulemavu, maeneo, kabila, uchumi, kazi na majukumu ya kitaaluma.
- Ziwe na uwezo wa kufanya kazi zake kwa ujuzi.
- Pawe na utaratibu na mbinu za kuhakikisha kuwa ripoti zake zinachunguzwa na kwamba zinatekelezwa kama ifaavyo.kutekelezwa kama ipasavyo
- Zitoe ripoti kwa wananchi au wawakilishi wa wananchi (bunge).
- Tume teuzi huria zinatzkikana kutoa ripoti kwa wananchi ama kwa wawakilishi wa wananchi (Bunge).

- Ikiwa zinaingiliana na wananchi, sharti ziweze kufikiwa – kimahali, kifedha na katika mtindo wa kufanya kazi.
- Zifanye kazi kwa usawa na kwa kuzingatia haki za binadamu za wale wanaochunguzwa pamoja na wananchi waliowasilisha malalamishi au masuala yao.

4. Rais Kama Mlinzi Wa Katiba

Katiba mpya inapendekeza jukumu jipya la Rais. Badala ya kuwa, kama ilivyokuwa hapo awali, mkuu wa mamlaka ya nchi anayefanya kazi kila siku, jukumu mojawapo muhimu litakuwa udumishaji wa uKatiba. Wadhifa wa Rais ni pamoja na:

- Kurejeshea bunge miswada ya sheria ili yafikirwe upya, pamoja na sababu za kufanya hivyo.
- Kuagiza mahakama kutoa uamuzi juu ya uKatiba wa sheria.

5. Kubadilisha Katiba

Huenda ikaonekana kama kitu cha ajabu kuzugumzia suala la kubadilisha Katiba hata kabla ya kuidhinishwa kwake – hadi hapo mtu akumbukapo wepesi uliokuwepo katika kubadilisha Katiba ya Uhuru. Jambo hili limekashifiwa sana. Tatizo lenyewe ni kwamba ijapokuwa Katiba itapewa wananchi wa Kenya na wananchi wenyewe, hapo baadaye udhibiti wao wa utaratibu wa kutunga sheria hautakuwa wa moja kwa moja. Lakini endapo patakuwa na kanuni inayosema kwamba Katiba haitabadilishwa, vitendo visivyoridhisha vya serikali vitazuiliwa. Hali hubadilika, na Katiba ni chombo cha wakati wake, na ikiwa Katiba haiwezi kubadilishwa, njia ya pekee huenda ikawa ya mapinduzi. Sululisho huenda ni kuweka mpaka baina ya wepesi wa kubadilisha. Mpaka huu si lazima uwe sawa katika kanuni zote za Katiba. Ni muhimu pia kwamba makundi fulani ya watu yawe na haki ya kushauriwa na labda yawe na kura ya turufu katika mapendekezo ya Katiba. Kanuni nyingine za Katiba huenda zikawa muhimu hivi kwamba haifai kabisa kuzibadilisha na nyingine zitahitaji kura ya maoni: upigaji kura ambapo wachaguzi wote watashiriki.

Tume inapendekeza kwamba mabadiliko ya Katiba yafanywe tu na robo tatu ya kura katika kila Ukumbi wa Bunge, ila ikiwa ni kanuni zilizokita zaidi zitakazohitaji pia Kura ya Maoni ili wananchi wote kutoa uamuzi.

SURA YA TANO

MPITO

Katiba mpya inahusu mageuzi makubwa ya kisheria na maisha ya kisiasa nchini. Haiwezekani kutekeleza mabadiliko ya kisheria mara moja, na maamuzi sharti yafanywe kuhusu kasi na ni mambo yapi ya muhimu zaidi.

1. Kudumisha ya Kale

Kwa hakika mambo mengi kuhusu maisha ya Kenya yatabaki vivyo hivyo – hata ya kisheria. Mfumo wa sheria utaendelea. Watumishi wa umma na waajiriwa wengi wanaohudumia wananchi wataendelea kuwa na ajira zao. Watu wataendelea kumiliki kile wanachomiliki isipokuwa kuna kanuni zinazohusu ardhi iliyopatikana kwa njia haramu au "iliyonyakuliwa."

2. Kuleta Mapya

Mambo ambayo huenda yakabadilika kwanza ni yale yanayohusiana na mfumo wa siasa na muundo wa serikali. Kwa kiwango fulani, hii ni kwa sababu huenda kukawa na uchaguzi mkuu mara tu baada ya kuidhinishwa kwa Katiba mpya. Kwa hakika, wananchi wengi wamedai uchaguzi ufanywe chini ya Katiba mpya. Lakini hii inamaanisha si tu mabadiliko ya mfumo wa uchaguzi bali pia mabadiliko katika majukumu ya kisiasa kwa waliochaguliwa.

Mfumo wa uchaguzi utakuwa tofauti na ule uliopo sasa – kwa sababu wapigaji kura itabidi wachague wabunge wa eneo lao, na pia wapigie chama kura. Kwa hivyo, itabidi pawe na fomu mpya za upigaji kura. Wasimamizi wa uchaguzi na wanaohesabu kura itabidi wapate mafunzo. Bunge itahitaji kutoa nafasi kwa wabunge tisini zaidi. Na karatasi ya kupigia kura katika uchaguzi wa Rais itakuwa tofauti.

- lli kuipa Tume ya Uchaguzi muda wa kupanga uchaguzi, Tume inapendekeza uchaguzi ufanywe April 2003. (Hii kwa hakika si kuiongezea Bunge muda kwa mujibu wa Katiba iliyopo).

Vyombo fulani vilivyopo itabidi viundwa upya. Hivi ni pamoja na Tume Ya Uchaguzi, Tume ya Huduma ya Mahakama, na Tume ya Huduma ya Umma.

Tume inapendekeza tarehe mbalimbali za utekelezaji, kutegemea dharura. Tume ya Huduma ya Mahakama ni ya dharura sana – hasa kwa sababu ya pendekezo la uundaji wa mahakama ya Juu na utaratibu wa majaji kuidhinishwa upya.

- Bunge sharti liunde kamati itakayochunguza uteuzi wa kimahakama kama jambo la dharura.

Muundo mpya wa serikali – wenye mamlaka mapya kwa Rais, Waziri Mkuu na kadhalika – utatekelezwa baada ya uchaguzi mkuu wa kwanza chini ya Katiba mpya.

Mfumo wa serikali iliyopunguza na kusambaza madaraka utachukua muda kupanga na tume inapendekeza kwamba iwe inatumika kikamilifu kufikia 2004.

Mipaka ya maeneobunge kwa ajili ya uchaguzi wa taifa ni muhimu kufikiriwa na ikibidi iwekwe upya na kwa wakati unaofaa kwa ajili ya uchaguzi wa 2008. Katiba inapendekeza kuundwa kwa Tume ya mipaka ya kitaifa mwaka 2004. tume hii itatoa mapendekezo juu ya mipaka ya wilaya na maeneobunge.

Maisha ya bunge itakayochaguliwa mnamo 2003 yatakuwa marefu zaidi ya miaka mitano ili kuwezesha kufanywa uchaguzi mnamo 2008 katika wakati unaofaa zaidi wa uchaguzi ambao ni Agosti.

- Tume ya Haki ya Binadamu na za Kiutawala lazima iundwe kufikia 2003

- Tume ya Ardhi lazima iundwe kufikia 2003

Sera zitakazoshughulikia unyanyasaji wa siku za nyuma zitaichukua muda kuandaliwa na hazina budi kuundwa kwa makini. Lakini ugumu na unyeti haupswi kucheleweshe utekelezaji kwa muda mrefu kupindukia.

Baadhi ya tarehe hizi zinaweza kuwekwa moja kwa moja kwenye Katiba. Lakini mipango mingine huenda yakahitaji ulegevu. Lakini watu wanaweza kuhakikisha vipi kwamba taratibu mpya zimetekelezwa kwa muda unaofaa? Tume inapendekeza kuundwa kwa chombo cha kushughulikia hasa jambo hili, nacho ni Tume ya Katiba. Chombo hiki kitaanzishwa baada ya Katiba hii kuidhinishwa. Tume itakuwa na wajibu, pamoja na afisi ya Mkuu wa Sheria na vyombo vingine vinavyohusika katika utekelezaji wa ibara madhubuti za Katiba kwa mujibu wa utaratibu wa kanuni za mpito kwenye Katiba. Itaangalia pia vile Katiba inatekelezwa na serikali na vyombo vingine na kutoa ripoti za mara kwa mara kuhusu maendeleo yake. Itatoa ripoti zake moja kwa moja kwa wananchi na Bunge. Na endapo maendeleo si ya kasi sana, itakuwa na uwezo wa kwenda mahakamani na kupokea uamuzi wa kutotekeleza Katiba – na katika hali fulani uamuzi dhidi ya mtu binafsi aliyeshindwa kufaulisha utekelezaji. Mwanzoni itakuwa na awamu ya miaka mitatu, inayoweza kuongezwa kwa muda wa miaka miwili zaidi.

HITIMISHO

Tume imependekeza Katiba ambayo ni tofauti sana na iliyoko. Inaamini kuwa mabadiliko haya ni muhimu katika kuleta mwelekeo wa umoja wa taifa, maendeleo ya kiuchumi na kijamii, heshima kwa watu binafsi na wanajamii, na haki ya kijamii pamoja na kuzipa nguvu mpya asasi zetu za kitaifa.

Muswada wa Katiba umeandaa ajenda yenye matumaini mengi yasiyotekelezeka mara moja. Jambo la kufanywa kama hatua ya awali ni kuanzishwa kwa mpango madhubuti wa utawala, hasa asasi na maadili yatakayoziongoza. Serikali ya demokrasia, inayoshirikisha na inayojali ni kitu muhimu zaidi ili kufanikisha asasi nyingine zinazopendekezwa. Kwa hivyo tunapendekeza kuwa Katiba, pamoja na mfumo wa uchaguzi, ianze kutekelezwa mara tu itakapoidhinishwa na Bunge. Tunapendekeza kwa dhati kwamba uchaguzi mkuu ujao ufanywe kwa misingi ya Katiba mpya. Ili kuhakikisha kwamba wakati wa kutosha unapatikana kwa ajili ya elimu ya uraia kuhusu Katiba mpya, mfumo mpya wa uchaguzi, na taratibu mpya za utawala kwenye uchaguzi tunapendekeza kuwa uchaguzi mkuu ujao ufanywe mnamo Machi au April 2003. Wakati huu unaafikiana na Katiba ya sasa kuhusu wakati wa kufanywa kwa uchaguzi. Tunatumaini kuwa kongamano la Taifa la Katiba litafikiria na kuidhinisha pendekezo letu.

Inawezekana kuwa baadhi ya watu hawatafurahishwa na idadi na ukubwa wa asasi mpya tunazopendekeza, hasa kwa ajili ya kuongezeka kwa mahitaji ya fedha za serikali. Asasi nyingi mpya tunazopendekeza ni za kuhakikisha kushiriki kwa umma, uwajibikaji wa mawaziri na mamlaka ya umma, utawala wenye uaminifu, na matumizi sawa ya uwezo nyeti wa kisiasa – pamoja na, katika sehemu nyingine, utoaji wa utaratibu wa kuandaa sera zinazoshirikisha, na za kitaalamu, zinazoongozwa na majukumu ya jumla yaliyofafanuliwa na Katiba na kanuni za gharama za utekelezaji. Tunaamini, kwamba mpango huu utaifanya serikali kuokoa fedha nyingi zinazochukuliwa, kinyume na sheria, na watu binafsi, kwamba utawapa watu wetu nguvu mpya, na kufungua nafasi za ajira na shughuli za biashara na kuleta uwekezaji wa kigeni na teknolojia.

Katiba mpya imetoa ahadi nyingi kwa wananchi wa Kenya. Tumeshirikiana nao katika ndoto zao za jamii yenye amani, maendeleo, na inayojali. Tunaamini kuwa Katiba tunayoipendekeza ikitekelezwa vyema, itatimiza ahadi hizi. Tunawasihi viongozi wasivunje matumaini na matarajio ya wananchi.